# KAZI YA MZUNGU

## DAVID NGOCHO SAMSON

MOGAMBI EMPIRE

**Kimechapwa na;**

Mogambi Studios Sumbawanga.

0629077792/0744509465

**Uhariri**

Joseph Kyando

0754588152

**Usanifu kurasa**

David Ngocho Samson

0629077792/07449465

dvdngocho2@gmail.com

**Usanifu Jalada**

Kindo Arts

0746997969

© David Ngocho Samson, 2020

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupigisha chapa, kutafsiri kusambaza au kukitumia kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi.

**ISBN 978-9976-5516-2-4**

**Hii ni kazi ya ubunifu, isichukuliwe kuwa ni uhalisi wa mambo. Majina ya watu, makampuni na mashirika yaweza kuwa ya kweli, lakini humu yametumika tu kinadharia. Siyo kwa uhalisi wake. Ni katika kunogesha tu simulizi hii ya kubuni.**


## RIWAYA NYINGINE KUTOKA KWA MWANDISHI DAVID NGOCHO SAMSON


- **Mheshimiwa The Don**
- **Tineja**
- **Siri Ya Marehemu**
- **Nadhiri Batili**
- **Kikokotoo**
- **Mateka Wa Huba**
- **Hamaniko (mkusanyiko wa simulizi fupi fupi)**
- **Pamela The Bad Seed (Imeandikwa kwa kiingereza)**


Tinoja


SIRI YA
MAREHEMU




Riwaya
KIKOKOTOO


David Samson Ngocho
Nadhiri
Batili


MHESHIMIWA

# KITABU CHA KWANZA

## 1

Miaka miwili iliyokuwa imepita, Masuke aliamua kuondoka kijijini kwao Malonje na kuingia jijini kutafuta maisha kama ilivyo kuwa desturi ya vijana wengi. Alifika jijini Dar es salaam na kufikia kwa dada ake Maimuna ambako kwa miezi miwili alokaa kwake alikuwa akifanya kazi ya kulisha ng'ombe wa tajiri Soud wa Masouud, kabla ya kuamua kuyatafuta maisha huko Zanzibar, kufuatia fununu alizosikia kwa rafikize kuwa huko maisha yalikuwa na uafadhali. Kazi kidogo kipato cha juu! Dada yake alipojaribu kumshauri aangalie kwanza hapo jijini, yeye alikuwa ameshaamua la kuamua. Hakusikiliza na alisisitiza maisha ni kutafuta. Ujira wake kwa bwana Soudi ulimwezesha kuabiri boti ya Azam na kuingia Zanzibar tayari kwa maisha. Hakubahatika kuonana na rafikize waliotangulia huko. Mawasiliano yalikatika walipoondoka Dar na hilo halikumtia wasiwasi bali aliamini wangekutana huko.

Alifikia nyumba ya kulala wageni nje kidogo ya feri ya Zanzibar. Usiku huo akautumia kutafakari. Alijiuliza ni nini angefanya. Alfajiri ya kesho yake, Masuke alijiamsha na kuanza harakati za kuzunguka kuufahamu mji aliofikia. Katika mizunguko hiyo ndipo alipopata

wazo la nini cha kufanya. Angeweza kusukuma mkokoteni wenye mizigo ya abiria kwa ujira mdogo mdogo ambao kwa kutwa nzima ungemudu kumpa hela ya kujikimu. Wakati akitafakari hayo, alimuona ustadhi mmoja mwenye kuvalia kanzu na barakshia kama ilivyo kawaida ya wazanzibar wengi. Masuke alimsogelea na kumsabahi

‘Asalam aleikum sheikh!' Masuke alitoa salam

‘Aleikum msalam! Wa bara weye!’ Alijibu ustadhi na kuuliza kwa lafudhi yake ya kizenji, Ilikuwa dhahiri kuwa sheikh yule alitanabahi kuwa Masu alikuwa mtu wa bara, na sio bara TU,bara huko nyikani na sio Pwani.

‘Naam sheikh na kazi yangu kubeba mizigo kwa ujira kidogo tu!’ Masu alilazimu kujinadi. Biashara matangazo ati.

Ustadhi alimtazama na bila shaka akaona imani.

‘Mizigo yenyewe mizito utaiweza weye?’

‘Naam sheikh, hii indo kazi yangu!’ Alizungumza kwa kujiamini.

‘Sawa, kwa mizigo hii utanitaka nikupe pesa ngapi?’

‘Mia tano tu itanifaa sheikh wangu!’

‘Haya basi, nipelekee hii kwenye ofisi hiyo ya Azam!’

Ni kama hakuamini bahati aliyokuwa nayo. Tayari ndoto zake alihisi zingetimia hapa. Kufikia magharibi, masuke alikuwa kamudu kujipatia buku nane. Hakutarajia. Sasa aliporejea pale guest alipofikia. Masuke alikuwa na wazo moja tu. Kesho angeamkia kazi yake mpya na saa za adhuhuri angezunguka kutafuta chumba cha kupanga maeneo ya jirani. Uzuri alikuwa na akiba kiasi ambacho angemudu kulipia chumba walau kwa mwezi mmoja. Akiba aliyomudu kukusanya alipomfanyia kazi bwana Soud wa Masoud kule jijini Dar.

**

Bwana Steve Curl alikuwa katinga suti yake mpya iliyomkaa vema, machoni alipachika miwani ya jua, nywele zake akiwa kazilaza kwa mafungu, na kutengeneza kijibarabara kidogo kwenye kichwa chake chenye nywele fupi nyeusi. Mkononi alikuwa na smartphone yake, na alionekana kutazama saa yake ya mkononi ya gharama kuonesha alikuwa anajaribu kupimana kasi na muda. Mwendo wake pia ulithibitisha kuwa, bwana huyo ama alikuwa anawahi ndege au basi kuna zito lilomtia mota miguuni hata aonekane kuvuja jasho kwa haraka alokuwa nayo. Aliikatiza mitaa ya mji mkongwe kwa haraka akielekea kwenye hotel aliyokuwa amefikia. Boda boda wala hawakuonekana mitaani, labda hicho ndicho kilichomfanya mzungu huyo kutoka

marekani avuje jasho asubuhi hii ya saa kumi na mbili kwa kutumia usafiri nafuu, miguu yake.

Masuke alikuwa keshaamka mapema. Sasa na yeye alikuwa kwenye harakati za kuwahi kivukoni, huko huenda angepata kazi ya kumbebea mtu kitu ili apate kitu kidogo kama ujira wake. Alishaanza kuzoea kutengeneza hela ya kutosha tu hasa alipowahi alfajiri. Kwa kazi yake hii ambayo alijipachika, alijikuta akipata kuzoeleka hasa kutokana na lafudhi yake, waliyoipa jina wenyeji, 'lafudhi ya kibara.' Asubuhi hii aliamka akiwa na tabasamu. Jana ilikuwa njema, ikimfanya ahisi leo itakuwa bora zaidi.

Kwenye kichochoro hapo mji mkongwe, Masuke akamuona mzungu akihangaika na mabegi. Akachanua tabasamu murua, hii ndio kazi yake. Ila sasa, akajikuta lile tabasamu likiyeyuka ghafla. Nini? Akakumbuka wakati wenzake wanajifunza alfabeti na kiingereza, yeye alikuwa kwenye mabanda ya kubeti akitengeneza hela na kuliwa hela. Mwisho wa siku, hakuna cha maana alichopata. Anaanzaje sasa kumuomba hiyo kazi huyu mzungu aliyekuwa mbele yake? 'Ah, kwani nini! Nitaongea Kiswahili changu cha bara, asiponielewa potelea mbali, hata yeye alipokuja nchi za wenyewe alipaswa kujua lugha yao pia' hivo ndivyo alivyowaza, huku akiongeza kasi kumfuata Yule mzungu. Tabasamu mwanana kabisa likiambaa ambaa kwenye midomo yake. Alishajua siri, siri ya kufanikiwa kwenye kazi

yake, ilikuwa ni tabasamu lake. Hakuna aliyeliona akagoma kutoa kazi. Hiyo ilikuwa siri yake kuu.

'Halo mzungu, unaweza kuongea Kiswahili? Mimi kazi yangu ni kubebea watu mizigo na kuwafikishia wanapotaka kwa pesa kidogo sana. Naweza kukusaidia, naona hiyo mizigo yako inakuelemea bosi wangu.' Masuke alitamka huku akiliachia lile tabasamu lake.

'Sawa, sawa. Ni shilingi ngapi?' bwana Steve Curl alitamka maneno hayo mithili ya mtoto mdogo anayejifunza kusoma. Neno moja moja kwa tuo.

'Oh, mefurahi sana unazungumza Kiswahili. Pesa itategemea ni wapi unapoenda.'

'Nazungumza kidogo sana. Nataka kufika kwa taksi!' Curl aliongea kwa ishara ya kuonesha kwa vidole vyake kwamba Kiswahili chake kilikuwa kiduchu sana.

'Hapo bosi utanipa elfu mbili tu!'

'Elfu mbili, hiyo ni kidogo sana. Nitakupa elfu tano' Curl alizungumza tena kwa mtindo wake ule wa kusoma. Lakini ikaonekana kama kutangaza dau hilo kubwa ingemsaidia kuwahi alikokuwa anaenda, kwa vile kuzungumza na mswahili kulionekana kunamchelewesha. Hivyo alitumia vitendo zaidi kumhamasisha Masuke abebe haraka na wawahi huko walikokuwa wanaenda. Masuke alielewa, fasta sana

akabeba mabegi yake, akanyanyuka kwa mwendo wa haraka, kumwahisha mteja wake.

Hakutaka kuongea, nadhani aliona kabisa kwamba huyo bwana wa kizungu, alikuwa na haraka isiyohitaji soga za kupoteza muda. Alipomfikisha, na kuiweka mizigo kwenye taksi, Masuke akatoa tabasamu lake akipokea buku tano yake, halafu akatamka;

'Ukirudi, ukiwa na kazi yoyote, mimi nipo tayari kufanya kwa ujira mdogo'

'Uko tayari, kazi yoyote? Sawa sawa, mimi natafuta wewe nikirudi. Naitwa nani wewe?'

'Niite Masu, ukinitafuta, tumia 'M'bara' watu wanafahamu M'bara zaidi kuliko Masu!'

'Mubara, mubara!' Steve alitamka jina hilo huku akiliandika kwenye shajara yake ndogo.

'Asante sana, hii itakusaidia pia' Steve aliongea huku akimuongezea shilingi elfu kumi. Akazama kwenye gari, taksi ile ikaondolewa kwa mwendo wa kasi. Steve alikuwa anawahi sehemu bila shaka.

'Yyess, ah leo zari leo. Hesabu ya siku nimeshaingiza kwa kazi ya kwanza tu? Mungu mkubwa wallah! Naamini leo naweza kulaza hata hamsini. Leo, ah Asante Mungu.' Masu alimaarufu M'bara, alijiongelesha huku akipanga mipango lukuki kichwani mwake. Alianza

kuona mpango wake wa kumiliki guta unaelekea kuwa kweli. Alishaulizia dukani, akaambiwa laki moja na nusu angeweza kujipatia guta la kutengenezwa na mafundi welding, lenye tairi za baiskeli. Na sasa kwa muda mfupi aliokuwa amefanya kazi tayari alikuwa keshajiwekea akiba ya elfu themanini, ukiongezea na hii, hii aliyojipatia alfajiri hii, basi alikuwa na shilingi elfu tisini na tano akiba. M'bara akadhamiria siku hiyo ajitume angalau aingize kama elfu kumi na tano nyingine.

Akajiendea zake akiimba wimbo wa hip hop wa msanii wa Kenya Jua kali, *mwoto sana*! Si kama aliimba kweli, basi ni ile tu kusema alipenda mdundo na hivyo alijiwekea maneno anayojua mwenyewe kwa rhythm ya wimbo ule. Safari na mdundo.

Aliingia kivukoni saa kumi na mbili unusu hivi, harakati zilikuwa zinaendelea. Leo alichelewa kwa nusu saa hivi, hata hivyo haikuwa bure, ilikuwa nusu saa sawa na siku nzima ya kazi. Tabasamu lake lilichanua vema.

'We M'bara, kuja hapa, nataka ubebe mizigo hii uipeleke kwa duka yangu. Fanya haraka.' Babu G, ilikuwa jina la duka lake, mhindi aliyekuwa na duka la kuuza vifaa vya ujenzi. Mara nyingi mizigo yake ilifikia hapa kabla ya kwenda dukani, maana muhindi huyu kama walivyo wafanyabiashara wengine pia, alikuwa hapa kaweka stoo. Na kuna wakati alificha mali humo na kuwaambia wateja imeadimika halafu tena angewaambia

kuna kidogo amepata lakini gharama ikiwa imepanda. Hivyo ndivyo alivyojipangia bei na kutengeneza faida maradufu. Hapa, kulikuwa na mzigo wa saruji. Mifuko hamsini. Yote ilikuwa imepata wateja na kilichofanyika ni kuipeleka dukani wateja wachukue mali yao.

Kawaida Masu alipopata tenda kama hizi basi alilazimika kukodi maguta au torori kwa mkinga aliyekuwa ashakuwa mzanzibar bwana Faustine Kyando. Hadi lugha na mavazi yake sasa yalikuwa ya kizanzibar kabisa. Usingemtambua. Huyu alijua kutumia fursa. Kama ilivyokuwa kwa Masu, Kyando naye aliingia Zanzibar kama mtu aliyepotea njia. Kutahamaki akakuta wazanzibar ni watu wa kupenda sana maisha hadi ikawa si kuyapenda tena bali kuyaendekeza. Hawakuwa na muda wa kufanya kazi hizi ndogo ndogo, kwao kazi za kuvuja jasho zilikuwa na wafuasi wachache sana. Na hata hao, walizifanya watimize kusudi, walipolikamilisha usingewaona tena.

Kwake, Kyando hiyo ilikuwa ni fursa. Aliitumia vema akajikuta anafungua duka kubwa na kuwekeza pia kwenye vifaa vya welding. Akajitengenezea bidhaa na kuuza. Akatengeneza pia mikokoteni na maguta kwa ajili ya kukodisha. Akawatonya marafikize waje, walipokuja wakawa wanaitumia mikokoteni na maguta kufanya zile kazi alizoanza nazo. Yeye akawa ashinda dukani na kupokea hesabu ya kukodisha mikokoteni yake jioni.

Masu alikuta huo utaratibu ukiwa umeshawekwa mahali pake. Alijihimu haraka na kumfuata rafiki yake Paulo, ambaye sasa alijiita Bakari. Wakachukukua mkokoteni mmoja walioupa jina 'moto faya'. Kazi ikaanza. Tabasamu mwanana likienea usoni mwake. Alijipangia hesabu ya siku kuwa kumi na tano, lakini hapa walipewa mifuko hamsini. Mfuko mmoja kawaida walibeba kwa shilingi mia tano. Elfu ishirini na tano. Bakari angeambulia elfu tano tu na yeye angetia kibindoni shilingi elfu ishirini. Huo ndio utaratibu waliojiwekea. Kama aliona ndogo basi angetafutwa mwingine. Bahati nzuri, haikuwa siku njema kwa Bakari, alikuwa majalala mbaya. Alihitaji hela kama alivyohitaji oksijeni. Kwake elfu tano ilikuwa kubwa sana. Naye alikubali kwa tabasamu akimshukuru nduguye huyu kwa kumpa mchongo.

Siku yake ilikuwa njema, na sasa aliamini marafiki waliomwambia Zanzibar kunazo fursa.

## 2

Kazi ya mhindi babu G ilikuwa ngumu Sana, mfuko wa saruji wa ratili hamsini (50), kutoka hapo stoo Hadi dukani mwendo wa kilometa Kama mbili (2) hivi Ilikuwa inachosha, lakini SI kwa M'bara Masu! Alikwishazoea kazi hizi, hata Ilikuwa Kama asipozifanya hujisikia hovyo tuu kutwa nzima.

Masu na Bakari walichangamka, kazi iishe haraka, waone ustaarabu mwingine mahali pengine. Mkokoteni wao 'motofaya' uliweza kupakia mifuko mitano kwa mzunguko mmoja, hivyo ingewachukua mizunguko kumi kumaliza kazi ya babu G.

Wanaume kazini. Jasho na kivumbi. Mwanaume hasifiwi kula, mwanaume anasifiwa kazi. Vijana hao wawili waliusukuma mkokoteni huku wakiimba kufuatisha ngoma ya Juma Nature na wanaume TMK, 'shiibe shibe, haina bei! Shibe shibe, haina bei', kazi ikawa Ni Mwendo mdundo. Kufikia saa nne hivi za asubuhi, Masu na Bakari wakawa wamemaliza kazi.

Miili ikiwa imeloweka kwa jasho. Harufu za kiume zikikerehesha waliopishana nao.

'Masuu' ilikuwa sauti laini ya mtoto wa kike Mwamvita, binti wa mzee Abuubakr!. Mwamvita na Masu wanafahamiana, vile Masu hupooza njaa yake hapo mgahawani kwa mama Mwamvita. Ashaweka uteja hapo, hata asipoonekana, yeye huwekewa msosi pembeni maana hajapata kukosa hata siku moja.

'Bee malkia' hivyo ndivyo Masu humuitikia Mwamvita, na Mwamvita hufurahi Sana! Kwa Masu Ni utani, lakini lo! Hajui tu vile Mwamvita anamzimia.

'Leo nitakuandalia chakula kitamu Sana. Ushawahi kula biriani wewe?. Wabara mshazoea kula magimbi na viazi vitamu, mkipiga hatua mwala wali bokoboko! Hivo Ulisema watokea bara sehemu gani?'

'Wewe mwanamke maneno mingi mingi Sana veve, Mimi mutu ya India veve!' Masu aliongea, na hivyo ndivyo anavyomroga mtoto wa watu, utani utani, na vichekesho vyake, humvunja mbavu binti Abuu na kumfanya awe Teja kwake. Asipomuona Masu, Mwamvita hukaa siku nzima akimtarajia na Hali hiyo humfanya apoteze umakini. Na kitu kingine, Mwamvita hupenda Sana kuinusa harufu ya jasho la Masu!

Mwamvita Ana umri wa miaka 17, Ni mwanafunzi katika skuli ya Maji kupwa, Yupo kidato Cha nne. Mara nyingi mgahawani, huwapo jioni baada ya kutoka skuli. Hakosi hapo, maana shurti amtie Masu machoni, alinuse

na jasho lake la kutwa nzima. Hapo moyo wake huwa buhudaani sana.

Masu hajawahi kumuwazia mapenzi binti huyo. Kwanza, kwa sababu Ni mwanafunzi, pili kwa kuwa kazi zake hizi alishajiwekea miiko, ili kufikia malengo. Hivyo utani utani wake, hajawahi kudhani unachukuliwa kuwa ni kitu cha kweli. Hata anapomwita mama Mwamvita 'mamkwe', hajui vile anampa shida mama huyo, maana mama Mwamvita alishaziona dalili za huba za bintiye kwa kijana huyo, na anajua kijana huyo Hana habari juu ya hisia za bintiye.

'Mbona leo uko hapa muda huu Malkia? Unatakiwa uwe skuli usije pata shida nazopata mumeo. Kunuka jasho kwa kubeba mizigo kutwa nzima, wewe unapenda?'

'Nilitaka nikuandalie biriani, ukija lunch uupate utamu wa pishi la mkeo, nimefanya vibaya?'

'Shule Kwanza mama, mapenzi jioniii!'

'Unanipenda Masu?' Mwamvita akauliza kwa deko, akiutupia mgongoni ukosi wa hijabu yake!

'Aah Malkia? Swali gani Hilo? Hujui Kama nakupenda mdogo wangu?'

'Mdogo wako? Mi sitaki. Mimi si mdogo wako, Mimi mkeo!' Mwamvita alimaanisha, alipoyatamka maneno hayo, aibu aliziweka pembeni kwa muda, akamtazama Masu machoni barabara!

'Wewe msomi bwana, soma uolewe na waziri, mimi msukuma mkokoteni nitakupa Nini mrembo ka wewe, Wacha niwe nakuita mdogo wangu tu!'

'Nakupenda Masu, usiniambie hivyo buana. Wallah nakupenda!' Mwamvita alizungumza kwa hisia, hata ikampambazukia Masu kuwa, utani wake ulikuwa umeleta balaa! Hakulitarajia hili.

'Sawa Malkia, nakupenda unajua, ila sikuwa nimefikia kiwango hicho. Kwa hiyo, hebu nipe muda kucheki nipo kiwango gani.?'

'Unanipenda Masu, Unataka ukajidanganye eti hunipendi. Mimi sitaki bwana, utakapokuja kwenye biriani mchana, nitakuwa nakusubiri hapa, tupange mipango ya familia!'

'Hahaha Malkia umejua kunizingua leo!' Masu akaongea huku akipanga hiyo baadae amkwepe mtoto wa Shule. Habari za miaka 30 jela hakutaka kuzisikia.! Masu alikunywa chai chapati, akaondoka huku akimuonesha tabasamu adhimu Mwamvita. Mwamvita akafurahia Sana.

***

Masu alirejea ghetto, ajipumzishe Kidogo halafu aingie Tena barabarani kuona uwezekano wa kubutua mchongo mwingine ambao ungetokeza.

Alipofika gheto tu, akamkuta Jamaa mwingine waliyefanya kazi hizi za kubeba mizigo, kakaa juu ya jabali upenuni mwa gheto lake.

'Ohoo! M'bara huyo! Nsha...kusubiri Sa...sana hapa we bwa..bwana, umekua a..adimu ka chozi la sa..samaki?!' Yusufu ndio jina la mgeni huyo. Aliongea hayo huku akitoa tabasamu. Na vile Yusufu Ana kigugumizi, Basi Ilikuwa tafrani kubwa kukamilisha kauli zake.

'Ah Yusuf mtu wangu, we chenga Sana ujue, kupata ile efu kumi ukapotelea kwa Hamida, najua imeisha Sasa, enhee, nambie mtu wangu, fureshi?'

'Hahaha, Ha...hamida wa...wapi, nliku..wa Daslam bwana. Ndo nimerejea. A..asa, Ku...kuna ishu mu..himu mekuja na..nayo. Hafu si..siku..jua wewe a..aluwatani shehe?'

'Das'salam au chumbageni? Acha urongo mapema yote hii. Sema Kama unatafuta dili, we Yusufu mi nakumanya sana, unapenda Sana hizi..' Masu aliongea akimuoneshea kwa vidole kifuani kwake, kumaanisha matiti, huku akipuuza kauli ya Yusuf ya kuwa na Jambo muhimu.

Yusuf Kama alivyotuhumiwa na Masu, Ni Kweli alikuwa Ni mtu wa totoz, yaani alikuwa radhi asile Cha mchana na chajio inapobidi, ahonge msichana wa kulala naye. Ilikuwa Kama Ni ugonjwa. Ajabu kuwa, Pamoja na kutibiwa Mara kadhaa magonjwa ya zinaa, Yusuf hakukoma. Masu na Bakari walishamkalisha kitako Mara kadhaa kumuasa juu ya tabia hiyo, lakini, Mara zote aliporudia makosa, alikuwa mwepesi kumsingizia shetani. Ikafika mahali, Masu na Bakari wakamkubali tu

kuwa alikuwa mraibu, mraibu wa wanawake! Na labda kwa vile Ni muhali Sana kuachana na uraibu, wakakubali TU kuwa, huyo mwenzao alikwisha kuwa Teja!

'Ushazoea fiksi, Nina ishu mujarabu Sana! Ishu ya hela mwanangu. Karibuni tutastaafu hii kazi ya punda.!' Yusuf aliyasema hayo kwa kigugumizi chake.

'Enhee, nambie kijana wa ku-kaya, mgosii. Leo umeniletea dili badala ya kutafuta dili? Mambo yamechenji!'

'Usishangae, Mimi Ni mtu na koneksheni zake. Unamfahamu yule Mzungu wa safari?'

'Mzungu wa safari?'

'Eee, wale wamarekani wanaomiliki ile hotel kwa weupe tu hapo kisiwani! Anaitwa Steve, buana!'

'Mie sio mwenyeji Sana maeneo Haya babu!'

'Yule alokupa 15,000/= kubeba mizigo yake!'

'Ahaa, kumbe aitwa Steve?'

'Naam, yule bwana ana dili kwa ajili yetu!'

'Enhee!'

'Sasa ndo wavuta makini, masikio yamekusimama ka sungura, kusikia Ni Mzungu alokupa fedha?'

'Utaeleza ama utaanza mipasho?' Masu akambwatukia Yusuf.

## 3

'Tulia basi'

'Ah, Yusuf ee, acha u****' Masu, subra ilionekana kukosekana. Kwa kazi zao hizi, kutoa matusi hovyo hovyo ilikuwa kawaida na hawakuchukulia siriazi.

'Ok, iko hivi, yule bwana ataka watu wa kumbebea mizigo. Kuitoa Zanzibar na kuiingiza Zanzibar! Tofauti na hi tunayobeba, ya Mzungu haitoi jasho na mshiko wake si Kidogo pia.' Yusuf alimweleza.

'Enhee, lini hiyo?'

'Sio lini, Ni kazi ya kuajiriwa, sema Nini, kazi fulani tutakuwa tunalipwa dollars kibao Mwisho wa mwezi.'

'Dollars kibao ndio Kiasi gani? Hebu nyoosha maelezo mgosi, watu wa mwambao nyie mna kiswahili mrefu Sana!'

'Maelezo zaidi utayapata kwa bosi mwenyewe. Halafu, dah! Jamaa kanisisitiza sana.'

'We ulifahamiana naye vipi kwani?'

'Ah wapi, mi nilikutana naye, nikashangaa naitwa na ngozi nyeupe, nikageuka nyuma kuona Kama Kuna Mzungu nyuma yangu, haha nilikuwa mwenyewe, ikabidi nijongee jirani yake. Nikasikia; 'Habari yako bwana, Mimi nauliza kuhusu Mubara, wewe fahamu yeye? Yeye nabeba zigo!', Nilivyosikia 'Mubara' na 'zigo'

nikakumbuka ile simulizi yako, nikajua Ni wewe watafutwa.'

'Enhee!'

'Nikamuuliza, 'unamtaka wa Nini? Mimi pia nabeba mizigo!', Akasema Kuna ahadi mliweka, kuwa akirudi utamfanyia kazi. Alipomaliza kauli hiyo, kabla sijamjibu, akaniuliza; 'wewe pia nataka kazi siyo?' nikaona hapa zali, nikakubali fasta. 'Unataka nikubebee mzigo bosi? Nikamuuliza! Akajibu, No... Not today', akimaanisha SI leo, akasema Ni kazi ina mshahara mzuri na safari za hapa na pale.'

'Anhaa! Aisee Mzungu Mzungu tu, hawanaga mizunguko, akiahidi anatimiza. Hivi unafahamu nlishaga sahau habari zake kabisa? Lakini, cheki amerudi na kunitafuta kweli. Halafu Yusuf, kwani Hawa wazungu unafahamu hapa Zenj wana ishu gani?'

'Ntafahamia wapi M'bara? Mi nachojua, wanamiliki hotel ya kitalii kwa ajili ya watu wenye ngozi nyeupe TU!'

'Wee, albino pekee?'

'Haha, Mimi sijasema albino, nimemaanisha wazungu. Hotel yao inabagua rangi man.'

'Ah, isijekuwa wabongo ndo wanajibagua, maana mihoteli ya kisasa ya watalii, inatoza dollars TU, mshiko mrefu, sa mbongo gani ataacha kwenda penye urahisi akatapanye fedha zake nyingi kwa siku moja TU? Nina uhakika, weusi ndio wanakwamishwa na kukosa fedha, enzi hizi, haiwezekani kuwa na ubaguzi wa rangi.!'

'Labda, Mie nasikiaga pale ukienda mweusi ka Mimi unatimuliwa.'

'Mh, dah, enewei, itajulikana TU. Kwa hiyo huo mchongo umekaaje Sasa!'

'Hilo sio swali babu, Ni wewe TU, muda wowote ukiwa tayari, Mie nakupeleka kwake.'

'Poa poa, mi naona Kesho tukaicheki hiyo kazi.'

‘Nitakupitia asubuhi mapema, uwe tayari saa moja basi.'

'Poa aisee.'

'Sasa, Mie najikataa hivi!'

'Haina noma Yusuf, iwe Heri, Kesho tujaaliwe uzima!' Wakaagana, Yusuf huyoo, akasepa zake, Masu akazama ndani kujilaza walau anyooshe mgongo.

***

Ilikuwa ajiegeshe TU kunyoosha mgongo, usingizi ukamvaa bila hiyana. Akashituka saa kumi jioni, baada ya kusikia mlango wa gheto lake unagongwa mfululizo. Akajinyanyua kivivu na kuufuata mlango, akaufungua, ndani akazama Mwamvita bila kusubiri 'karibu ndani'. Masu alishangaa TU, mtu keshazama ndani. Wasi wasi ukamkumba ghafla. Mtoto wa skuli ghetoni mwake? Hii Ilikuwa hatari.

'Nilikusubiria Sana mchana, hukutokea. Nimeamua nikuletee mwenyewe!' Mwamvita alitamka huku akilitua kapu lake kwenye meza ndogo mle chumbani. Taratibu akaanza kutoa vilivyomo ndani. Hotpot kubwa ilibeba

biriani, hotpot ndogo ilikuwa na nyama iliyoungwa vizuri kwa viungo vilivyotoa harufu nzuri ya kuvutia, mboga za majani Kiasi, na tufaa mbili zilihifadhiwa kwenye bakuli lenye mfuniko. Soda ya koka kola, aliyopendekea zaidi nayo ilikuwepo ndani ya kapu alilokuja nalo Mwamvita. Muda wote huo, Masu alikuwa kaganda TU akimtazama binti huyo mrembo kwa Hali ya mfadhaiko. Heri Basi ingekuwa fadhaiko lile la awali. Fadhaiko hili liliupeleka moyo wake puta. Likaifunga akili yake isifanye kazi, likautia mwili joto. Macho yake yakakodoka kwa huba, yakawa yanapanda na kushuka kufuatisha mtikisiko wa mwili maridhawa wa Mwamvita. Mwamvita ima kwa kukusudia au kwa majaliwa, akampa mateso yaso chuki M'bara wa watu.

'Na mbona hukuja lunch mpenzi? Ndio umetoka kuamka, unaumwa Masu jamani?' Mwamvita akahoji kwa hamaniko, makini yake ikisadifu simanzi. Akamsogelea Masu na kumpima joto la homa kwa mgongo wa kiganja Cha mkono wake wa kuume. Masu akasisimkwa kwa kitendo hicho. Hata akashindwa aseme Nini isipokuwa kumkumbatia Mwamvita. Mwamvita akatabasamu, furaha yake ikidhihirika wazi. Harufu ya Masu ilipopenya pua zake, Mwamvita akajihisi raha ya pekee. Akajitahidi kwa ujanja, akajinasua kwenye kumbato la Masu.

'Karibu chakula mpenzi, nawa ule tafadhali!' Mwamvita akazungumza, sauti yake tamu, ikasikika

Kama sauti laini tamu ya malaika watukufu. Masu akatii na kufanya alichoagizwa.

Akala chakula Cha Mwamvita, akilishwa kama mtoto, akakubali kudekezwa. Hali yao ikibadilika kadri muda ulivyozidi kusogea. Masu akaridhia yote, akaridhia kuvunja miiko yake. Ilidhihiri udhaifu wa mwili, akili ikafunikwa isitafakari Cha ziada. Wakaruhusu miili yao kugusana, wakayaamsha yaliyojificha.

# 4

Masu alishituka saa 10 za alfajiri. Lo! Asalale! Akakumbana na mwili wa malkia pembeni yake!. Akatabasamu kwa furaha, akaunyoosha mkono wake wa kuume, akaifikia redio yake ndogo na kuifungulia. Akakutana na sauti ya mtangazaji ikimtaarifu Ni saa kumi kamili za alfajiri. Alfajiri? Haikumwingia akilini. Ina maana alilala na mwanafunzi usiku wote? Hofu ikamwingia na kuutikisa uhimilivu wake.

Kumbukumbu ya usiku uliopita ikamrejelea vema, hakukumbuka Ni saa ngapi alipopitiwa na usingizi. Kitu kingine pia kikagutua akili yake. Mwamvita aliingia Kama mvamizi. Hakukumbuka Nini hasa kilichomkwamisha kusimamia misimamo yake. Ikampambazukia kuwa walishiriki tendo Mara kadhaa Tena bila kizuizi. Je! Kama kamtia mimba mwanafunzi?

Masu akaamua kumuamsha Mwamvita, 'amka Malkia, amka!', akamtikisa taratibu, Mwamvita akaamka akipendezea pozi la kupiga miayo na kujinyoosha. Masu akasema moyoni, 'hakika wewe Ni Malkia, unanivutia kwa kila kitu, ona mwayo wako unavyonivutia, na huto tudimpo twako, we mtoto umeniweza!'

'Masu, Ni saa ngapi?' Mwamvita akauliza kwa hamaki. Masu akarejea kutoka huko alikotopea kwa hisia na fikra.

'Ni saa kumi alfajiri!' Masu akatamka akiwaza kwa sikitiko!

'Woii! mzee Abuu ataniua, mamaa!' Mwamvita akalalamika.

'Nipeleke nyumbani Masu, niwahishe nyumbani. Mzee akiamka saa kumi na nusu lazima ataniulizia, ili kunikumbushia swala ya alfajiri saa kumi na moja.' wakati anayaongea hayo, Mwamvita alikuwa anavaa nguo kwa haraka Sana. Ikamlazimu Masu kuamka na kuvaa pia.

Walipokwisha kuvaa, haoo, mdogo mdogo wakaanza kuikatiza mitaa ya Mwembe makumbi kuelekea nyumbani kwa mzee Abuubakr barabara ya tatu tokea hapo alipoishi Masu. Ikawa Ni Mwendo wa nusu kukimbia nusu kutembea.

Katika Kona ya kuingia nyumbani kwa mzee Abuubakr, wakamshuhudia mzee huyo akipiga mswaki upenuni. Wakalazimika kurejea nyuma Kidogo na kuingia nyumbani kwa mzee huyo kwa kupitia uwani. Ilibidi kufanya uninja ili kuingia ndani ya fensi. Masu akainamisha mgongo, Mwamvita akaukwea na kukamata mgongo wa ukuta, Masu akajinyanyua na kumuinua juu, mtoto wa kike akarukia ndani. Kishindo Kidogo kikisikika. Masu akalazimika kutoka hapo, nduki.

***

'Oyaa M'baraa, leo wapi mtu mzima?'

'Ah, leo hakusomeki mwanangu!'

'Vipi, aisee mbona umedoro Sana?'

'Dah! Mwanangu! Zenj kunanishinda muda si mrefu! Jana nimejikuta nikivunja miiko yangu. Nimetembea na mwanamke bila hata Kinga!'

'Ah!, faza Masu kaanguka kwenye uzinzi? Hahaha! Da! Hii hatari Sana. Ila mwanangu, hayo Ni Mambo ya kawaida Sana, we Ni mwanaume bana, utakaaje bila demu? Cha msingi, Tulia na huyo Sasa, usiongeze mwingine ukawa Kama Yusuf!'

'Dah, acha Bakari, Heri ingekuwa hivyo, binti mwenyewe mwanafunzi mwanangu!'

'Mwanafunzi kitu gani man, kwani umefumaniwa?'

'Acha kunijaza ujinga Bakari! We hujui kuwa na mwanafunzi Ni hatari ya mvua thelathini?'

'Ah, ila Kweli aisee, mwanetu Muddy tushasahau habari zake. Walisema amebaka mwanafunzi ilhali demu ndio alimfuata ghetto!'

'Dah, unanitisha ujue, maana dogo alinifuata mwenyewe na nikajikuta Mambo si Mambo, hofu yangu Ni Kama dogo hajadaka Kweli? Na mzee wake mwenyewe ni swala tano, mtoto wa shehe!'

'Loh, mwanangu, jipange aisee. Kama vipi Rudi jijini kwa wajanja, usikilizie Kwanza kabla ya kibendi kutokeza, kinapojitokeza wakikusaka uwe mbali, wapooze hasira zao. Halafu, wakati huu, jipange kusilimu aisee maana huyo lazima utamuoa Kama ameshiba mimba!'

'Dah, nipo njia panda. Mtoto mwenyewe nimemkubali Sana aisee. Wacha nisikilizie Kwanza! Kama akinambia Mambo yameharibika ndio nitalala mbele'

'Yeah hata Hilo nalo Ni wazo zuri! Lakini ikikubalika, si mnaichomoa tu, Yupo dokta Mugambo, yule M'bara mwenzio ndiyo michongo yake, we wekeza vijisenti tu kwa Sasa, Enhee mpango umekaaje?'

'Kuna ishu nafuatilia, ikiwa fresh, nitakujulisha. Ila inahusiana na yule Mzungu niliyowasimulia siku zile. Anadai Kuna kazi ya kuajiriwa! Hivi nataka niende huko mida ya saa moja. Alimtuma Yusuf kunipasha habari!'

'Dah, siwezi kuunga tela?'

'Ah, we sikilizia Kwanza, nikifika huko nitakupigia pande! Akiingia kingi, nitakujulisha, wewe Tena mwanangu mwenyewe nakuachaje Sasa?'

'Poa poa mtu wangu, fanya hivyo! Naona inabidi sasa nende zangu kwa Kyando pale, nicheki Kama kunaweza kuwa na dili.'

'Haina noma, baadaye Basi.'

Saa moja asubuhi, Masu na Yusuf walikuwa kiguu na njia kwenda kwa Mzungu Steve Curl. Walivalia poa siku hiyo, fulana na jinsi za bluu ziliwatoa, wakapendeza Kweli kweli. Mdogo mdogo wakaambaa na barabara ya Malawi kutokea Stone town, wakakutania Gulioni na Dereva wa Steve Curl. Kijana wa kihindi, anayaongea kiswahili kwa ufasaha. Gari likachoma mafuta na kuondoka Gulioni, likipandisha na Malawi road, kuelekea kaskazini mashariki, Hadi walipokutana na

Barabara ya Nungwi. Waliifuatisha hiyo Hadi kwenye ufuo wa Nungwi. Mbele yao wakashuhudia hotel ya kitalii yenye kila sifa ya usasa. Kwa M'bara, hii Ilikuwa Mara ya kwanza kuona mazingira ya hoteli hiyo ya kisasa kwa ukaribu na kutalii kwa ndani, kila Kona na mandhari zake maridadi. Bwawa kubwa la kuogelea, vyumba vya kulala vyenye hadhi ya kifalme. Utulivu na usafi uliozingatia weredi wa kimataifa kwenye uga wa kitalii..

Kwa muda wote waliozunguka eneo la hotel hiyo, wakiwa na mwenyeji wao Khassam, Hilo ndiyo jina la Dereva aliyewafuata, hawakuweza kuona mtu mwenye ngozi nyeusi Kama wao. Masu akakumbuka ile simulizi ya Yusuf kuwa hotel hiyo Ilikuwa kwa ajili ya wazungu pekee. Alielekea kuamini Hilo Hadi pale Yusuf alipovunja ukimya na kumuuliza Khassam kwa Nini mtu mweusi hakuonekana. Khassam akamtazama kwa mshangao na kutamka.

'Si kwa ubaya, lakini nadhani watu weusi Ni stingy (bahili) Sana, hawawezi kulipia milioni 2 kwa chumba kwa usiku mmoja tu. Hapa Kama uonavyo, Ni wazungu pekee, na hata hao, unaona wengi Ni vibabu ambavyo hapa wanakuja kutumia pensheni zao baada ya kustaafu. Na wengine Ni wale matajiri wenye kumiliki vyanzo imara vya kipato na biashara huko Kwao. Na kingine, hapa hawaji watoto, Ni watu wazima pekee!' Khassam aliongea na kujibu maswali yaliyokuwa yafuate bila

shaka. Na kuthibitisha Hilo, kabla Masu hajafunua mdomo wake kuuliza, Khassam aliongea.

'Nachojua Ni kwamba, huo Ni utaratibu wa hoteli hii. Sijui kwa Nini waamue kuwa Ni eneo kwa ajili ya watu wazima pekee.' Maelezo hayo, yakawa Ni Kama yamelenga kumnyamazisha Masu asiulize swali lake. Swali ambalo tayari Khassam alilijibu.

'Mnaonaje Haya mazingira?' Khassam akauliza.

'Dah! Nadhani walokole wa huko bara ndani ndani wakifika hapa, haki ya Mungu watajua wameingia mbinguni. Maana zile nyimbo zao kuwa mbinguni Kuna barabara za almasi, majumba ya kifalme yenye kung'ara kwa dhahabu, taa maridadi na mazingira tulivu!, Hapa Ni zaidi ya wanavyodhania.' Masu alizungumza na kuchokoza vicheko kwa wenzake.

'Kama hivyo ndivyo, Basi ndugu M'bara, sisi tunayo bahati ya kufika mbinguni kabla yao haha!' Yusuf aliongezea. Wakacheka Tena.

'Na Kweli, mnayo Bahati Sana. Kwa maana tangu nianze kufanya kazi hapa, huu mwaka wa kumi Sasa, na sijawahi kuona ngozi nyeusi kwenye eneo hili. Bahati yenu Ni kubwa sana.' Khassam alizungumza, wakiwa wanaketi kwenye sofa katika moja ya maeneo yenye mandhari nzuri, kwa nje bahari ya Hindi ikionekana mubashara kwa uzuri usio kifani na kwa nyuma yao, bwawa la kuogelea likikolea bluu bahari yenye mvuto unaovutia.

'Steve atakuwa hapa muda wowote kuanzia Sasa, haichukui muda mrefu. Mtakula nini niwaagizie?'

'Ah, da! Braza, tuchagulie mwenyewe. Na vipi, twalipa wenyewe'? Yusuf akauliza na kuongezea,

'Kama tunalipia wenyewe, kwa Kweli Mimi Sina njaa!'.

'Msihofu, kila kitu Steve analipia. Bei za hapa nyinyi hamziwezi wazee, nyie furahieni fursa hii adimu.'

Khassam akawaagizia wali samaki. Wakala na kushiba na walipokwisha kunawa, wakiwa wanashushia na juisi ya ukwaju, wakamuona Mzungu akitokeza.

# 5.

'Oh, furaha Sana kuona wewe mubara! Na leo uko pendeza Sana. Sasa tutaenda mahali kwa mazungumuzo. Yeye wawili nafuata Mimi!' Steve alizungumza huku akiwaashiria kufuatana naye. Kiswahili chake kikionekana kuboreka Kiasi. Kwa Sasa alitamka maneno Kama anavyosoma mtoto wa darasa la tatu.

Waliongozana na Steve na kutoka nje ya jengo la hotel ile ya kisasa kwa upande wa nyuma wa hoteli hiyo. Ilikuwa na eneo kubwa la wazi lenye misitu ya mikoko. Huko wakaona ubunifu mkubwa uliotengenezwa kwa ajili ya kuwapa burudani wageni waliofika mahali hapo. Bembea imara ziliwekwa humo porini, kwa umbali wa kukadiria ili kwamba, isitokeze usumbufu kwa watumiaji bembea wengine. Sasa, Ilikuwa dhahiri kwa Nini watoto chini ya miaka 17 hawakuruhusiwa. Hotel hii Ilikuwa maalumu kwa wapendanao. Hasa wale waliotoka kuoana wakataka faragha kwa ajili ya fungate lao. Na labda pia kwa wale wazee waliokuwa wanazeeka Pamoja.

Walilibaini Hilo maana waliweza kuona wazee hao, na kwenye bembea zile, walionekana pia watu wawili wawili wa jinsia tofauti wakifurahia huba!

Uzuri wa hili eneo la hotel, lilikuwa limeinuka, na kufanya kuwepo mwonekano Bora kabisa wa bahari chini yao. Na hapa walipokuwa, kulitoa mandhari nzuri

Sana ya kuiona hotel ile ya kisasa na mazingira yake tulivu, lakini pia, ilitoa fursa kuliona jua linapozama baharini saa za jioni.

Walijitenga mbali na watu wale waliokuwa wakifurahia bembea, wakaketi chini ya mti mkubwa uliopandwa, ukitengeneza kivuli mujarabu kuwakinga na jua. Hapo, wakavuta makini zao kupokea maelekezo ya kazi yao mpya.

'Ok, mubara karibu sana, nawe pia Mr Yusuf. Hii kazi Ilikuwa kwa ajili ya mubara, na Ni kusema wewe Yusuf uliamua kutumia fursa ya Mimi kukuulizia kulazimisha upate kazi pia. Najua mubara Yuko tayari, alinambia mwenyewe atafanya kazi yoyote ile. Je wewe, Yusuf uko tayari kwa kazi yoyote ile??'

Yusuf akataka kutafakari Kwanza lakini akahisi kusita kwake kungetumika kumtoa kwenye fursa, maana Kama Steve alivyosema, ilionekana yeye alikuwa hahitajiki ila alilazimisha. Akajibu haraka haraka bila kusita.

'Ndiyo'

'Ok, Kama hivyo ndivyo, nataka nipate Kiapo chenu Cha utii. Kazi hii Ni kazi inahitaji ujasiri, na ukakamavu, na Kama Unadhani kufanya kazi ya ujasiri na ukakamavu, Tena inayohitaji usiri mkubwa Ni shida, Basi Sasa Ni muda mwafaka wa kujiondoa. Kama unakubali, maana yake Ni kwamba, huwezi kurudi nyuma kamwe. Ukikubali utakuwa unalipwa pesa nzuri

Sana. Mnaonaje kulipwa elfu sitini kwa siku?' Steve aliongea na kuuliza.

Masu na Yusuf macho yakawatoka kodo! Akilini mwao mchakato wa hisabati ulikuwa unaendelea. Sio kanuni za Pythagoras wala Newton wabobezi wa mahesabu na Fizikia. Lah, Ni zile hesabu maarufu za magazijuto. Wakayaondoa mabano, Wakagawanya, wakazidisha, wakajumlisha na kutoa. Wakapata Sawa Sawa na 'NDIYO' yenye herufi kubwa. Wangeachaje sitini kwa siku, ilhali kazi yao ya awali Ilikuwa ya maguvu, na walipojitahidi Sana na Mungu kuwaangazia Nuru za uso wake, walifanikisha elfu ishirini TU!

'Tuko tayari.' wakatamka Kama waimba ngonjera, kwa kupokezana.

'Vema, kwa kusaini hapa kwenye hii dokumenti mtakuwa mmekubali masharti ya kazi na kula Kiapo Cha utii. Pia mtakuwa mmesaini mkataba wa malipo ya shilingi elfu sitini kwa siku!' vijana hao kusikia elfu sitini kwa siku, kukawapumbaza, wakang'ang'aniana kalamu, kila mmoja akitaka kuwa wa Kwanza kusaini. Maelezo ya mkataba yaliyoandikwa kwa lugha ya malkia wa uingereza hawakujali kuyasoma. Waliridhika na Maelezo ya Steve Curl.

Walipokwisha kusaini, kila mmoja akiandika majina yake matatu na kuweka dole gumba, waliongozana na Steve Curl kuingia kwenye eneo lililokuwa na fensi ndefu ya ukuta mle mle kwenye pori, likiwa na maandishi mlangoni, 'WAHUSIKA TU'. Steve aliingiza

namba fulani fulani kwenye kifaa kilichofanania na meta ya luku yake, hivyo ndivyo Masu alivyodhania. Baada ya zoezi Hilo, kwenye mlango ule, kulikuwa na kitu Kama katobo hivi, Steve alisogeza jicho lake jirani na tobo lile, ikawa Ni Kama anapiga chabo kinachoendelea mle ndani, Mara, Masu na Yusuf wakasikia sauti ya mwanamke ikitamka maneno, 'welcome Steve' mlango ule ukaachama kwa uwazi. Nafasi ikajitokeza na wao wakazama ndani. Walipokwisha kuingia ndani, mlango ule ukajifunga Tena. Kwa M'bara Masu, hii Ilikuwa kitu mpya! Mlango unaozama ukutani unapofunguka!!

Fensi ile ndefu, kumbe ndani Ilikuwa Ni eneo kubwa Sana lenye ofisi chache, na magodauni mengi ya kuhifadhi bidhaa na Mali kadhaa ya hoteli bila shaka, lakini walichogundua baadaye Ni kuwa, chini ya ardhi kulikuwa na vyumba ndani ya eneo hili lililolindwa kwa mitambo ya kisasa na makamera ya cctv. Huko chini, kulikuwa na Mambo mengi ajabu. Kama si kwa kuingizwa kule na Steve, Wasingejua kuwa, huko kulifanyika anasa za kila namna.

Waliteremka kwa lifti, wakashuhudia ukumbi mkubwa unaowaka Waka taa za rangi tofauti. Huko walijazana wazungu na waafrika pia. Vinywaji mikononi, wengine sigara, na hata waliotumia dawa za kulevya za unga unga wakizisokomeza kwenye pua zao. si hivyo tu, wapo walioonekana wakipapasana miili hadharani bila aibu. Lakini ilivyodhihiri machoni mwao, wengi wa waafrika waliokuwamo humu, walikuwa Ni

wasichana warembo wa miaka kumi na mbili Hadi ishirini hivi!

Wote hao, wakionekana kuwepo pale kwa ajili ya kuwaburudisha wazungu wale. Muziki ulikuwa unasikika kwenye ma-spika makubwa ya kisasa. Muziki uliochujika Vema na kuburudisha masikio. Ilikuwa club moja ya kisasa. Ajabu, muziki huo, haukusika walipotoka pale ukumbini na kutokeza kwenye korido ndefu iliyokuwa na ngazi za kupanda juu. Kukiwa na taa zenye mwanga hafifu wa njano kuwaongoza. Walitokezea nje kwenye pango. Isingekuwa rahisi mtu kudhani kuwa Hilo pango liliongoza njia ya kuingia kwenye jumba la starehe na anasa. Kwa nje lilitisha, nyasi kibao zilijiotea hapo, na Kuna namna Masu alishuhudia bonge la joka likiishilia kule walikotokea. Hata hivyo, akapotezea kwa kuhisi Ni fikara zake tu.

Baada ya kutokeza huku kulikoonekana kuwa porini, waliuona ukuta ule uliozunguka zile godauni kwa nyuma yao.

'Huku Ni eneo la mazoezi, mtajifunza kutumia silaha mbalimbali kushambulia na kwa ajili ya kujilinda pia!' Steve alizungumza na kuuondoa ukimya uliokuwa umetawala safari yao.

Masu akatabasamu, hofu akaiondoa moyoni, Nuru ya matumaini ikamrejea.

'Kumbe kazi yenyewe Ni ulinzi!' akawaza. Kwake hii Ilikuwa Ni kazi rahisi yenye mshahara mnono. Akakumbuka maneno ya awali ya Mzungu Steve, kuwa

Ni kazi inahitaji ujasiri na ukakamavu. Masu akatabasamu Tena, safari hii akionesha furaha yake wazi wazi.

Mbele yao, akatokeza mwanaume mwenye mwili uliojengeka Vema. Kijasho chembamba kikinatia kwenye ngozi yake. Alikuwa kifua wazi. Huyu hakuwa Mzungu, labda mchanganyiko wa mkorea na Mzungu, maana sura Ilikuwa ya kikorea, lakini mwili wa kimarekani. Alikuwa mrefu wa kimo, kifua kipana, mwili wa kati kiwastani, au tuseme, si mpana si mwembamba!

'Master Park Hye, kutana na 'mubara' Pamoja na Yusuf, wanafunzi wako wapya!

Mubara, Yusuf, mwalimu wenu, master Park Hye!'

Masu akamsogelea master na kumpa mkono akiwa mwingi wa tabasamu na bashasha!

'Naitwa Masuke Masu...!' Masu alikuwa anaongea Kama anayelia. Tabasamu lake lilinyauka ghafla. Mkono wake ulipokutana na wa master, Masu alihisi kubanwa na chuma! Maumivu makali yakapenya ngozi ya mkonowe na kuipeleka taarifa hiyo kwenye ubongo wake..

'Karibu' Park Hye akajibu akiwa bado ameshikilia mkonowe Masu. Uchozi ukamdondoka Masu, huku akifanya jitihada za kujinasua. Alionekana kujinyonga nyonga kwa maumivu!

Yusuf alishuhudia kilochomtokea mwenzie, akajaribu kutafuta namna ya kuuepuka mkono chuma wa master.

Yeye akajifanya salamu yake badala ya kushikana mikono, akatoa saluti. Ah wapi! Mkono chuma wa master ulimkamata barabara, tofauti na Masu aliyedondosha chozi na kugugumia maumivu, Yusuf alitoa kilio Cha mtoto mdogo!

'Mamawee!'

'Hapa panaitwa kwa master. Kuna vitu kadhaa tutavi-master mkiwa hapa. Nitawapatia ratiba na mtatakiwa kuifuata kikamilifu' Master aliwaeleza, wakati huo Steve alikuwa hatua kadhaa kurejea kule walikotokea.

# 6

Kama walidhani kazi hii mpya ingekuwa na urahisi wowote, walikosea kudhani hivyo! Waliamka alfajiri ya saa kumi usiku, wakaingia uwanjani. Baada ya hapo, saa moja kamili walipata kifungua kinywa kwa dakika kumi na tano. Saa moja na robo waliingia darasani kujifunza lugha tatu muhimu. Kiingereza, kiitaliano na Kifaransa. Zoezi Hilo lingefanyika Hadi saa sita za mchana. Kulikuwa na walimu wa kuwafundisha kusoma, wa kuongea, na wa kuwaonesha kwa vitendo tamaduni za wenye hizo lugha tatu. Walipomaliza Hilo, walikula. Wakaruhusiwa kupumzika kwa masaa mawili, wakarejea Tena darasani kujifunza computer na masuala ya kiteknolojia. Jioni saa kumi walirejea uwanjani kwenye mazoezi ya kijeshi.

Walianza na mazoezi Kidogo Kidogo ya mwili, yakaongezeka kadri siku zilivyosogea. Baadaye wakaanza drill za kijeshi kwenye upande wa mazoezi ya viungo, kutembea na mizigo mizito, kujongea Kama nyoka, miruko ya aina mbalimbali. Miili yao ikabadilika. Umakini wao ukaongezeka. Wakatengeneza mlango wa sita wa fahamu! Uwezo wa kuona bila kufumbua macho, kuhisi hatari kabla haijatokea, kusikia sauti ya kimya! Mwishoni walijifunza matumizi ya silaha, kila aina ya silaha! Hotel hii, Ilikuwa Sawa na nchi inayojitegemea

kiulinzi. Hivyo ndivyo walivyodhania. Walimudu kuzitumia silaha na hata kutengeneza zingine. Mabomu madogo madogo waliweza kuyatengeneza kwa kutumia vifaa mbalimbali, na mali ghafi muhimu kwa kazi hizo.

Miezi tano Sasa Ilikuwa imekatika tangu waingie hotelini. Kama ungewaona, Masu na Yusuf, hakika usingewatambua. Walibadilika! Walikuwa tofauti. Waliongea kiingereza na Kifaransa Kama vile walizaliwa huko. Miili yao, ilionekana kubadilika Sana. Zaidi mno, walionekana Ni watu wenye fedha zao, maofisa wa idara nyeti labda.

Walipopewa likizo ya mwezi mmoja kabla ya kurejea kazini kuanza rasmi kazi yao, Wazo la Masu lilikuwa kwa Mwamvita pekee! Hivyo, aliliendesha gari dogo aina ya ist, Mali ya Steve, ambalo aliamua kumzawadia kwa kufuzu Vema zile harakati, na moja kwa moja akakamata breki mgahawani kwa mama Mwamvita. Akaitafuta Kona yake mle mgahawani, meza aliyokua kajizoeza kutumia miezi kadhaa hapo awali, akaketi. Alivalia miwani myeusi na suti Kali ya bluu. Mkononi alikuwa na smart watch (saa ya mkononi ya kijanja) ambayo ilimpa taarifa kadhaa muhimu Kama vile Hali ya joto Ni kiwango gani, Kama simu yake iliita, lakini pia ilimpa taarifa juu ya chumba alichoishi kule porini chini ya ardhi,na kumtaarifu Nini kiliendelea akiwa hayupo. Picha za video zilionekana kwenye kioo Cha saa hiyo, mubashara kabisa. Aliketi hapo akisubiri muhudumu amfuate.

Mara akaja muhudumu, Masu akatoa macho yake kwenye saa yake hiyo na kuyainua amtazame huyo mhudumu. Akautaliii mwili wa muhudumu kwa macho yake, kuanzia miguuni na kupandisha juu huku akitabasamu. Aliifahamu miguu ya Malkia wake Mwamvita. Bila shaka akijiambia Sasa Mwamvita atakuwa keshamaliza kidato Cha nne, na Kama Kuna lolote, itakuwa Ni kusubiri matokeo ya kujiunga kidato Cha tano. Akawaza vile atapata wasaa mzuri wa kutumia na malkia wake kwa mwezi huu mmoja.

Masu akaendelea kuutalii mwili huo kwa pozi, akayatua macho juu Kidogo ya nyonga ya Malkia huyo. Mshituko ukamkamata ghafla. Uvimbe wa kitambi, ama la! Basi mimba. Macho yake yakataka majibu. Akakutana na uso wa malkia wake, macho yake yakamtazama usoni. Kulikosekana lile tabasamu adhimu, tabasamu ambalo lilimfanya Mwamvita avutie na kupendezea. Alionekana kupungua pia. Mawazo! Alionekana kujawa mawazo na wasiwasi.

'Karibu mgeni, nikuhudumie Nini tafadhali?' Mwamvita akazungumza huku akilazimisha tabasamu!

*'Ha! Mwamvita hajanitambua*? Masu akashangaa. Akaamua kuivua miwani.

'Kama kawaida yangu, ila Kama biriani ipo basi utakuwa umenitendea haki zaidi Malkia!' Masu akatamka kwa ile sauti yake ya utani! Akawa Sasa anaiwazia mimba ya Malkia, akijiuliza Kama yeye ndiye baba au la!

Mwamvita aliposikia hivyo akashituka. 'Sauti Kama Masu, Hadi macho na sura zao zafanana. Lakini hawezi kuwa Masu. Duniani wawili wawili.' akajiwazia huku akijaribu kupotezea hisia kuwa huyu alikuwa Masu wake. Lakini kitu fulani hakikuwa Sawa. Ni Masu pekee aliyemwita malkia, huyu kaanzaje, kwamba Ni Bahati tu? Hata! Kuna kitu hakikuwa Sawa. Labda Ni Kaka yake, na Masu kamsimulia habari zangu na yeye! Masu aliyemjua, alipewa habari za kuaminika kuwa alitekwa na watu wasiojulikana, na tangu hapo hakuwahi kuonekana kokote kule Zanzibar. Alikwisha muombolezea machozi yakakauka. Vipi Sasa hili litokee! Kama hiyo haitoshi, huyu alikuwa mtu wa familia Bora! Suti Kali, gari, mwonekano wa kifedha!

'Kawaida yako Ni ipi, samahani, Ni kwa sababu ndiyo Mara ya kwanza nakuhudumia!' Mwamvita aliuliza, huku akidhamiria kufuta kabisa kumbukumbu ya Masu iliyokuwa imefufuliwa.

'Ok, bila samahani. Nikuombe tafadhali uketi hapo!' Masu alimweleza Mwamvita na kumuoneshea kiti kilichokuwa mkabala naye. Mwamvita akaketi huku akijiuliza, *'wanawezaje kufanana sauti hivyo?'*

'Dah, Hadi Sasa siamini kabisa Malkia wangu unaweza kuwa umenisahau kabisa Kiasi hiki. Miezi mitano tu na umeniondoa kabisa akilini mwako?. Nisamehe Sana mpenzi, naweza kuwaza tu, kwa ujauzito huo na Mimi kutoonekana itakuwa ilikutia simanzi kubwa…..' hakumalizia, Mwamvita alinyanyuka na

kumsogelea Masu, akamshika mashavu, akaipapasa shingo yake, akanusa shati lake kwa pua zake, akakutana na harufu nzuri ya marashi, bila shaka marashi ya ghali pia. Akaikosa ile harufu nzuri ya jasho la Masu. Hakuelewa. Akatamka

'Masu!?'

'Naam, Ni Mimi Malkia, Ni Mimi Masu wako!' Masu akamvuta Mwamvita na kumkumbatia! Mwamvita alikuwa analia. Machozi yake yakatotesha shati lake. Masu akatoa kitambaa Safi cheupe mfukoni mwake. Akamfuta machozi. Dakika moja na ushei ikakatika wakiwa kimya, wamekumbatiana.

Mwamvita alipoona Vema, akatamka.

'Niliambiwa ulitekwa na wasiojulikana! Lakini nikuonavyo, hukutekwa. Kuna siku niliota umekuja, ukanambia umetuandalia sehemu Mimi na mwanao tukaishi.! Mbona hukuniaga? Ulinifanya nikuomboleze. Kumbe uko hai Masu!' machozi yakamdondoka.

'Nipo hai, Nani huyo aliyekudanganya nimetekwa?'

'Masu hapa mtaani kila mtu anajua umetoweka baada ya kutekwa na wasiojulikana!'

'Dah, ila binadamu wana habari nyingi. Malkia, Mimi sikutekwa. Kuna dili nilipata, nilipoenda kwenye usahili, nikafuzu na sikupewa nafasi ya kurudi, tukawa tumepelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kazi. Sikuwa na namba ya simu ya hapa kwenu, ningekupigia simu walau nikujulishe kilichojiri, lakini ndio hivyo Tena, mawasiliano yalikatika!' Masu alidanganya, alizingatia

maelekezo ya bosi wake kuwa, habari za kule walikokuwa, hazikutakiwa kutoka.

'Kwa hiyo Sasa umerudi?'

'Kwa likizo ya mwezi mmoja tu!'

'Utaondoka Tena?'

'Ndiyo Malkia….'

'Bora usingekuja. Nilishaanza kuzoea hali. Kuja kwako na uondoke Ni Kama umeamua kufumua kovu la kidonda kilichopona na kutengeneza donda kubwa jipya!' Mwamvita alizungumza akitoa machozi.

'Mbona wasema hivyo Malkia?'

'Baba ananilazimisha kuolewa Kama bi mdogo wa babu mmoja, Mzee Kisiki, Mie sitaki Masu, hii mimba niliyobeba, Ni matokeo ya mahaba yetu ya siku ile. Wakinilazimisha Sana nitakufa Masu!' Mwamvita akazungumza kwa huzuni kuu machozi yakitiririka.

'Kwa Nini, mbona mzee Abuubakr Ni ulamaa mzuri, nwanazuoni wa dini, vipi akufanyie hivi.?'

'Kwa sababu kupata mimba nyumbani nimemfedhehesha Sana, anavyosema yeye!'

'Hata Kama, bado haimpi haki ya kukulazimisha uolewe na kibabu. Ila usijali. Wewe na mtoto wetu hamtalazimishwa kuishi na huyo kibabu! Nataka nikupeleke kwa dada yangu Dar, huko utakaa kwa furaha, nitakuwa nakutumia fedha kwa ajili ya matumizi yako yote. Au nikupangie Nyumba kabisa huko? Ah, nitakupangia Nyumba Dar, ila kwa Sasa, utakaa kwa dada Hadi utakapojifungua. Ukishajifungua, Kuna

mdogo wangu yupo kijijini atakuja kuishi na wewe kwenye hiyo Nyumba nitakayokupangia, anaitwa Maureen. Unaonaje Hilo Wazo?' Mwamvita Kidogo amrukie Masu kwa furaha, lakini mgahawani akawa ameingia mteja.

'Asante Sana Masu, nilikuambia, Unanipenda, huwezi kujidanganya eti hunipendi! I love you Masu' Mwamvita akatamka huku akiondoka akamhudumie mteja alioingia.!

# 7

Mwamvita akaondoka, Masu akawa anamwangalia. Akabaini Mwendo wa Malkia ulikuwa tofauti na alipokuja kumhudumia. Alionekana kuchangamka zaidi.

Aliporejea, kutoka kumhudumia mteja, Mwamvita alikuwa tofauti, huyu ndio Mwamvita aliyemfahamu. Malkia. Tabasamu mwanana!

Jioni ya siku hiyo Masu na Mwamvita walikuwa Pamoja wakizungumzia mpango wao wa kutoroshana. Walipofikia mwafaka, wakakubaliana mawasiliano yafanyike ili kuweka mazingira ya pa kufikia kueleweka.

Siku hiyo, Mwamvita hakulala kwa Masu, na hata hivyo si Kama Masu alikuwa bado mpangaji pale Mwembe makumbi, hivyo hata hapa walikokuwa wamekutania Ilikuwa tu Lodge, mtaa mwingine mbali na Mwembe makumbi.

Kufikia saa tano hivi, Masu alimrejesha Mwamvita nyumbani. Safari hii hawakutumia njia ya kuuruka ukuta. Walimtumia ujumbe dada wa kazi, akafungua geti Mwamvita akaingia ndani'.

***

Masu aliingia jijini mnamo saa tano alfajiri. Akapanda daladala kuelekea Tandika. Dada yake Maimuna alikuwa Ni mchuuuzi wa mboga na matunda kwenye soko la

Tandika. Ilikuwa kitambo tangu aonane na dadake, Toka alipoondoka kwenda Zanzibar. Mawasiliano yao hayakudumu Sana hasa baada ya simu ya dadake kufungiwa na TCRA, na alipofanikiwa kusajili namba mpya, hakuwa na namba ya Masu. Hiyo ndiyo sababu iliyopelekea afunge safari kwenda jijini ili kufanya mkakati wa kumhifadhi Mwamvita hapo.

Alitokeza gengeni kwa dada yake akiwa kavaa kizungu, suti nyeusi, miwani machoni, shingoni alininginiza tai nyekundu maridadi kabisa. Mfukoni alikuwa na senti za kutosha. Senti zilizomwezesha Masu kumbebea dadake na wapwa zake zawadi za kutosha Toka Zanzibar, na zingine akiwa amezichukulia hapo hapo jijini.

Ilikuwa furaha, kuku walichinjwa, mchele ukapembuliwa kuondoa chuya, mchele wa gredi. Vinywaji vikaletwa, Ilikuwa sherehe. Walipokwisha kushiba, simulizi zikaanza, maswali kede kede. Ulikuwa wapi, unafanya Nini? Mbona umebadilika. Anko siku hizi Una hela? Anko ulikuwa Ulaya? Anko unaongea kizungu? Yote hayo akayajibu kiufasaha kabisa. Akiwa makini kutotoa Siri za kule kwa Mzungu.

Akawaeleza kwamba bado Yuko Zanzibar na anafanya kazi kwenye shirika kubwa la kitalii Kama mwongozaji wa watali. Mwishoni, akapata faragha na dada yake na kumweleza mpango wake. Dada yake Maimuna, akamweleza Hana shida na hili, isipokuwa

maamuzi ya Mwisho yalikuwa kwa shemejie Bwana Jumanne Mgunda.

'Bwana shemeji, Hilo ndilo Jambo nataka unifadhili, akishakujifungua, nitampangishia Nyumba na ataishi hapo akifanya biashara nitakayomfungulia. Tafadhali Sana bwa'shemeji!' Masu alimrai shemejie

'Bwana shemeji unachoniomba Ni kitu kigumu Sana. Huyo Ni mtoto wa wenyewe, akapata tatizo, sie tutafanya Nini? Mimi ningekushauri uwatake radhi hao wakwezo, umtolee mahari awe mkeo! Shida gani hata umfiche binti wa wenyewe, ilhali unao uwezo wa kumuoa?, mbona ufanye hivyo bwa'shemu!?!' Bwana Mgunda alijihami. Labda kwa uzoefu na umri wake, alijua hili lilikuwa suala la kitoto, ambalo hakutaka kulishiriki.

'Nakuelewa Vema usemacho bwa'shemeji, shida Ni kazi nayofanya, hainitaki kuwa na mke!'

'Kazi ya kuongoza watalii haikutaki uwe na mke? Bwana shemeji, una hakika kazi yako Ni uongozaji watalii Zanzibar?' Mgunda aliongea, akitilia mashaka kauli za Masu.

Ni Kweli hakupaswa kuwa na mke, kazi yake hii, kwa mujibu wa maelekezo ya master Park Hye, kuwa na mke, au familia, lilikuwa Ni kosa kubwa Sana. Bila ufafanuzi wa ziada, masta alionesha kuwa Ni rahisi familia kutekwa na kusababisha mhusika kutoa Siri. Ilikuwa bado kuchakatwa na ubongo wa Masu Kama kazi ya ulinzi Ilikuwa na Siri nyingi vile. Hoja ya

shemejie, Ilikuja kumpa changamoto. Ingawa alipewa onyo juu ya familia, Masu alikuwa radhi kuifanya Siri, lakini si kumkana Mwamvita, Tena akiwa tayari kumletea mtoto? Atafanya lolote kumlinda Mwamvita na mtoto wao ajaye.

Kwa Nini walisisitizwa kuwa na Siri? Mbona Siri zenyewe hawakuzifahamu bado? Siri pekee waliyojua Ni kutoeleza kile walichofundishwa na mahali walikojifunzia. Je kulikuwa na umuhimu wa kuendelea kuficha hata nduguze?

'Asijue baba Wala mama, asijue mpenzi au nduguyo. Siku atakayojua mtu Siri hizi ndiyo siku utakuwa umetangaza kiama chako.' maneno ya master yakajirudia kichwani mwake. Maneno ambayo yalifuatana na kunyweshwa kinywaji kichungu kupata kuonjwa na ulimi wake. Ikiaminika kuwa kinywaji hicho Ni Kama jini lililowekwa kuilinda Siri. Siri gani na kwa Nini Siri?

Kumbukumbu hiyo ikamuonesha hatari iliyokuwepo mbele yake. Hakutaka kuendelea na mazungumzo zaidi. Hakutaka kupoteza kazi kabla hajaianza kazi.

'Nimekuelewa bwana shemeji. Wacha nione Nini Cha kufanya.' Masu akaongea huku akisimama. Kichwani mwake alitafakari safari ya kijijini Malonje.

***

Baada ya mazungumzo ya Masu na shemejie kutozaa matunda aliyotarajia, alimpigia simu Mwamvita na kumjulisha kilichojiri, hata hivyo hakumweleza ukweli

kwamba, sababu ya ombi lao kukataliwa lilikuwa na uzito wa kutosha. Sababu ambayo Kama angemjulisha, Mwamvita angekaa upande wa shemeji. Akamwahidi Hilo halitakuwa kikwazo Cha yeye kumhudumia na kumtoa kwenye zahma ya kuozeshwa kwa babu Kisiki.

Kesho ya siku hiyo, Masu akapanda Basi kutoka Dar kwenda Morogoro, hapo Tena angetafuta usafiri wa kumfikisha kijijini Malonje. Mbali na hitaji la kumchukua Maureen ili aishi na Mwamvita, Masu aliwamisi familia yake. Miaka Ilikuwa imepita akiwa hajamuona mamake kipenzi. Alimmisi kuliko wengine wote.

Alfajiri Sana, Masu alijihimu na kuamka mapema, alipanda gari la Msango Exp lililofanya safari zake kutoka Moro mjini kwenda vijijini, kikiwemo Kijiji Chao Malonje. Kikawaida gari hizi hazikuwa Basi, zilikuwa Ni zile gari maalum za kubeba mizigo, canter na fuso. Hili alilopanda lilikuwa Ni fuso. Kutokana na haiba yake kubadilika, maana hakuwa Masu wa miezi kadhaa nyuma, aliamua kutumia haiba mpya kupata huduma ya kiwango Cha hadhi yake. si kwa ubaya, na Wala si kwamba maskini akipata sijui Nini kulia mbwata, hataa! Ukweli Ni kuwa hakuna anayeoga akarudi kugalagala kwenye tope. Masu alipewa siti kwa Dereva. Leo, alivalia suruali ya kadet ya kaki, iliyomkaa Vema, juu akaningiza fulana yake form six maridadi, iliyokuwa ndani ya jaketi saizi yake. Miaka ya nyuma, Masu alikuwa na kawaida ya kuvaa ovasaizi. Siyo kwa

kupenda lakini, uwezo wake ulimudu hayo maovasaizi aliyojichagulia kwenye mitumba iliyoletwa na mnada kijijini Malonje. Muda wake wa kuyavaa ulikwisha pita na Sasa ulihifadhiwa Vema kwenye kasiki la kumbukumbu, Kama hatua muhimu ya maisha yake.

Mvua kubwa ilinyesha na kufanya safari kuwa na mushikeli, hata hivyo baada ya vikwazo vya hapa na pale, Kama vile utelezi, kukwama, na hata pancha, Masu aliwasili kijijini Malonje. Aliposhuka, alikodi baiskeli impandishe nyumbani, kitongoji Cha mlimani. Hali ya hewa Ilikuwa njema. Kijani kibichi kila Kona. Maharage, mahindi, miti ya matunda, Malonje ilivutia Sana. Alipofika tu nyumbani, mbwa wao akawa wa kwanza kumlaki, akitikisa mkia kwa furaha na kumrukia rukia. Hali hiyo ya mbwa ndio iliwafanya mama yake na mdogo wake waliokuwa bize wakipepeta ngano, wabaini ujio wake. Na hata hivyo, walionekana kusita sita kuamini Ni yeye. Alikuwa amebadilika Sana.

'Kakaa!' Maureen aliita kwa mshangao!

'Hujambo mdogo wangu?' kusikia hivyo Maureen akamkimbilia na kumrukia, akamkumbatia Kaka yake kwa nguvu, Kidogo waanguke. Mama naye akajinyanyua chini kwa furaha, akamsogelea huku akiimba nyimbo za lugha yao, nyimbo za kumkaribisha mwanae nyumbani. Wakakumbatiana wote watatu kwa furaha.

Akakaribishwa nyumbani, wakatoa kiti Cha mbao Cha kukunjwa, kikakunjuliwa, Masu akaketi akinesanesa

kifalme. Ilionekana Kama Masu huyu waliyekuwa wanamuona Ni Masu tofauti na waliyemzoea. Ingawa ucheshi wake ulidumu naye, lakini hadhi yake Ilikuwa tofauti. Wakawa wanamwangalia kwa kuibia. Walimtamani. Maisha aliyoishi huko alikotoka walitamani wayaone. Wayaishi. Maureen, alikwisha amua kichwani, atamganda Hadi akubali kwenda naye. Kama Masu, Masu ambaye kuoga Ni Hadi anyeshewe zamani zile ametakata hivi, huko alikotoka ndiko kwa kuishi.

Haikuchukua muda kabla majirani kujua kuwa Masu karejea kijijini. Tetesi zilisema kijana huyo kawa mzuri kupindukia. Wote walitaka wamuone. Mama Saba yeye hakusubiri kumuona, alichotaka Ni mwanae Marietta kupata nusura ya kuolewa na kijana huyo, aliyekuwa gumzo kijijini masaa machache tu baada ya kurejea. Mwendesha baskeli alikuwa mpiga mbiu makini bila shaka.

'Marietta, we Marietta!!' mama Saba aliita kwa sauti. Marietta aliyekuwa jikoni akiosha vyombo, akaisikia sauti ya mamaye.

'Bee mama' akaitika huku akitoka kwenda kumsikiliza mama yake.

'Njoo mwanangu, njoo nikwambie!' mama Saba akaongea. Marietta akafanya hima kumfikia mama yake.

'Umeshamaliza kuosha vyombo mama?' mama Saba alimuuliza mwanae.

'Ndio namalizia mama'

'Anhaa, Sasa hivyo vyombo achana navyo. Cha kufanya, nenda kaoge uvae upendeze. Tutaenda kwa mzee Masuke. Yule kijana wake Masu nimeambiwa karudi. Nijuavyo Mimi, wakishaenda mjini, ukisikia wamerudi wakiwa tofauti na walivyoenda, wengi wanakuwa wamefuata jiko. Fanya hima upendeze na ujipendekeze kwa Masu mapema, kabla hajaona wengine. Mwanangu ulivyo mrembo, wewe ndio unastahili kwenda mjini. Jiandae mama ee!' mama Saba alimpasha Marietta. Marietta aibu ikamshika. Ingawa uhusiano wake na mama yake ulikuwa wa kirafiki mno, hili la Leo kuambiwa na mamake, lilimtia fadhaa Kidogo. Lakini, Marietta alimfahamu Vema Masu, walisoma na mdogo wake Maureen. Haikuwahi kuwa bayana kwenye ufahamu wake, lakini huenda alimpenda mvulana huyo. Kama sivyo, mbona alimuogopa bila sababu?. Mbona alipokutana naye alikosa kujiamini? Kwa Nini sauti ilimkauka kila alipotaka kumsabahi au aliposabahiwa naye? Mbona alimuonea aibu? Bado hakuwa na jibu. Na hapo, alikuwa anamtafakari Masu yule wa zamani. Hajamuona huyu Masu mpya!

# 8.

Kidogo Kidogo, familia ya mzee Masuke ilianza kupokea wageni. Mmoja, wawili, watatu, kadri muda ulivyosonga mbele, watu wakaongezeka. Hatimaye mikeka ikakunjuliwa na kutandazwa nje. Haikuwa Tena Siri, kwa mzee Masuke kulikuwa sherehe ya kumkaribisha Masu kutokea jijini Dar.

Huko mitaani watu walialikana, wakaungana wawili ama watatu wakaelekea nyumbani kwa mzee Masuke.

'Unaambiwa kijana Ana hela si Kidogo. Ameamua kuchinja ng'ombe wa kutosha kulisha Malonje na vitongoji vyake!' alisikika kijana mmoja akipasha wenzie habari njema za sherehe.

Lo! Heri Masu angelijua taarifa zilizoonea kijijini. Ajabu, wahusika wa sherehe wenyewe hawakujua wana sherehe!

Kutanabahi, muziki ukashushwa kwenye baiskeli, mitambo ikaunganishwa, muziki ukasikika. Alouleta muziki ndio kabisa akawashitua wale ambao hawakupata taarifa awali kujua kwa mzee Masuke neema imeshuka.

'Braza Kama utataka tukeshe utachangia elfu ishirini tu.' Dj alinongona sikioni kwa Masu.

'Kukesha kwa ajili ya Nini?' Masu akahoji.

'Ah Braza, kwani Una mpango wa kuzima muziki muda gani? Dj Yusto akauliza.

'Sina mpango wowote, muziki umekuja nao utauzima utakapoona vema.!'

'Hadi saa sita usiku, kawaida tunatoza elfu tano tu, na inakuwa burudani ya uhakika braza.'

'Sasa.,. Kwani aliokualika hapa nani? Sikia Dj, hapa hapana taarifa yoyote ya sherehe.,mie nikajua mmefurahi tu kuniona mmeamua kunikaribisha kistaarabu!?' Masu alizungumza na kuongezea

'Tangu lini mmeanza utaratibu wa kuvamia Nyumba za watu na kuwatoza fedha za muziki?'

'Bro Mimi nimefuatwa, nikaambiwa hapa Pana sherehe ya ukaribisho hivyo muziki unahitajika, wakanambia pesa nalipwa hapa hapa, Sasa nashangaa Tena unachosema!' Dj Yusto akalalamika.

'Ila, no sweat bro, naondoka na muziki wangu.'

Masu aligeuka nyuma akaona jinsi mama yake na wakina mama wengine walivyokuwa wamefurahi wakicheza ngoma ya kikabila iliosikika kwa ubora kutoka kwenye spika za Dj Yusto.

'Nikuombe tu uchangie hata buku nikalipe nishati. Sola na betri nimelazimika kukodi maana zangu zinatumika baa kwangu.' Dj Yusto akarai.

'Hapana, we gonga muziki Hadi watakapochoka!' Masu akaongea huku akiwatazama mama zake.

Hakutarajia hili. Lakini kwa vile kijijini vitu si ghali Sana, Masu akajikuta akiridhia sherehe iendelee. Tayari ng'ombe mnono alikuwa keshachinjwa bila hata yeye

kutaarifiwa, mwenye ng'ombe alikuwa katulia anasubiri kulipwa fedha zake.

Giza lilishaanza kuingia Masu alipomuona mzee wake 'Masuke mwana wa Miganda'. Hivyo ndivyo alivyojiita. Masuke Miganda Kama wazee wengi kijijini Malonje, alikuwa na familia za mitaala. Kwa maana ya wake wawili na zaidi. Habari za kijana wake Masu kurudi kijijini na kufanya sherehe kubwa, alizipata kilabuni alipokuwa anakunywa ngano na wazee wenzake. Mpashaji wa habari alisisitiza kuwa kila mwenye nafasi alikaribishwa huko nyumbani kwa mama Masu. Masuke wa Miganda kusikia hivyo akasimama kwa ufahari na kutangaza,

'Pombe yote iliyopo hapa, ibebwe ipelekwe nyumbani. Wazee wenzangu, leo tutakunywa pombe kwa hisani ya kijana wangu, Haya twendeni nyumbani.' Wazee wenzake wakasimama na kuambatana na Masuke wa Miganda.

Masu akashuhudia kundi la wazee nane walioambatana na mzee wake. Akafurahi. Ingawa Masuke wa Miganda alikuwa chapombe, alimudu kutengeneza mahusiano chanya na wanae. Aliwasomesha, alifurahia muda Pamoja nao na kuwapa mawaidha Haya na Yale kuwajenga. Hakuwa bahili alipokuwa na hela. Na, Kama Kuna kitu kimoja alichokijua mzee Masuke wa Miganda, Basi Ilikuwa Ni furaha na matumizi ya fedha.

Pamoja na ugumu wa maisha ya kijijini, kwa mzee Masuke hapakukosekana chakula. Na ilipopatikana fedha, kwa mzee Masuke Ilikuwa sherehe. Ndio maana Masu aliporejea akiwa kapendeza na kutakata, watu wakajua itakuwa sherehe tu. Wakatangaza sherehe.

Masu alimfuata baba yake na kumsalimia kwa heshima Pamoja na wazee wenzake alioambatana nao.

'Ah kijana wangu umenifurahisha Sana. Ona wazee wako Hawa wanavyofurahi, Ni kwa sababu yako. Na ashukuriwe Mungu kwa kukufikisha salama.'

'Asante Sana baba.'

'Masuke wa Miganda umejua kutengeneza urithi na hata wajionea vile utakavyoenziwa siku ukiwafuata baba zako. Kijana anapita kwenye njia zako kabisa. Hapa kijijini kila mtu anajua nyumbani kwa Masuke Ni nyumbani kwa sherehe!' alidakia mzee Albano na kumsifia Masu. Wazee wengine wote wakacheka wakitikisa vichwa vyao kuafiki kauli za mzee Albano.

'Asanteni kwa maneno mazuri wazee wangu na karibuni Sana. Vipi mwajionaje na Hali?' Masu akahoji.

'Salama kijana, furaha tu.' alijibu mzee Kisoka kwa niaba ya wengine wote.

'Asante Sana kijana wetu Masu kwa kuona umuhimu wa kutualika kwenye sherehe yako hii ya kumtambulisha mchumba wako. Hizi zimekuwa habari njema Sana maana umri nao unaruhusu Sasa. Hilo Ni Jambo jema Sana!' alizungumza mzee Rashid. Wazee wenzake wakaafiki kwa kutikisa vichwa vyao.

Masu alizidi kachanganyikiwa na habari zilizokua zinaendelea hapa. Yalikuwa yanaibuka mapya kila baada ya muda, uchovu wa safari ukaisha bila hiyana. Akalazimika kukabiliana na Haya yaliyokuwa yanatokea. Akataka akanushe lakini akaona si busara. Akajisemea moyoni;

'Nitamwita baba pembeni, nimkanushie habari hii wasije wakaamini Ni sherehe ya utambulisho wa mchumba.'

Busara hiyo hiyo ikamweleza ampe muda kwanza angalau awakaribishe wageni wake ndiyo afanye mpango huo wa ukanushaji habari.

Akatoka hapo, akaongee na mama yake kuhusu Hilo suala pia. Ile anageuka akakumbana uso kwa uso na Marietta. Ilikuwa Kidogo tu wavaane.

'Oh, samahani Sana, sikukuona!' Masu akatamka.

'Asantee!' Marietta akaitoa sauti yake tamu huku akitawaliwa na aibu zake, akawa anatafuna tu ukucha wa kidole chake. Marietta alijua kujipamba wee, jioni hii na Giza lake kwa mbali, yeye aling'ara kwa uzuri. Kwa sekunde kadhaa, Masu alipotezwa. Akazama kwenye wingu la fikra ghafla. Nadhani alijiuliza Kuna msichana mrembo kijijini hapa Kama huyu. Akili yake iligoma kumuachia aondoke zake.

'Waitwa Nani ewe mrembo?' Masu akatamka kwa huba.

'Masu jamani, umeenda mjini ndio umetusahau hata sisi tuliosoma Shule moja?' Marietta akajitia moyo wa

ushujaa, ule woga akajitahidi kuuondoa, japokuwa Ni Kweli moyoni kulikuwa na kitetemeshi kwa mbali, lakini alibaini si Kama enzi zile. Masu alikuwa mtanashati. Hakuwa yule Masu wa zamani. Marietta akakiri moyoni kuwa alimpenda kijana huyo. Akajishangaa vile leo alivyomudu kusimama na hata sauti yake kutoka bila hofu Kama zamani. Bila shaka safari yake ya Dar, Ilikuwa na mengi ya faida. Moja ikiwa Ni kumuondolea hofu, lakini pia ilimfunza kuvaa kisasa, na Hilo lilimpa kujiamini zaidi. Ndiyo, hata aliporudi kijijini Toka Dar, Marietta alikuwa habari mpya. Wanaume walimfuata fuata na yeye aliwakatalia, aliamini heshima ya mwanamke si kukimbizana na wanaume. Lakini, daa! Maisha Ni nyoso Sana. Ukikaa kizembe yanakutia kidole jichoni. Hakuwa na pesa za kudumisha usistaduu kijijini. Alipotafakari, akagundua hakutaka kuwa mwanakijiji aliyekuwa hapo awali kabla ya kwenda jijini. Akaona kudumisha usistaduu sharti awe na pesa. Angezipataje? Marietta akaweka mpango.

Mpango wake ulimhakikishia anapata fedha za kununulia viwalo na vipodozi. Walimu wa Shule ya msingi Malonje, walitoa hizo fedha, walimu wa kiume vijana na hata wale wenye wake zao. Na Wala walimu hao, hawakujua kuwa, Marietta alikuwa wao wote, wote Saba. Kila mmoja akifanya kuwa Ni Siri. Kisa Nini? Marietta alikuwa binti mdogo, na hakuna mwalimu Kati yao alitaka ifahamike anatoka na mtoto huyo. Marietta Sawa na Mwamvita, alikuwa na miaka 17 tu. Ni mama

yake pekee aliyeona binti huyo anafaa kuolewa. Na Sasa akawa anampambanisha na Masu. Umaskini mbaya nyie!

'Wee, Unataka kunambia wewe tumesoma wote pale Malonje Shule ya msingi?'

'Ndio bwana. Mimi nilikuwa darasa moja na Maureen. Sema Kuna kipindi nilienda Dar kwa dada ndio nikamalizia darasa la Saba, niliporudi wewe ulikuwa ushaondoka. Naitwa Marietta'

'Marietta mtoto wa mzee Thomas?'

'Ndio'

'Waoo! Dah tungekutana sehemu tofauti nisingekubali kabisa kuwa wewe unatokea Malonje. Mtoto unapendeza, unawaka Kama Malaika. Unawazidi hata waliopo Dar.'

'Asante' Marietta alijua kutumia sauti yake kuamsha hisia. Alipotamka Asante, Kuna vile alimvutia zaidi Masu, na kwa kutambua Hilo akajitia kuondoka. Ah wapi? Masu akamkamata mkono.

'Usiondoke Marii! Tunahitaji kuongea.' akatamka, mara, simu yake ya mkononi ikaita. Akavaa earphones masikioni ili kuipokea simu.

'Samahani kidogo.' akamweleza Marietta. Akaipokea simu.

'Hello!'

'Masu' Ilikuwa sauti ya Malkia wake Mwamvita. Sauti hii iliambatana na kilio Cha kwikwi. Kulikoni? Akajiuliza.

Akajisogeza mbali na Marietta.

'Kulikoni Malkia, mbona walia mpenzi? ee Kuna Nini mamii?'

'Masu wanapanga kunifungisha ndoa ya mkeka kwa hila, nimepata habari kutoka kwa watu wa jirani na familia ya mzee Kisiki, sijui nifanyeje Masu!'

Masu akili ikachanganyikiwa. Katika kutapatapa akamwambia 'subiri hapo dakika moja!'

Akaonekana kuzunguka hapa na pale Kama anayetafuta majibu. Akapiga simu Tena.

'Malkia, nakutumia pesa mpesa, Tumia Kama nauli uende Dar, Kuna mtu atakupokea.'

Alipomaliza mazungumzo hayo, hakukumbuka Tena Kama kulikuwa na Marietta akimngojea. Masu akatoka hapo kwenda chumbani kwake. Huko akapata utulivu wa kutafakari nani wa kumpokea Mwamvita. Dada yake, Maimuna. Akampigia simu na kumjulisha akampokee wifi yake. Hakumpa nafasi ya kuhoji.

'Ukishampokea mweke Lodge jirani na hapo kwako!' alitoa agizo akakata simu. Akafanya muamala na Sasa akapata ahueni nafsini mwake. Hapo tena, ndipo kumbukumbu ya Marietta ilipomrejea. Akatoka nduki kumfuata. Hakumuona.

Dj Masu alikuwa kafunga mitambo yake Vema. Nyumbani kwa mzee Masuke wa Miganda kuling'aa kwa taa za Sola na harakati za kufurahi, kula na kunywa ziliendelea Kama kawaida. Mara, kwenye spika

kukasikika sauti aliyoifahamu Vema. Sauti ya mzee Masuke wa Miganda.

'Mh... ah!' Mzee alianza kwa kusafisha koromeo ili sauti itoke vema, halafu akafanya kupuliza kwenye kinasa sauti, kujaribu ufanisi wa maiki.

'Ah, karibuni Sana wanamalonje nyumbani hapa tusherehekee ujio wa kijana wetu Masu. Nimeambiwa sherehe hii inahusika pia na utambulisho wa mchumba wake, Marietta binti wa mzee Thomas.' mzee Masuke akavuta pumzi kabla ya kuendelea. Akaachia mwanya kwa akina mama kushangilia kwa vigelegele na nderemo zikiwemo na mbija kutoka kwa vijana.

Tangazo Hilo likapokelewa kwa mshituko na Masu, lakini kwa mama yake Hali Ilikuwa tofauti kabisa. Alizimia baada ya kusikia tangazo Hilo.

Kwa upande wa pili, mzee Thomas mwenyewe ambaye pia alikuwa kwenye sherehe hii, alionekana akisukumana na watu wampishe njia, akielekea alipokuwa Masuke wa Miganda. Alionekana kujawa na Shari isiyo na kipimo. Labda, hili lilikuwa tangazo ambalo lilitolewa bila maelewano ya familia zilizohusika na hivyo mzee Thomas akaona anadhalilishwa. Labda! Ila kilichoanza Kama furaha kilikuwa kinaenda mrama.

## 9

Mzee Albano alimuona mzee Thomas alipokuwa anamfuata mzee Masuke akiwa kaghafirika anafuka Shari. Akaona kinachoenda kutokeza Ni aibu, akanyanyuka haraka na kuwafuata wazee wenzake kabla hawajachafua heshima ya wazee kwenye kadamnasi ile. Akaukaza Mwendo na kumfikia mzee Thomas na kuudaka mkono wake uliokuwa unarusha ngumi kwa mzee Masuke. Akaingilia Kati kile kilichoonekana kutaka kutokeza balaa.

Akawachukua wazee wale na kuingia nao ndani. Akiwatuliza hasa hasa mzee Thomas aliyeonekana kufura kwa hasira Kali. Mzee Masuke alipigwa na butwaa! Hakuamini hiki kilichokuwa kinaendelea hapa. Kumbukumbu yake ilimwambia hili suala lilikuwa na baraka za mzee Thomas, vipi Sasa ageuke mbogo? Hakuelewa.

Kitu Kama dakika kumi hivi kabla ya mzee Masuke kupanda jukwaani na kushika kipaza sauti, alikuwa amefanya mazungumzo na mkewe mzee Thomas, mama Saba. Mama Saba alikuwa amempa taarifa kuwa watoto wao, Marietta na Masu walimpasha habari kuwa wao wanapendana. Akataka kujua Kama mzee Masuke alikuwa na taarifa hiyo. Kwa mzee Masuke lilikuwa geni. Akamweleza kwamba alikuwa bado kupata nafasi

ya kuzungumza na mwanae. Lakini pia akamuuliza Hilo suala mzee mwenzie, mzee Thomas alilichukua vipi. Mama Saba akamwambia 'hana pingamizi' Yuko tayari kabisa endapo yeye mzee Masuke angeridhia. Masuke wa Miganda, labda kwa vile alikuwa keshachangamka kwa ile ngano aliyokunywa, hakuona haja ya kupoteza fursa. Vipaza sauti vipo, Nani mwenye maamuzi Kama SI yeye? Mama Masu atapata taarifa baadaye, na kilichompa kujiamini zaidi Ni ile habari kuwa kijana wake mwenyewe alikuwa karidhia. Akataka amfanyie hamaniko la furaha. Amshangaze kwa kutangaza habari njema.

'Wazee wenzangu, aibu gani hii mnataka kufanya hapa, mbele ya jamii nzima, mnataka kuonesha Nini wazee?!' mzee Albano alizungumza kwa hisia.

'Huyu Bwana Ni mpuuzi Sana huyu. Na ningemuonesha kazi leo!. Anaanzaje kumtangaza binti yangu hadharani kwa suala Kama hili? Anajipatia mamlaka ya kumtangaza binti yangu bila hata kuwasiliana na Mimi? Upuuzi gani huu.? Mwanangu nimemlea katika maadili,Leo huyu Bwana anajifanya yeye ndiye mwenye maamuzi ya kumuozesha kijana wake? Ndo utaratibu gani huo.?' mzee Thomas alikuwa na hasira Kweli Kweli!

Masuke wa Miganda aliinamisha kichwa chini kwa Soni. Maneno ya mzee Thomas yakamwingia na kumsuta. Akajutia kukurupuka kwake. Ama Kweli shibe mwana malevya!

'Ya Kweli Haya mzee Masuke? Kwamba hata bila kuwasiliana na mzee mwenzio wewe umeona fahari kujichukulia maamuzi? Umesahau tamaduni na Mila zetu?' mzee Albano Sasa alizungumza kwa jaziba. Kama Kweli mzee Masuke alifanya hayo bila kuwasiliana na mwenzake, alikuwa amemkosea Sana mzee Thomas.

'Wazee wenzangu nikiri kwamba nimeteleza. Na kuteleza kwangu kumetokana na mazoea mabovu. Nilisahau kwamba Mila zetu zinatutaka sisi wanaume ndio tufanye maamuzi. Nikajikuta nimempa sikio langu mama Saba, ah nimekuwa dhalili kwa kusahau ya wahenga!. Mkeo, amenihakikishia mlikubaliana, na Mimi ndio mlikuwa mwataka kusikia nasemaje, Kumbe Ilikuwa tamanio tu la mama Saba vijana wetu waoane? Ah, mzee Thomas Nisamehe Sana ndugu yangu. Tuliangalie suala hili kwa jicho lingine tafadhali. Bado tunaweza kuzungumza na kuwapa baraka vijana wetu Kama wamependana wakaanzishe familia zao.' Masuke wa Miganda alionesha uungwana.

'Umemsikia mzee mwenzio, Kumbe naye kauingia mkenge tu. Hebu yamalizeni Haya kiungwana wazee wenzangu.' mzee Albano alitoa Rai.

'Wanawake, wanawake. Mama Saba Mara ngapi nimuonye kuingilia majukumu ya wanaume? La! Shida hii. Lakini hata hivyo, mzee Masuke, Mimi na wewe hatuwezi kuoleana kabisa. Wewe na Mimi mwiko kabisa kuoleana.' mzee Thomas alizungumza huku akijaribu kutafuta kigezo Cha kuweka kikwazo kwa wao

kuoleana. Hakikuwepo. Siri ya siku nyingi Ilikuwa ifichuke kama angesema Sababu..

'Kwa Nini iwe mwiko, Mimi na wewe hatuna udugu wowote, mbona iwe mwiko kijana wangu kumuoa binti yako?' Masuke wa Miganda akatahamaki. Hayakumwelea Haya! Mara, mlangoni akasimama mzee Kisoka na kutamka maneno yaliyoahirisha kikao kile Cha usuluhishi.

'Wazee wenzangu, Kuna shida Kidogo imetokezea. Mama Masu Yu nusu kaputi hivi navyoongea. Hebu tuone namna gani tunasaidia Kidogo.' Wazee wakanyanyuka na kumfuata mwenzao. Lo! Kizaazaa!

'Mama Masu kimempata Nini? Hajawahi kuzimia Leo anazimia, shida Nini hasa?' Masuke wa Miganda alijiuliza bila kupata' majawabu.

Sherehe Ilikuwa imeingia dosari. Kila mmoja alionekana kuhaha na kushangazwa na matukio yaliyokuwa yanageuka geuka. Minong'ono ikasikika, watu wakiongea hili na lile. Kuna waliosema, Kuna uwezekano mtu mbaya kaona wivu kamtupia jini kuharibu sherehe. Lakini wapo walioenda mbali na kutoa kauli za tuhuma nzito dhidi ya Masu

'Wewe Unadhani huu utajiri Masu kautoa wapi? Fikiria, ametoka hapa juzijuzi tu, Leo anarejea akiwa tajiri, Tena hakai hata siku moja, anaweka sherehe kubwa Kiasi hiki! Hamjiulizi tu? Huyu atakuwa kapata pesa za manyoka. Mtanambia Kama hajamtoa kafara mama yake. Hawa wakishaenda mjini tu, kazi yao Ni

kujiunga Freemason. Haipiti mwaka unasikia mtu wa karibu kaaga dunia.' alisikika mama mmoja akisimulia kikundi Cha wanawake.

'Wee, ndiyo maana anavaa bonge la Pete kidoleni. Ah kwa Kweli pesa za majoka mie aku sizitaki!' msichana mmoja alidakia akishika kiuno chake na kukitikisa kwa nyodo.

'Hebu huko, hivi nyie kazi yenu kuongea ya wenzenu tu.! Watu wazima hamfanyi kazi, kazi kuzusha maneno tu. Kuna mwenye uhakika na msemacho hapa? Na mkishamchafulia jina nyie mwafaidikani?' Ilikuwa sauti ya Marietta akiwazodoa wazushi. Moyoni alijaa tele Masu, hakutaka kusikia habari za kumchafulia sifa mahabuba wake.

***

Masu alipopata taarifa ya mama yake kuzimia tu, haraka haraka, alikodi baiskeli ili kumuwahisha dispensari.

Akajikuta anajutia uamuzi wake wa kutowaambia wazee, juu ya habari za mchumba, kwamba hazikuwa za Kweli. Akadhani kuwa tangazo lile lilisababisha hayo madhila.

Alikokota baskeli akisaidiwa na Kaka yake, kwa mke wa kwanza wa mzee Masuke wa Miganda, aliyejulikana kwa jina Miganda. Ilikuwa Kama utaratibu wa kikabila wazazi kuwapa watoto majina ya ndugu zao waliokwisha kutangulia mbele za haki.

Miganda alisukuma baiskeli, huku Masu akimshikilia mama yake kumpa balansi. Maureen na dada zake, na wakeze Masuke wa Miganda, kwa Pamoja walionekana kuhuzunika Sana na walionesha ushirikiano mkubwa. Tukio hili liliwaweka wakeze Masuke wa Miganda Pamoja Kama familia.

Kwa mbali, Masuke wa Miganda na wazee wenzake walikuwa wanajongea kuwafuata wale waliokuwa na baiskeli. Kimya kilitawala Kati yao.

SI mzee Masuke tu aliokuwa na wasiwasi juu ya mkewe. Yeye alikuwa hajui Nini kimempata mkewe, lakini mzee Thomas alihisi lile la tangazo la awali ndio sababu. Alijua mshituko alioupata mama Masu, utakuwa ulipelekea Hali hiyo. Kwa sababu hata yeye, Ni kujikaza kiume tu kulikosababisha asidondoke chini. Mzee Thomas alikuwa na Jambo lililomfanya awe mwenye huzuni zaidi. Walikuwa wanamalizia kamtremko, jirani na kwa mzee Albano, hatua chache kutoka nyumbani kwa daktari wa kijiji bwana Mgode. Mama Masu akapiga chafya! Akafunua macho Kama atokaye usingizini.

'Ameamka, ameamka!' Masu akajikuta anaimba kwa furaha na kumkumbatia mama yake. Kumbato lake likamnyima hewa mama yake. Ilimlazimu Miganda kumtandika ngumi ili kumpa taarifa ya janga alilokuwa asababishe. Masuke akashituka, akajitoa kwa mama yake, mama akapata nafasi ya kupumua.

'Pole mama!' Masuke na Miganda wakatamka kwa Pamoja.

'Kimenipata Nini. Mbona mmenibeba kwa baiskeli utadhani mgonjwa?' mama Masu alihoji.

'Usijali utakuwa Sawa tu. Ni mshituko ulikupata halafu ukazimia'

Taratibu kumbukumbu zikarejea.

'Naona Niko Sawa, tungerejea tu nyumbani.!' akatamka kwa huzuni. Kuna kitu kilimtia hofu moyoni, au kilikusudia kumnyong'onyesha kabisa. Kwa muda wote huo walipokuwa wakizungumza, walikuwa Sasa wamesimama.

Mzee Masuke na wenzake waliwafikia mama Masu na wanawe. Wote wakionekana kushusha pumzi za 'Oh afadhali, Asante Mungu'. Kila mmoja alikuwa anasema pole, pole. Mzee Masuke akapata taarifa ya mkewe kutaka warudi nyumbani. Hakuiafiki.

'Kwanza tumuone daktari Mgode, akufanyie vipimo, aangalie shida Ni Nini na ikibidi atuambie chanzo Cha shida hiyo ndio Sasa turejee nyumbani.' akahitimisha. Safari ya kwa daktari Mgode ikaendelea.

***

Mwamvita aliamka alfajiri mapema kwa ajili ya sala. Akamwandalia baba yake chai na vitafunwa. Baadaye saa moja hivi, alikuwa na mpango wa kuondoka nyumbani. Akili yake ilitawaliwa na habari ya kutoroka

tu, kwani habari ya kuolewa na mwanaume makamo ya babake haikumwingia akilini.

Alimweka Sawa dada wa kazi. Kawaida walitumia huduma ya dobi Nyumba ya tatu Toka pale. Kazi ambayo ilifanywa na Husna, dada wa kazi, kubeba lundo la nguo chafu na kwenda kuziosha kwenye mashine hapo kwa dobi Juma. Kwenye mzigo wa nguo zile chafu, nguo na begi lake vilitangulizwa mbele. Mwamvita angezipitia na kuanza safari ya kuelekea feri ili kuabiri boti kwa safari ya kuingia jijini Dar. Lakini shida ikawa kujulikana. Nani hakumfahamu Mwamvita mtaani Kwao. Mtoto wa shekhe Abuubakr? Akamuwaza Masu, vile angekuwepo amsaidie kuibeba, ili asiulizwe 'aenda wapi Tena', au kuambiwa, ah 'Wenda bara?'. Wazo Hilo likampatia njia. Akachukua simu yake, akatafuta jina, Bakari, akaliona,akampigia!

'Halo' simu ikapokelewa, na sauti ya Bakari ikasikika. Aliifahamu Vema sauti hiyo. Sauti iliyowahi kumpasua moyo kwa taarifa ya majonzi, ilipomtaarifu kuhusu kutekwa kwa Masu. Ni kipindi hicho walipobadilishana namba ili kutaarifiana habari za Masu Kama angepatikana.

'Shem wangu najua nimekuangusha! Kusema Kweli bado sijapata fununu wapi alikopotelea Masu…' Bakari hakumalizia Maelezo yake. Mwamvita akadandia mazungumzo yake.

'Shemu Nina shida, nahitaji msaada wako tafadhali. Kuna mzigo wa kubeba, waweza kuja?'

'Naja Shem, wapi upo?'

'Njoo kwa Juma dobi'

'Nipo njiani'

Tangu Masu alipomweleza habari za Mzungu, kwamba kulikuwa mchongo, Bakari hakupata kusikia Tena habari yoyote kutoka kwa Masu au Yusuf. Wiki zikakatika, juhudi za kuwapata rafikize hao hazikuzaa matunda. Kutokana na wimbi la watu kupotea, kutekwa na hata kutoweka lililokuwa limeikumba nchi, Bakari, alipoulizwa juu ya Masu na Mwamvita, akajikuta ametengeneza sababu rahisi kueleweka, 'Masu alitekwa na wasiojulikana!'. Hata hivyo, Bakari alihisi M'bara atakuwa aliamua kurejea Kwao kuuepuka msala wa kutia mimba mwanafunzi.

Dakika tano zilimwezesha Bakari kumfikia Mwamvita. Walikutania kwa dobi Juma. Wakaongea mawili matatu, kusabahiana na kujuliana Hali. Kisha mdogo mdogo wakaanza kutoka, Bakari akiusukuma mkokoteni wao 'motofaya'. Hawakujua hawajui.

Zile habari za mipango ya kuozeshwa kwa mzee Kisiki, hazikuwa utani. Mwamvita alikuwa mwali. Alitakiwa kukaa ndani wakati mipango ikiendelea. Mzee wake sheikh Abuubakr, hakutaka kufedheheshwa kwa Mara ya pili. Aliweka ulinzi kwa bintiye bila Mwamvita kuwa na taarifa.

Habari ya Mwamvita kukutana na Bakari ilimfikia mzee Abuubakr. Aliyempasha hakumweleza utofauti Kati ya Masu na Bakari. Hivyo sheikh Abuubakr,

alijihimu kuondoka dukani kwake na kuelekea kituo Cha polisi kutoa taarifa na kupata' Askari wa kumkamata mhalifu, kijana aliyetia mimba bintiye mwanafunzi.

Hawakujua kilichokuwa kinawapata muda mfupi ujao. Ilikuwa ghafla tu, Askari alitokeza mbele yao na kuwaweka chini ya ulinzi. Bakari na Mwamvita hawakuamini kilichotokea. Walikumbwa na fadhaiko. Hawakujua Nini Cha kufanya. Bakari alichukuliwa kupekekwa polisi Asijue kosa. Sheikh Abuubakr alikuwa mbogo, amefura kwa hasira.

'Afande, huyu anayetia mimba wanafunzi, afungwe kwa mujibu wa sheria, tutashirikiana kukamilisha ushahidi.' Sheikh Abuubakr alitamka, tamko ambalo Sasa lilimwamsha Bakari juu ya balaa lililomkumba. Hakuwa na kosa, wema wake ulikuwa unamponza. Akajaribu kutaka majibu, akamkazia macho Mwamvita, 'kulikoni?', macho yake yaliuliza, Mwamvita hakuwa na jibu.

'Nakuapia sikulijua hili Bakari.' Mwamvita akajibu huku chozi likimdondoka,wakati huo sheikh Abuubakr alikuwa anamvuta mkono bintiye kuondoka kituoni.

## 10

(Zamani za ujana wa wazazie Masu)

Kwa kawaida Mnada wa bidhaa mbalimbali ulifanyika kijijini Malonje siku ya jumamosi. Janice alikuwa mrembo, lakini hakuruhusu ulimbwende huo umfanye tegemezi. Alikuwa mchakarikaji Kweli Kweli. Mjasiriamali. Mwanamke mchakarikaji. Ijumaa hii Ilikuwa Ni miongoni mwa ijumaa kadha zilizompeka mjini Morogoro kujichagulia mabelo ya nguo za watoto na wanaume, kwa ajili ya kuyapeleka mnadani huko Malonje. Soko lilikuwa zuri, hasa miezi ya tano, sita, Saba Hadi nane. Ni kipindi ambacho wanakijiji wachapakazi wa Malonje walikuwa wanavuna mazao yao. Pesa zilikuwepo za kutosha mifukoni mwao, hata wakawepo waliowehuka kwa wingi wake, kiasi kwamba ungekaa kizembe, Basi wangeweza hata kukuzaba makofi, na kwa kiburi, wangekuzaba Tena halafu uulizwe Unataka kulipwa sh'ngapi!

Janice, kwa wastani kipindi Cha miezi hiyo aliuza Sana, Tena kwa Bei iliyomrudishia mtaji, na faida Mara mbili au tatu, ukitoa fedha ya nauli, chakula na malazi. Alikuwa na uhakika wa kuuza zaidi pia kwa sababu, ukiachana na lugha yake ya mvuto kwa wateja, yeye

mwenyewe alikuwa na mvuto hasa kwa wanaume. Hao walikuwa wateja wake wakubwa. Wengi waliamini kwa kuwa wateja waaminifu kwa Janice kungewapa ngekewa ya kukubalika kirahisi siku za usoni. Wakaendelea kuishi kwa Imani, huku Janice akitengeneza faida maradufu.

Janice hakuwahi kumkatalia mwanaume yeyote kijijini pale aliyejitokeza kumtongoza, ila vigezo alivyowapa hao watongozaji, ndivyo vilivyowakwamisha kumpata. Na Mara nyingi Janice alijua kuwafanya hao kuwa waaminifu kwenye uteja wao wakitarajia siku moja watafikia vigezo vyake. Kwa njia hiyo, Janice hakuwa na adui, Bali alijitengenezea marafiki wengi miongoni mwao hao wanaume. Lakini pia, kwa wale majasiri waliopendelea kuonesha umwamba wao, wengi walitoka kimaisha baada ya kuingia kwenye ligi ya kumuwania Janice.

'Ah Janice, mtoto mzuri. Nakuahidi vigezo vyako nitavifika tu, siwezi kukukosa asilani. Nambie, u Hali gani mrembo?' Ilikuwa sauti ya Masuke wa Miganda.

'Niko poa Masuke, Leo nimekuletea bidhaa adimu Sana. Mahsusi kwa ajili yako. Tena usimwambie mtu. Hebu shika hii kwanza, halafu nambie waionaje? Hayo ndo mapigo ya vijana sasa.' Janice alizungumza huku akimkabidhi suruali ya jinsi la bluu. Ilikuwa nzuri, na Masuke alivutiwa nalo Sana.

'Janice unajua kunishika pabaya we mtoto, utaja nifilisi ujue, wakati ndio kwanza nachipukia kwenye utajiri wangu. Hii unaitoaje?'

'Elfu kumi TU, Na hapo Ni kwa sababu wewe Ni mshikaji wangu. Kawaida naziuza hizi kwa shilingi ishirini na tano.' Janice aliongea kwa sauti ya chini akimnong'oneza Masuke wengine wasisikie.

Masuke alizama mfukoni mwa suruali yake na kuibuka na shilingi elfu tano. Akamshikisha kwa kificho na kumnong'oneza Janice.

'Sina ziada na suruali hii Ni mahsusi kwa ajili yangu, naanzaje kuiacha Sasa?. Asante kwa hii zawadi!'

Janice alikuwa mjanja, lakini alikiri Masuke alikuwa mjanja zaidi yake.

Kwa miaka miwili, Masuke na Janice walionana mnadani kila ulipokuwapo Mnada kijijini pale. Wakati huo Janice alikuwa anatokea mjini Morogoro ingawa alikuwa mwenyeji wa kijiji jirani na Malonje. Mazoea yakawafanya marafiki walioshibana. Utani wa Masuke, ulikuwa kitu kingine kilichomfanya Janice kuvutiwa naye. Hata ilitokea kwamba Masuke alitoweka ghafla kijijini. Hakuna aliyejua alipopotelea kijana huyo. Janice akahisi Kuna kitu hakikuwa sawa. Alijihisi upeke na upweke! Alimkosa na kumkosa huko kukalinyausha tabasamu lake. Akawa hutabasamu tu kimazoea, lisiwe Ni tabasamu halisi lililompa furaha ya Kweli. Alimpenda kijana huyo!

Miezi kadhaa mbele, karibia mwaka baada ya kutoweka kijijini, Masuke alirejea kijijini. Akakutana na kisanga. Uamuzi ulifanyika Kwao. Familia yake haikujua Kijana wao alipopotelea, na kwa tamaduni za

wanamalonje, mtoto wa kiume, sharti kuwa na familia. Awe kazaliwa mlemavu, awe na mtindio wa ubongo, haikujalisha. Mwanamke aliozwa kwenye familia ya kijana huyo, ili tu, kuendeleza kizazi kwa jina la ndugu yao ambaye angekuwa na mojawapo ya sababu hizo. Uchizi, ulemavu, kifo kabla ya kuoa, kupotea iwe vitani au kupotelea mbali na jamii hiyo. Jina la mtu huyo lingeenziwa tu. Ndugu wa mhusika, walihusika kuzaa na mwanamke aliyeozwa ndugu yao, majina ya watoto wangeitwa kwa jina la ndugu yao huyo alokumbwa na hayo madhila tajwa.

Aliporejea akakutana na habari za mke. Alikuwa na mke. Wakamkabidhi. Akampokea. Maisha yakaendelea. Lakini, yeye alikuwa bado hajaridhika Hadi atimize ahadi yake. Ahadi ya kumpata Janice.

Jumamosi iliyofuata, Masuke akaenda mnadani. Akamuona Janice akiwa kwenye jukwaa lake la kunadi mavazi. Akafurahi kumuona. Akiwa mbali, furaha ya kumuona ikimkereketa moyoni, akashindwa kuizuia furaha hiyo. Akaita kwa sauti kubwa jina la Janice. Janice alipomuona Masuke wa Miganda, furaha ikamwingia. Akaweka nguo chini, akatoka mbio kumlaki Masuke. Wakakumbatiana kwa furaha kila mmoja akionesha alivyokuwa amem-miss mwenzie.

'Nimekidhi vigezo, nimekamilisha ahadi. Je Janice, binti wa mzee Petero, utakubali nikuoe?' Masuke wa Miganda akahoji, walikuwa wameingia kwenye banda la Janice, alimohifadhi bidhaa zake. Mabelo ya mitumba.

Juu ya Belo moja akaweka kijifuko Kidogo, kilichoshonwa Kama hirizi, ndani kilikuwa na madini aina ya almasi. Punje moja yenye ujazo wa karati mbili ushei hivi. Kumbukumbu ikapita kichwani mwake Janice. Akakumbuka vigezo alivyompa Masuke wa Miganda,

'Kunioa Mimi gharama Sana Masuke, ukiweza vigezo, hata Sasa, leo hii unanioa Mimi binti wa Petero.' ndivyo alivyoanza kumbabaisha.

'Vigezo gani mpenzi?' Masuke akauliza kwa upole.

'Nilitee Almas yenye ujazo wa karats 1 angalau.'

'Mh, Kama hunipendi ungesema, kwa Nini unipe mtihani unaojua nitafeli?'

'Kama wanipenda hutafeli.' Janice aliongea kwa msisitizo, akamwangalia kwa namna iliyoonesha kumsuta kijana wa watu.

'Kwa uwezo wa mola mtukufu, nitaileta almasi. Utakuwa wangu.' mazungumzo hayo yakapita kwa Kasi akilini mwake Janice alipoyakumbuka.

Masuke wa Miganda hakujua tu. Janice Petero, alikwishampa nafasi hata kabla ya hizo almasi. Kilichodhihiri wazi, Ni Kweli kwamba kuja kwa almasi kulimfanya awe mwanaume kamili kwa Janice. Hatimaye Masuke wa Miganda na Janice binti Petero, wakaoana. Hakuona shida kuwa mke wa pili!, Alimpenda Masuke.

Mwaka mmoja ukapita, Janice na Masuke hawakujaaliwa mtoto. Mke wa kwanza, tayari alikwisha

jifungua mtoto wa kiume. Waliyempa jina, Miganda. Jina la marehemu babu yake Masuke.

Almasi ile, Janice aliihifadhi. Ikafika kipindi akaona heri waiuze, wabadili maisha, labda ingemsaidia Janice kuwa na maisha yenye heshima. Alitafuta heshima kwa sababu, tayari maneno maneno yalianza kuwa mengi kutoka kwa watu wa Malonje, wakihoji kwa Nini hakumzalia Masuke watoto. Wajuaji wa Mambo wakayafichua Yale waliyojifanya kuyajua, ili kujenga hoja zenye mashiko. Wakadai, huko mjini alikokuwa anafuata mitumba ya kuuza, (maana Sasa alikuwa na duka kubwa kijijini Malonje), basi kulimharibu, kwa sababu huko wanawake walikuwa sawa na wanaume. Walitumia dawa za kuzuia mimba ili washindane kibiashara na wanaume. Wakahitimisha kwa kumtuhumu Janice kuwa alikuwa kwenye kundi la wazuia mimba. Hali hiyo aliipuuza mwanzoni, lakini moyo umeumbwa kwa nyama laini, Ni mwepesi kuhisi furaha, lakini Ni mwepesi zaidi kuhisi maumivu. Alianza kuhisi maumivu, akapoteza uchangamfu. Hapo ndio alipata Wazo la kuiuza almasi aliyozawadiwa na Masuke wa Miganda.

Janice akamshirikisha Masuke Wazo lake. Masuke wa Miganda akamwambia ruksa kufanyia chochote hiyo almasi maana alimletea yeye na Ilikuwa yake. Akamkubalia kuiuza ili wafungue duka kubwa mjini Morogoro. Alitaka atoke kijijini, ajiepushe na maneno ya waja!

Alipata habari soko la almasi yake lipo jijini Dar es salaam. Akafunga safari kwenda huko. Mjini Morogoro, akapanda Basi la Abood, kiti Cha jirani yake kilikuwa wazi. Wakati gari linaondoka, mwenye kiti akatokea, hakuwa mwingine, alikuwa mmoja Kati ya wateja wake waaminifu. Thomas Mogetango. Alifahamika zaidi kwa jina la Thomas Waa. Jina la pili halikufahamika Sana.

'Waa! Cheki nayekaa naye leo?' Thomas akachombeza.

'Thomas mzee wa waa!' Janice akatamka kwa bashasha.

'Waenda wapi Janice, na wapi umemuacha mumeo?'

'Nilikuwa nikuulize swali Hilo hilo, umemwachia Nani mkeo?'

'Ah, Kuna kazi nimeitiwa na rafiki zangu. Nataka nikaicheki.' Thomas Waa Kama alivyojulikana zaidi, kutokana na kupenda kutumia mshangao wa 'waa!' alikuwa Ni fundi mwashi. Rafiki zake walikuwa wamepata dili la kujenga Nyumba ya daktari huko Mbande jijini Dar. Hivyo, Thomas Waa alikuwa njiani kufuata ajira hiyo ya muda.

'Oh, hongera bwana, hongera Sana'

'Asante Sana Janice, tunaomba Heri tu kwa Mungu. Enhee, Kama kawaida yako, Mambo ya biashara siyo?'

'Ndiyo Toma, sema hii ndiyo Safari yangu ya kwanza kwenda jijini.'

'Oh, na Mimi nikajua wewe Ni mwenyeji!'

'Hataa, Sina uwenyeji wowote na Hilo jiji!'

'Sawa, enhe nambie, ukanipa vigezo wakati navikamilisha nikasikia umeolewa na Masuke. SI ungenambia ukweli TU jamani?' Thomas akaitua lawama yake. Hata Sasa, Thomas alionekana bado anamhusudu Sana Janice.

'Ooh! Pole. Ulifanikisha lakini?'

'Ndio, na kusema Kweli ndio màana sikulaumu kabisa. Nilichelewa mwenyewe, lakini nashukuru bidii ya kutafuta kigezo chako ilinipa badiliko kubwa, ndio maana unaona hatua nilizopiga. Bila shaka unakubaliana nami kuwa Mimi ndiyo mjanja pekee kijijini mwenye kumiliki jengo la maana, ramani ya ulaya, paa la msauzi. Bila wewe kunipa ile changamoto, bado ningekuwa naishi kwenye kile kibanda changu Cha awali. Najivunia hatua hizo, ila bado nakosa furaha kamili. Nakukosa wewe mrembo.'

'Eboh! We mwanaume wewe, huna aibu? Mie mke wa mtu. Shemeji yako Sasa!' Janice alizungumza akiigiza ukali, lakini ikawa Ni kituko ambacho waliishia kukicheka wote. Mazungumzo yakanogea wawili hao. Walipowasili jijini, Janice na Thomas wakajikuta kwenye Nyumba moja ya kulala wageni. Roho iradhi lakini mwili Ni dhaifu. Udhaifu wao ukawazidi nguvu. Siku hiyo ikawaweka Pamoja kwa huba. Kesho yake, wakaagana huku wakiapizana kuwa hiyo ingekuwa Mara ya kwanza na ya Mwisho ili kulinda heshima ya ndoa zao.

Walipokutana Tena kijijini,Ilikuwa Ni miezi miwili tokea walipokutana kimwili jijini Dar. Janice alikuwa Ni mjamzito.

***

Ukweli kwamba Masu alikuwa kijana wa Masuke wa Miganda ulikuwa uongo ulioishi kuaminiwa kuwa Ni Kweli. Ukweli huo ukilindwa na Siri iliyobebwa kwa dhati na mioyo ya watu wawili. Janice mama mzazi wa Masu na Thomas baba mzazi wa Masu. Tangazo la Masuke wa Miganda, lilikuja Kama tetemeko lililotishia kuing'oa Siri hiyo katika msingi wake imara. Moyo. Moyo wa Janice, ulizima kwa sekunde. Ukatikiswa Kidogo ung'olewa. Asingeruhusu mtu na dada yake kuoana. Laana kubwa hiyo! Lakini pia asingeruhusu Siri hiyo kuwekwa wazi.

Aliporejelewa na fahamu zake, mama Masu aliapa moyoni kupinga mahusiano Kati ya Masu na dadake Marietta. Potelea mbali kuchukiwa na mwanae. Alipanga kutishia kuacha radhi Kama Masu angeshupaza shingo yake.

Daktari Mgode baada ya kumpima mama Masu alimwandikia dawa za kutuliza maumivu, ingawa hakukuwa na ulazima huo. Lakini, watu wa Malonje usipowapa dawa, hawakubali kuwa u daktari makini. Mgode aliwaeleza kuwa Ni mshituko wa kawaida ambao ulitokana na kusikia taarifa ambayo hakupendezewa nayo.

Wakarejea nyumbani. Ilikuwa yapata saa sita za usiku. Mbalamwezi ikiuangaza ulimwengu kwa mwanga wake akisi. Masu akawalipa wadeni wake. Dj Yusto, mwenye ng'ombe mnono. Muuza mchele, muuza nyanya na vitunguu, kila aliyeorodhesha Deni akalipwa. Jumla zikatumika laki nne na ushei. Mfukoni akabakiwa na Kiasi Kama elfu themanini hivi. Akaazimu kukikimbia Kijiji.

Kesho yake, Masu akapata muda wa faragha na mamake, Janice.

'Hizi habari kwamba unamuoa binti wa mzee Thomas, Zina ukweli gani?' Janice akamhoji Masu.

'Kwa Kweli sijui hata zilianzaje, labda mzee anaweza kuwa na majibu na hili swali mama!' Janice roho ikadunda kwa tumaini jema.

'Wewe umezipokeaje?'

'Dah nilishituka Sana mama, Kama Ni sapraizi, Basi haikuwa njema hata Kidogo!'

'Kwa Nini wasema hivyo?'

'Nilidhani ingekuwa Bora kushirikishana kabla ya kuliweka mbele za kadamnasi. Huwezi jua, unawezakuta binti Ana mchumba tayari, fikiria huyo mchumbaake anamchukuliaje Sasa? Na huyo binti je? Haikuwa nzuri kwa Kweli. Na… na kusema Kweli mama, Mimi tayari Nina mchumba tayari, muda usiozidi miezi mine hivi mtaitwa babu na Bibi!'

Habari hiyo, japo kuwa haikuwa imezingatia Mila na desturi zao, ilimpa faraja mama Masu na kumrejeshea tabasamu lake halisi.

'Alulululuuu!' mama Masu akapiga vigelegele.

'Anaitwa Mwamvita, mzanzibar, wazazi wake Ni chotara wa kishrazi na kitumbatu.'

'Mie nakutakia Heri mwanangu, yote ya Mungu, kwa vile yameshakuwa hivyo, hatuwezi kubadili matokeo. Ila mwanangu, nakuasa baba, asilani asilani usijekufikiria mahusiano na Marietta. Tafadhali Sana unisikie mwanangu. Hilo tu ndilo nakuomba. Uwe Masu wangu anisikilizaye, nakutakie mema mwanangu. Nakukanya kwa Heri kabisa.' mama Masu akasisitiza.

'Nimekusikia mama.'

'Asante mwanangu, nakuamini. Nachukua kauli yako Kama Kiapo!'

'Ninakuahidi, nitakaa mbali naye. Pia nitumie muda huu kukujulisha kuwa Kesho nitakuwa safarini kurejea Zanzibar. Nahitajika kibaruani keshokutwa.'

Masu hakutaka kubishana au kujua kiundani, kwa Nini alikuwa anakatazwa mahusiano na Marietta. Hata hivyo, kwa kazi yake, asingemudu kuwa na wake wawili. Huyo mmoja tu alilazimika kufanya Siri uwepo wake. Kumbukumbu ya maelekezo ya master Park Hye Ilikuwa Moto bado akilini mwake.

'Oh jamani, na Mimi nikidhani tunao muda mwingi wa kuwa nawe?' mama Masu akalalama.

'Ningependa iwe hivyo, lakini kazi, kazi zenyewe za wazungu, hawapendi kupoteza muda kabisa.'

'Ah, sawa mwanangu, nashukuru kwa zawadi na kutukumbuka mwanangu. Ubarikwe Sana mwanangu. Iwe Heri unapoenda kuanza kazi yako. Ukafanikiwe mwanangu.'

'Asante Sana mama. Nanyi pia mbarikiwe. Lakini, ninalo ombi pia. Kwa Hali aliyonayo mkwe wenu, anahitaji usaidizi kwa karibu Sana. Nilitaka nimuibe Maureen akamsaidie kipindi hiki Cha kuelekea kujifingua.'

'Hapana, mlete nyumbani hapa, mamako mkubwa Ni mkunga, akiwa hapa atakuwa Salama. Mie Sina Imani na Mambo ya mjini. Siku hizi kila mzazi anayejifungulia hospitalini utasikia operesheni. Mbona huku Wala si lazima hizo operesheni? We mlete tu nyumbani. Maureen nenda naye ili arudi naye. Na lini Sasa sisi tutakutana na wazazi wake?.!'

'Ngoja kwanza ajifungue, halafu tutapanga tu.'

'Vipi lakini, wazazi wake wako radhi na uhusiano wenu?'

'Hilo ndilo suala gumu Kidogo. Hawanijui bado na hivyo sijui Kama wataridhia au la! Nisingeweza kujitambulisha, ningekamatwa kwa sababu alikuwa mwanafunzi bado, kidato Cha nne. Ila.. alifanikiwa kufanya mtihani bila kushitukiwa.'

'Mhh!' mama Masu akaguna huku akionekana kutafakari kwa kina.

# 11

Simu ya Masu iliita wakati tu alipomaliza mazungumzo na mama yake. Ilikuwa namba ngeni. Akaipokea na kutega simu sikioni.

'Hallow' akazungumza.

'Masu jamani, wamemweka ndani Bakari. Wanadhani yeye Ni wewe!' sauti ya Mwamvita ilijaa kitetemeshi.

'Taratibu Basi mpenzi, nieleze taratibu Malkia, Bakari kazua Nini Tena huko jamani. Na Mimi nikidhani muda huu utakuwa Dar?'

'Nilikuwa natoroka asubuhi na Bakari alinibebea bag la nguo kwenye mkokoteni. Sikutaka nionekane nasafiri, ili kupoteza nyayo. Sijui baba alijuaje, alikuja na polisi wakamkamata Bakari wakimdhania ndio mhusika wa mimba yangu na alijaribu kunitorosha. Hivi navyoongea, Yupo kituo Cha polisi ….. nimekwama mpenzi.'

Habari hiyo haikuwa njema. Ilivuruga mipango kabisa, na mbaya zaidi ilimweka Masu kwenye hatari ya jela. Adhabu ya kutia mimba mwanafunzi Ilikuwa sawa na adhabu ya ubakaji. Alihitaji kutuliza akili yake ili kujua Nini angefanya kujinasua. Lakini, Hilo halikuwa changamoto pekee, msela wake Bakari alikuwa ndani akisotea starehe yake aliyofanya kipindi hicho, akiwa Hana hatia! Alitakiwa kumtoa ndani kwa namna yoyote ile.

'Ok, nisikilize Malkia. Wewe Tulia, na jaribu kuangalia Nani anakuchunga na kufuatilia nyendo zako. Kwa Sasa, ninalazimika kuamini kwamba Kuna mtu kawekwa na baba mkwe ili kuchunguza nyendo zako. Hivyo ndivyo walivyofanikisha kumkamata Bakari. Hii namba Ni ya Nani?'

'Ni ya rafiki yangu Radhia.'

'Namba yako vipi?'

'Baba kaninyang'anya!'

'Anhaa, Unadhani Radhia anaweza kutunza Siri akitakiwa kufanya hivyo?'

'Kwa Kweli Sina hakika, Ni mtu wa maneno mengi!'

'Basi usimjulishe Kama unawasiliana na Mimi. Tumia namna nyingine kuwasiliana nami.'

'Kwa Sasa anajua mpenzi. Nilimweleza nataka kuwasiliana nawe!'

'Anhaa! Ok, mwambie asimweleze mtu kuwa tumewasiliana. Mimi nitaingia huko muda wowote, na tutayamaliza Haya. Mpango wetu tutaukamilisha Kama tulivyopanga. Kama kabla sijakufikia watakuwa wanajaribu kulazimisha ndoa na Babu Kisiki, jitahidi ukaripoti kwa sheha au jaribu hata kutoroka lakini usikubali wakuozeshe tafadhali. Nakuja kukuchukua Malkia'

'Asante mpenzi, nakutegemea! naa.. Masu!'

'Naam Malkia'

'I love you so much!'

'I love you as much!

***

Alitaka alale, lakini kwa habari hiyo, usiku usingelalika. Hakuwa tayari kupoteza hata sekunde, wakati mpenzi wake Mwamvita, alikuwa kwenye hatari ya kuozeshwa. Asingeruhusu Hilo litokee kwa maana, Kama lingetokea, jamii isingemwelewa Kama angefanya juhudi za kumchukua kutoka kwa babu Kisiki. Jamii ingemhukumu kwa kosa baya kabisa la kuchukua mke wa mtu. Kosa ambalo jamii isingesita kumhukumu bila kupepesa macho.

Masu akawaeleza wazazi kuwa angeondoka usiku huo. Kwa Nini? Waliuliza. Kulikuwa na dharura kazini. Akadanganya.

Alisota barabarani kusubiri gari ambalo lingekuwa linaenda mjini Morogoro. Masaa mawili alikuwa Kakaa kwenye upenu wa duka la nguo la mama yake. Pamoja naye, alikuwepo Kaka yake Miganda na vijana wengine kadhaa Rika lao wakisogoa, wakati akisubiri gari, na ndugu zake hao wakipoteza muda, siku ipite. Ajira Ilikuwa changamoto. Hicho ndio kitu kilichomchosha akaamua kwenda Dar Mara ya kwanza. Hakuona maana ya kuamka, ukae upenuni ukipiga soga, ulitazame jua likichomoza na ulishuhudie likizama ukiwa hujaingiza shilingi. Na shida ya kijijini, ukishalima, huna Cha kufanya Bali kusubiri muda wa palizi, kuweka mbolea, unasubiri Tena muda wa kuvuna. Muda mwingi unamkuta kijana Hana kazi. Matokeo yake wengi

walitokea kuwa walevi wa pombe, wakinywa mataputapu. Kama hiyo haikutosha walikuwa na muda mwingi wa kujaribu aina nyingine za ulevi, bangi, mirungi, ugoro na gongo. Hayo yote kwa Masu hayakuwa na maana. Hakutaka hata kujaribu. Alikwisha ona madhara yake, kwa Nini ajaribu sumu kwa kuonja? Vijana walizeeka kuliko baba zao, hawakuwa na nguvu za kuanzisha familia. Wizi mdogo mdogo ulishamiri. Wanakijiji hawakuhofia mwewe au vicheche dhidi ya kuku wao, waliwahofia vijana wao walevi. Wezi wa kuku.

Lorry la mageyo trans lilifika baada ya masaa mawili. Masu hakujali hadhi yake safari hii, alidandia gari Hilo na safari ya mjini ikaanza. Waliingia mjini Morogoro usiku wa saa tatu. Masu alitafuta Nyumba ya kulala wageni kupata' huduma ya bafu, alipokwisha kuoga, akaingia stendi, akabahatika kupata gari la mtu binafsi safari ya jijini ikaanza. Hakujali m-banano uliokuwemo ndani ya gari Hilo dogo aina ya probox, Wala hakuwa na namna ya kuikwepa harufu nzito, mbaya, iliyotokea kwenye moja ya vinywa vya wasafiri wenzie, isipokuwa kumlazimisha mtu huyo kunyamaza, maana Jamaa alijua kila soga za jijini, siasa, uchumi, mastaa wakubwa duniani na nchini. Ajabu hakujishitukia kwamba hakuna aliyempa makini yake, na kuwa kila mtu alionekana kukwepesha sura yake mbali naye.

'Oya broo, hebu tupumzishe Kidogo. Hili gari Ni dogo mno kwa kila mtu kuzungumza wakati kila mtu anajua

alichokula jioni hii. Wengine tumetoka mbali, tunahitaji utulivu wa kutosha kupumzisha akili na miili yetu.' Masu alimfikishia ujumbe.

'Unataka kusemaje….' yule bwana alitaka kuanzisha zogo. Lakini hakufanikiwa,abiria wote waliunga mkono hoja ya Masu. Jamaa akatulia Kama kanyeshewa mvua ya mawe!

Waliingia jijini Mwendo wa saa Saba usiku. Masu akaelekea feri. Akatafuta boti za kukodi, akapata moja na safari ya Zanzibar ikawiva.

***

'Oyi M'bara!' Yusuf alipokea simu ya Masu. Alikuwa Yupo kwenye club moja ya usiku, akiwa kawekwa Kati na watoto wa kike, mmoja wa kiitaliano na mmoja wa kibongo. Walikuwa wanatumia vilevi vya gharama, maana Yusuf hakuwa mchoyo kwa jinsia ke, hasa akiwa na pesa.

'Nahitaji kampani yako kwenye misheni fulani muhimu. Uko wapi kwanza.?' Masu aliuliza.

'Nilipo Mimi we M'bara huwezi kutia miguu. Swali ni, lazima nihusike na hiyo misheni yako?' Yusuf aliongea kwa kigugumizi chake kilichokolezwa na kilevi Basi ikawa Kama burudani kwa wale warembo wake.

'Ni muhimu sana.' Masu akajibu.

'Swali kwako Sasa, uko wapi wewe, ndiyo la kujibiwa na siyo nilipo Mimi?' Yusuf alitamka kwa mbwembwe

akilenga kuwakoga warembo wake aonekane Ni mtu mwenye maamuzi.

'Njoo forodhani!'

'Nakuja, jas giv mi e miniti!' Yusuf akachomekea kiingereza chake. Ingawa walikula kozi ya lugha zile mbili muhimu, Yusuf alikuwa na kauzito Kiasi kwenye kushika. Lakini haikuwa sawa na bure, alijua Cha kuweza kusikia na kusikika kwa kiwango kikubwa tu.

Walipokutana, Masu alimweleza msala uliokuwa mbele yao. Akamtaka Yusuf ampe Wazo Nini Cha kufanya. Labda kwa sababu ya ulevi, Yusuf akapendekeza wavamie kituo Cha polisi wakamuokoe rafiki yao, halafu wakodi boti imkimbize Mwamvita mafichoni, Dar.

'Unataka wanitoe busha Nini? Mbona mpango wako Ni Kama nguvu za Giza?. Hivi wewe unajua Hilo Ni kosa kubwa Kiasi gani? Uvamie kituo Cha polisi? SI sawa na ugaidi huo? Halafu kuwa siriazi Mara moja moja Yusuf.!' Masu akawaka. Kwa Yusuf, alikuwa na hamu kubwa ya kuweka mafunzo aliyopata kwa master Hye kwenye uwanja mapambano.

'Haya Sasa wewe sema Una mpango upi, haya, haraka, nakusikiliza!' Yusuf akakoroma.

'Nataka tumtie kashkash sheikh Abuubakr, iwe njia ya kumnasua mwanetu Beka, na kuondoka na Mwamvita!'

'Huna nidhamu wewe, wabara hamnaga Miiko kwenye Mila zenu, nini?. Unataka kumfanya Nini baba

mkwe wako?' Yusuf akuliza kwa dhihaka akitokwa na kicheko Cha nguvu.

'Una ujinga mwingi Sana Yusuf, maana hukomi kutoa pumba wewe mtu. Hebu nisikilize kwa makini. Tunahitaji cash, kitu kama em moja hivi. Tukishaipata hiyo, tutaenda nayo kwa sheikh Abuubakr. Tunamwekea hizo fedha zote mezani. Tunampa ilani. 'Kesho mzee, tunatarajia kusikia Beka ametoka ndani. Hiyo hapo milioni moja. Ifikapo saa kumi jioni, tunataka tusikie Bakari ameachiwa huru. Kwa Nini tunataka aachiwe? Kwa sababu, siye muhusika wa mimba ya binti yako.' unaliona vipi Hilo Wazo Yusuf?' Masu akamsaili rafiki yake Yusuf.

'Naona ukosefu mkubwa wa nidhamu kwa baba mkwe wako. Huwezi kumfanyia hivyo. Hata hivyo, Nakubaliana na mpango wako. Ila Swali la msingi Ni, tunaipata wapi hiyo million ya kumpa mkweo, M'bara?'

'Kuna yule mjinga mmoja amekuwa anatapeli fedha wafanyakazi wa serikali. Anajifanya anawakopesha halafu anachukua kadi zao za kutolea hela. Unampata?'

'Wapo wengi siku hizi.'

'Yeah, ila Kuna mmoja aliyesababishia kifo cha mzee Konokwe, alimpiga nusu ya mafao yake, mzee akapata stroke kwa mshituko, maana wanasema mzee yule alikuwa na mpango wa kufungua kampuni ya usafirishaji abiria akistaafu. Kumbe Jamaa walikuwa washategea,zilipotoka TU, wakatoka pasu kwa pasu. Mzee hakuamini, wakamkuta anatoka udenda'

'What? Hivyo ndivyo ilivyokuwa?'

'Eee!'

'Unajua hii mifumo ya kulipa pensheni wazee Ni shida kwa Kweli. Mtu keshasota miaka yote ya ujana na Hadi uzee wake akitegemea mshahara kiduchu, wakati Hana uwezo wa kusimamia mipango mipya anakutana na fedha ambazo hakuwahi kushika, lazima awehuke TU. Wengi hufa kwa sababu ya pesa hizo.'

'Ndiyo, kwa hiyo yule mjinga anazo hela za kutufanikishia huu mchongo. Tumvamie usiku huu huu, ili Kesho tumtoe mwanetu.'

'Haina noma, ila ninapendekeza maboresho namna ya kumweka sawa sheikh Abuubakr!'

'Enhee!'

'Hakuna haja ya kumvamia na kumpa hizo fedha. Yule ndo keshakuwa baba mkwe wako, lazima uoneshe heshima kwake. Njia Bora Ni kumtumia hizo fedha zikiwa na ujumbe wetu. Ujumbe wetu ndio unapaswa kuwa na sharti la ukomo. Nina uhakika haitafika saa sita za mchana tutapata habari mwana katoka.'

'Ah kudadeki wallah! Skuli Ni skuli tu. Leo hii siamini kabisa Yusuf wewe unaweza kuwa na mipango makini namna hii. Bonge la idea mtu wangu. Tusilaze damu Sasa. Mida ya wanga hii, tuingie kazini kabla hakujakuchwa!'

'Unalo wazo lolote juu ya ramani ya kuingilia nyumbani kwa huyo mjinga? Kama Ana walinzi? Au

anamiliki Cha Moto? Wanaishi watu wangapi hapo nyumbani kwake?' Yusuf akahoji.

'Hayo ndio Mambo ya msingi Sasa. Nimekuwa naliwazia suala Hilo safari yangu yote. Kuna njia ya kurahisisha misheni yetu.'

## 12

'Nipo makini bro, nakusikiliza,leta hizo Intel (taarifa)!'

'Iko hivi, Jamaa Ana walinzi wawili wenye mafunzo ya Mgambo. Bastola atakuwa nayo, lakini si kisheria. SI unajua hio biashara yake sio halali kwa sababu Hana vibali ingawa nimesikia Yupo kwenye ufuatiliaji wa kuhalalisha. Nyumbani Yuko na mke na watoto wa kike watatu, mmoja akiwa Yaya. Jengo lake Ni la kisasa, ameweka CCTV camera kila Kona, hivyo tunahitaji kwenda kininja. Tutaficha sura zetu, na tukishamaliza misheni tunaondoka na footage za CCTV. Nimekadiria kwamba, misheni yetu itatuchukua dakika kumi na tano Hadi ishirini hivi kukamilika.'

'Walinzi tutadili nao vipi?'

'Swali la msingi. Kwanza, hatuna mpango wa kuchukua uhai wa mtu. Kwa hiyo, tutawazimisha TU kwa muda wakati tukifanya shughuli yetu. Tukishaingia ndani tunawalaza usingizi wa nusu kaputi familia nzima isipokuwa huyo mjinga. Huyo mjinga akishatupatia fedha na yeye tunamzimisha kwa pigo tunasepa zetu baada ya kuondoka na footage.'

'Sawa. Ila huyo tapeli kwa Nini tusimvunje wallau kidole?' Yusuf akahoji akiweka sura ya kauzu.

'Hahaha, Kama unaona Hilo litakupa faraja, we mvunje tu, yeye keshavunja wangapi? Vunja mbaba!'

Baada ya kukubaliana na kuweka mipango yao sawa, Masu na Yusuf walitinga mavazi kwa ajili ya kazi. Damu zao zilichemka kwa hamu ya kufanya aksheni. Hawakuwa na bunduki, na waliamini wangeweza kutumia za wenyeji wao Kama ingelazimu.

Nyumba aliyoishi Nzinyangwa, mkopeshaji maarufu wa fedha za riba kubwa, kinyume Cha sheria, Ilikuwa imezungushiwa ukuta mrefu wenye nyaya za umeme juu yake. Namna pekee ya kuingia ilikuwa kwa kupitia getini. Ukiwa usiku wa saa Tisa, walihitaji kutumia akili Sana kuzama ndani ya jengo Hilo lenye ulinzi mkali.

Ndio maana Walivaa magwanda ya polisi.

Kwa muda, Masu alikuwa keshafanya upelelezi wake na kugundua Nzinyangwa alivyoshirikisha baadhi ya watumishi wa jeshi la polisi kwenye utapeli wake, akiwatumia kuwaweka ndani wadeni wake walioshindwa kulipa riba zake, ili kushinikiza familia zao kuchangishana kulipa hizo fedha. Utaratibu wao wa kufuata malipo yao kwa Nzinyangwa wakiwa doria usiku aliufahamu pia.

Walipofika getini, walibonyeza switch ya kengele. Mlinzi aliyekuwepo Zamu getini akachungulia kwenye dirisha dogo la kioo. Akaona sura ya afande. Afande Masu akaonesha kitambulisho chake fasta na kukirejesha mfukoni haraka.

'Tunahitaji kuonana na Nzinyangwa. Fungua geti.' akatamka kwa sauti iliyojaa mamlaka. Kuna namna Askari wanaamrisha heshima kwa Walinzi. Nadhani kwa vile Walinzi wengi wana ndoto za kuwa maaskari wakikuwa wakubwa□!

Haikuwa Mara ya kwanza kwa mlinzi kupata' ugeni aina hiyo. Kwa kazi ya bosi wake, hii ilitokea Mara kwa Mara, na kawaida polisi hao walishikishwa fungu la fedha wakasepa zao. Leo, mlinzi hakuwa na taarifa ya ujio wao na hakuachiwa fungu kuwapa wanapokuja. Akalazimika kufungua geti. Hilo likawa kosa kubwa kwa upande wa mlinzi.

Jamaa walivyoingia tu! Mlinzi akajikuta anapaa juu. Alipotua chini, tayari alikuwa nusu kaputi. Master Park Hye angetabasamu Kama angeona jinsi vijana wake walivyokuwa wameiva!

Kishindo alichotua nacho mlinzi huyo kikamwamsha mwenzake aliyekuwa amejilaza kwenye mkeka kwenye kile chumba Cha Walinzi. Akakurupuka kwa wenge, akamuona Masu akinyata kuelekea kwenye mlango wa jumba la Nzinyangwa. Akatoka kwa kunyata vile vile. Alipokaa kwenye nafasi ya kumudu shambulizi, akarusha rungu lake kwa mkono wake wa kushoto, isingekuwa ile hisia ya sita aliyofunzwa na master Park Hye, Masu angekuwa marehemu. Alichezwa machale akaikwepa Kidogo, akasikia mvumo wake ukipita sikioni mwake kwa Kasi. Mlinzi yule Sasa alikuwa

anamfuata kwa Kasi ya ajabu. Huyo, akairusha ngumi yake iliyokuwa na ujazo wa kilo kadhaa, lakini Masu aliiona, akaidaka ngumi ile na kumvuta mlinzi upande wake, mlinzi akavutika na kukosa balansi, hapo hapo Masu akanyanyua guu lake la kushoto na kumchota mlinzi tumboni, mlinzi akapaa juu, aliporudi chini, Masu akampa bapa la kono lake maeneo fulani nyuma ya sikio, mlinzi akalala usingizi.

Mlinzi wa tatu alikuwa amelala fofofo kwenye godoro kwenye Nyumba ya walinzi, walibaini baadaye kuwa huyu hakuwa mlinzi Bali raia TU asiye na ujuzi wowote wa ulinzi. Yusuf alimnyatia raia yule, akampa pigo la kininja akaendelea kulala unono.

Walinzi walikuwa na funguo nyingi Sana. Masu na Yusuf wakahisi Kuna funguo ya kuingilia ndani ya jengo la Nzinyangwa. Wakazijaribisha haukuwepo wa kufungua mlango wa mbele. Wakati Yusuf anaendelea na Hilo zoezi, Masu alikumbuka kwamba SI Kawaida wabongo kutumia mlango huo. Hata Kuna baadhi ya familia funguo wa mlango wa mbele haujulikani ulipo kabisa kwa jinsi usivyotumika, alizunguka kwa nyuma. Mlango wa nyuma kuingilia jikoni ulikuwa umerudishiwa TU. Akafanya kuusukuma kwa tahadhari. Hapo jikoni akamuona binti wa kazi, alikuwa kalala chini kwenye mkeka, kajifunika kanga. Mbu wakimgeuza pipa la pombe, walikuwa wanamnyonya damu binti wa watu maana hakuwa na chandarua Cha

kumlinda dhidi ya wadudu hao hatari wanaoongoza kwa kuua watu kusini mwa jangwa la Sahara.

Masu akabonyeza simu yake na kuandika maandishi 'back door'. Yusuf akahisi mtetemo wa saa yake mkononi akaitazama na kusoma maneno Yale. Back door. Akazunguka kule.

Masu alimfuata yule binti pale chini, akamfunika mdomo huku akimwamsha.

'Kimya!' akanong'ona. Dada wa kazi mkojo ukamtoka. Alikuwa anatetemeka vibaya Sana.

'Chumba Cha bosi Ni kipi?'

Binti akaonesha kwa kidole Cha shahada.

'Sina shida na wewe lakini ukileta ujuaji, nakulipua. Kaa kimya.' Masu akamtishia binti wakati akimfunga kwa kanga yake mwenyewe mikononi kwa nyuma pamoja na miguu, akamtia tambara mdomoni. Akafungua mlango walimolala watoto wa Nzinyangwa, akapuliza dawa ya usingizi na kufunga.

Wakati akienda kwa Mwendo wa kunyata, ili aingie chumba Cha Nzinyangwa, akashuhudia mlango ukivutwa kwa Kasi ya ajabu Sana. Hakutarajia hili.

'Chwaa!' Masu akachezea mjeledi, akawewesuka na kupiga magoti chini. Alipojaribu kujinyanyua, akakumbana na mdomo wa bastola. Nzinyangwa alikuwa na mwili mkubwa. Jitu. Ligoliati kabisa. Jamaa huyo, alipomuona Masu Ni mtu mwenye mwili mdogo, akajua atamuweza. Akamdharau. Akamshushia mjeledi wa pili mgongoni. Masu maumivu yakaupenya mwili

wake. Akayumba kushoto. Mjeledi wa tatu ulikuwa unamfuata, akaruka Kama ngedere kwa namna ambayo Nzinyangwa hakutarajia, akawa ameikamata koromeo yake mkono mmoja na mkono mwingine ukadaka bastola. Nzinyangwa akawa anapigania pumzi yake. Masu akamtandika na kitako Cha bastola na kumsukumia ukutani, haraka Sana akamtegua miguu, Nzinyangwa akanguka chini Kama zigo.

Masu akasikia sauti toka chumbani, mkewe Nzinyangwa alikuwa anaongea kwenye simu. Akamwacha Nzinyangwa aliyekuwa anagugumia kwa maumivu, akazama chumbani alipokuwa mkewe Nzinyangwa, Akamrukia mwanamke huyo na kuidaka simu, akaiweka sikioni.

'Sijakuelewa unasemaa..!' mtu wa upande wa pili wa simu alikuwa anahoji. Ilikuwa sauti ya kike.

Masu akampa simu yule mwanamke ikiwa loudspeaker, 'malizia mazungumzo yako' akatamka huku akimwonyesha bastola. Alijua inamaanisha Nini.

'Nimesema ile hela ya vikoba Ni Kesho!' mwanamke akatamka. Masu akatikisa kichwa kukubaliana na akili aliyotumia mwanamke huyo kupoteza lengo la awali la kupiga simu ile.

'Jamani, ndiyo unanipigia usiku huu mama Shani? Sisi ni majirani umeshindwa kungoja kukuche unambie?'

'Ee nawe, saa Tisa mwanamke bado umelala. Haya Basi endelea kulala!' akakata simu.

Yusuf alipoingia mlango wa uani, alikuta binti wa kazi kalazwa chini, akapita kwenye korido na mbele akamuona mtu akigalagala, akamsogelea kwa tahadhari. Alikuwa mtu wao. Akajua Masu keshamaliza kazi. Alijidanganya, Kumbe Nzinyangwa alikuwa kazuga TU, alinyanyuka haraka Sana, akamtwika Yusuf konde moja hatari, Yusuf akayumba na kugonga ukuta. Akapasuka Kidogo, damu zikavuja Kidogo lakini. Hali hiyo ikamtia hasira Yusuf, Nzinyangwa alikuwa anamfuata kwa pigo lingine, Yusuf akawa amemuona, kwa wepesi akageuka na kutupa teke lililompata Vema adui yangu kwenye mvungu wa kiuno chake, Nzinyangwa akatoa ukelele akizikumbatia Mali zake na kuketi chini. Maumivu makali yakasambaa kutoka hapo hadi tumboni mwake. Mara, Masu akatoka chumbani akiwa amemtanguliza mkewe Nzinyangwa mbele.

'Enhee!' Yusuf akauliza, akiwa mguu mmoja kaikanyaga shingo ngumu ya Nzinyangwa.

'Ukileta ubishi, nakumaliza' Yusuf akatamka akimkazia macho Nzinyangwa.

'Hawataki kueleza zilipo fedha. Nataka tuwaue pamoja na watoto wao. Tunaanza na watoto kwanza. Watu wana roho mbaya Sana Hawa. Umeona binti wa kazi anapolala? Na wanajiita matajiri.'

'Fedha ziko wapi?' ule mjeledi wa bwana Nzinyangwa Sasa ulikuwa mkononi mwa Masu. Aliunyanyua halafu akaushusha mgongoni kwa bwana Nzinyangwa kwa hasira za kulipiza.

Chwaa!

Nzinyangwa akatoa kelele za maumivu. Alikuwa Hana ujanja, bastola yake mwenyewe ilikuwa inatishia uhai wake.

'Mfunge mikono' Masu akamuamrisha Yusuf.

Yusuf akachomoa kamba kwenye gwanda lake. Akamfunga mikono Nzinyangwa. Masu akaushusha Tena mjeledi mgongoni kwa Nzinyangwa.

'Nawapa pesa, tafadhali msiue wanangu.' Nzinyangwa akawarai.

'Simama utuoneshe zilipo'. Yusuf alikuwa kamshika mkono binti mdogo wa Nzinyangwa.

Nzinyangwa akaongoza njia kwenda chumbani.

'Dah na unafaidi Sana we mjinga, Una mwanamke bomba Sana!' Yusuf alizungumza.

Mkewe Nzinyangwa akajua leo Ni leo alikuwa bubu ghafla akitetemeka kwa hofu.

Chumbani kwa Nzinyangwa kulikuwa kasiki. Kasiki la chuma. Akawaonesha funguo la kasiki hiyo. Masu akalifungua kasiki. Mlikuwa na fedha nyingi Sana.

'Zipo Kiasi gani jumla?!' Masu akauliza wakati huo akizipakua na kuzihifadhi kwenye mfuko waliokuja nao kwa kusudi Hilo.

'Mia mbili Nzinyangwa akatamka.

'Milioni Mia mbili! Tunachukua Mia tunakuachia Mia.' Masu akatamka.

'Tunakomba zote, mwachie hamsini tu' Yusuf akabwata. Wakazichukua zote, na halafu wakapunguza

hamsini. Walipomaliza zoezi Hilo. Wakawalaza kitandani, wakapuliza dawa ya usingizi wakatokomea zao na footage ya CCTV. Hawakuacha ushahidi. Master Park Hye aliwafunza vyema. Walikuwa wametumia dakika 25

***

Walipokwisha kuondoka nyumbani kwa Nzinyangwa, walipanda pikipiki la Yusuf waliokuwa wametumia awali Hadi alikoishi Yusuf. Alikuwa SI Yusuf yule, huyu aliishi kwenye Nyumba nzuri, Nyumba yenye kiwango, self contained. Wakahesabu zile fedha wakagawana pasu kwa pasu. Walikuwa mamilionea. Milioni sabini na tano za utajiri.

Wakakubaliana kutoa milioni tano kila mmoja kwa ajili ya kumpa kianzio msela wao. Beka. Walikuwa na uhakika anaachiwa mchana wa siku hiyo. Ilikuwa yapata saa kumi Sasa. Uchovu wa safari na aksheni iliyomtwika mijeledi miwili yenye ujazo, Masu alikuwa kachoka mbaya. Aliposema anajiegesha kwenye sofa, usingizi mzito ulimvaa akiwa ndani ya mavazi Yale ya misheni.

Alipoamka usingizini, ilikuwa saa nne za asubuhi. Akamkurupua Yusuf ambaye alikuwa anakoroma kwa sauti kubwa.

'Oya! Kushakucha mzee baba, amka tukamilishe misheni.'

Yusuf akaamka akionekana kuchoka. Pombe za usiku zilimpa hangover ya hatari.

Walioga Kisha wakaweka mpango wao mbashara.

Waliamka mamilionea. Wakashukuru kukutana na Steve Curl. Huu ulikuwa mwanzo mzuri, na bado walikuwa hawajaanza kazi ya Mzungu.

***

Sheikh Abuubakr, alikuwa dukani akichezea tasbih yake! Akaingia mtoto mdogo wa miaka takribani nane. Alimfahamu mtoto huyo.

'Wa jina huyoo, wamekuagiza Nini? Tambi?' Sheikh Abuubakr alimchangamkia Abuubakr mtoto.

'Kuna dada amenipa hi bahasha nikuletee.'

'Dada? Dada gani Abuu?'

'Mi simfahamu, ndio nimemuona leo! Na keshaondoka, alikuja na gari'

'Haya, asante swahiba!'

'Haya, Mie naenda'

'Mung'unya hizo ukienda' akampatia pipi tatu.

Sheikh Abuubakr akafungua bahasha na kutoa vilivyomo,

'Astaghfirullah!' sheikh Abuubakr akatamka huku akirudi nyuma kwa kihoro. Yalikuwa manoti ya shilingi elfu kumi. Jumla milioni moja.

Ndani ya bahasha hiyo pia kulikuwa na ujumbe.

'Sheikh Abuubakr,

Pesa hiyo Ni yako. Tunakutaka amani. Kijana unayekusudia kumfunga jela SI mhusika wa mimba ya binti yako. Kwa sadaka hiyo, tunakuomba umwachie huru. Yeye hajui lolote kuhusu suala Hilo. Ni ungwana TU Kama utaona vema kumuomba msamaha kwa kumweka ndani pasipo hatia. Mwanao ndiye anamfahamu mhusika wa mimba yake, hukuona busara kumuuliza Hilo? Tunakutaka uwiwe kutenda haki. Kama kufika saa Tisa atakuwa bado hajaachiwa, utakuwa umetangaza Vita na sisi. Ukiona vema kuripoti ujumbe wetu kwa polisi, Ni uamuzi wako. Tunatumaini busara itakuongoza vema.
Wapenda haki.'

Alipomaliza kusoma ujumbe huo, sheikh Abuubakr alikuwa anatetemeka mikono. Akafanya hima, akafunga duka na kuelekea polisi. Njiani akawa anawaza kuwashirikisha polisi kuhusu fedha na ujumbe ule. Akawa yuasita Sana kufanya hivyo. Ingemsaidia Nini kuingia vitani na watu asowajua? Akaona heri kufuata Rai ya 'wapenda haki'. Hata bintiye pia alikuwa kamlaumu Sana kumweka ndani kijana yule. Lakini hasira Ilikuwa imempofusha asione Kama alikuwa anatenda kosa bila kujua.

'Naama Sheikh Abuubakr, karibu Sana sheikh.' Askari wa Zamu alimkaribisha mzee Abuubakr.

'Asante Sana afande, vipi, mwaendeleaje hapa?'

'Hapa Ni heri sheikh wangu, Munyazi Mungu atutendea heri TU, tuwazima wa afya sheikh!'

'Hilo la kheri Sana. Sasa bwana Askari, Mimi nimekuja hapa kwa ajili ya ile kesi ya Jana.!'

'Naam!, Yule mbakaji tupo naye, na kusema ukweli Ni mgumu Sana huyo kijana, hata baada ya mateso mengi, amegoma kukiri Ni mhusika wa ile mimba. Mgumu Sana sheikh'

'Oh!' sheikh Abuubakr akatoa sauti, akahisi Kama Kuna maumivu yaliupenya moyo wake.

'Tumemkosea Sana kijana wa watu Afande, nimekuja kubaini tulifanya makosa. Huyo kijana Kumbe Kazi yake kubebea TU watu mizigo yao. Sasa nilivyokuta binti yangu kachukua mizigo anatoroka, nikajua huyu yuamtorosha Kumbe yeye alikuwa TU kapewa kibarua Cha kubeba Asijue aa Wala be! Tumemkosea Sana huyo kijana.'

'La! Haula! Mimi nikasema kijana mgumu Kweli kukiri makosa, Kumbe alikuwa aonesha uadilifu?. La la la! Kwa Kweli Tumemkosea Sana.'

'Naam afande, hivyo mie naomba tumwachilie huru kijana huyu.'

'Hilo la kheri sheikh wangu, SI vema kuendelea kumweka hapa shughuli zake zikiendelea kulala. Ila hapo utachangia shilingi elfu hamsini TU, kufidia usumbufu uliojitokeza kwa jeshi la polisi'

'Hamna tabu, wacha tulimalize hili.' sheikh Abuubakr akatamka akijua wazi ile Ilikuwa hongo. Lakini yeye hakuona Hilo, alijua baadhi ya watumishi wa jeshi la polisi kwa hongo Ni chuma kwa sumaku, na hapa

alikuwa anakimbizana na muda! Wapenda haki walimpa muda mahsusi kutekeleza Rai yao.

## 13

Million 75 kwa kila mmoja wao, Ilikuwa Ni hela kubwa. Nzinyangwa alijua ingekuwa rahisi kuwakamata wezi wake. Alikadiria kwamba, wezi wake wangeonesha umwamba, kutumia isivyo Kawaida. Anasa kwa wingi. Akawapanga vijana wake kuzungukia maeneo ya starehe kuangalia watu ambao wangekuwa na matumizi yasiyo ya Kawaida. Hiyo ingekuwa Kweli kama Masu na Yusuf wangekuwa waswahili, kwani waswahili huamini maskini akipata sijui nini hulia mbwata. Alipoteza muda.

Masu na Yusuf walikuwa na Wazo tofauti. Walikubaliana kuhifadhi zile fedha na kutulizana kwanza. Waliwaza kuwa kutumia pesa isivyo Kawaida yao, ingevutia nzi Kama inavyokuwa kwa mizoga. Kila mmoja akaichimbia alikoona Salama. Hawakuzihifadhi benki. Kama kazi ya Mzungu ingeonekana namna gani, walikusudia kuondoka Zanzibar na kuanzisha biashara au kuwekeza fedha zao kwenye makampuni makubwa kwa mtindo wa kununua hisa au hatifungani. Nzinyangwa asingewapata.

Mara baada ya kuachiliwa huru, Bakari aliona Zanzibar kunamwekea usiku. Rafikize walipompatia Kiasi kile Cha fedha, aliondoka Zanzibar na kurejea kwao Iringa. Fedha ile akaitumia kununua mashamba yenye miti izalishayo mbao, Cyprus na pines. Kiasi

Kidogo akaanzisha biashara ya duka la jumla. Mungu akaibariki kazi yake mpya. Akafanikiwa sana. Miaka mitano mbeleni, Bakari, ambaye Sasa alijulikana kwa jina lake halisi Paulo, alikadiria kwamba angepata mamilioni ya fedha kwa kuchana na kuuza mbao kwa ile miti yake.

***

Siku moja baada ya kuachiwa kwa Bakari, Masu na Yusuf waliomba kikao na sheikh Abuubakr. Sheikh Abuubakr akawakaribisha nyumbani, wakawa wameketi wanakunywa ghahawa. Masu alikusudia kumweleza sheikh Abuubakr, kuwa kusudio la safari yao hapo Nyumbani, Ilikuwa kuutaka mkono wa bintiye Mwamvita kwenye ndoa tukufu.

'Sheikh, sisi Ni vijana wako, tupo hapa kwa sababu tunahitaji kuzungumza nawe.. Mimi naitwa Yusuf, na huyu mwenzangu anaitwa….'

'Naitwa Masuke Masuke mzee wangu!' Masu alidakia kabla Yusuf hajamalizia kumtambulisha. Lafudhi yake ya bara ikimtambulisha vilivyo kuwa yeye Ni mtu kutoka bara. Akaunyoosha mkono wake amsalimie sheikh Abuubakr. Ah wapi!? Sheikh Abuubakr aliposikia jina Hilo, kumbu kumbu yake ikamtendea haki. Ikamweleza kuwa mkewe mama Mwamvita akikwishamwelezea hofu yake kuwa Masu alihusika na mimba ya binti yao. Haikuwa kitambo, Ilikuwa usiku wa

Jana baada ya kumweleza habari za Bakari. Aliyakumbuka vema Maelezo ya mkewe.

'Mume wangu, Kama ulosema Ni sahihi, Basi mie namhisi kijana mmoja, rafikiye huyo Bakari, kuwa ndiye mhusika wa hiyo mimba. Aitwa Masu. Nasema hivyo kwa sababu, huyo kijana alikuwa na mazoea ya kuniita mamkwe, na si mara moja alipomwita Mwamvita Malkia nikaliona huba machoni mwa binti yetu kwa kijana huyo. Sikutilia maanani kwa sababu kijana mwenyewe alikuwa mwadilifu sana, ila alipotoweka ghafla, Hakuna alojua kendaapi, zikavuma habari alitekwa na wasiojulikana! Hivi unapoongea habari za Bakari, ndio umenifanya niliwaze hili.'

Hasira zikamvaa sheikh Abuubakr, akaona kijana huyo alikuwa analeta dhihaka. Akanyanyua bakora yake amtandike nayo kijana huyo. Mara akaisikia sauti ya mkewe.

'Sheikh Abuubakr mume wangu.' sheikh Abuubakr akaishusha chini bakora yake.

Busara yake ikamshawishi kutuliza hasira na kuwasikiliza hao wageni wake.

'Enhee, mwasemaje vijana?' akauliza, macho kayatua barabara usoni mwake Masu.

Huenda akawa SI huyu, maana Masuke aliyenieleza mke wangu alikuwa mlalahoi, mla kwa jasho litokanalo na kusukuma guta na mikokoteni, akajiwazia Sheikh Abuubakr. Alimtazama kijana huyo, akajaribu kutafuta hiyo hadhi ya msukuma mikokoteni asiione. Huyu.., ah!

huyu alionekana kuwa mtumishi wa serikali, kitengo nyeti chenye kucheua marupurupu na mshahara mnono bila shaka. Masuke alikuwa katinga suti Safi ya hudhurungi. Nywele zake nyeusi zilichanwa Vema na kungara kwa mafuta ghali ya nywele. Mguuni alitinga moka safi, Loh, hakuvaa soksi. *'Vijana wa siku hizi*!' akawaza Sheikh Abuubakr. *'Hawafanyi kitu kikamilike wasikitie doa, kapendeza lakini kaharibia hapo tu, mbona asivae soksi?'* akaendelea kujiuliza.

'Eeh, mzee tumekuja na kijizawadi Kidogo. Tunaomba ukipokee kabla hatujaeleza dhumuni la ujio wetu.' Yusuf akazungumza, Huku Masu akitoa bahasha na kumkabidhi mzee huyo. Sheikh akaipokea zawadi. Akachungulia ndani na kuona burungutu la fedha.

'Nyie vijana Ni Nani? Mnataka Nini? Hii maana yake Nini?' Sheikh akalipuka kwa hasira.

'Tumekuja kuomba radhi kwa usumbufu tulokusababishia. Tunajua Kuna namna tumekufanya uwe na hasira na hata kufikiria vibaya. Kama nilivyojitambulisha awali, Mimi naitwa Masuke. Mimi ndio mhusika wa mimba ya Mwamvita.' Masuke akajieleza. Safari hii akachezea bakora.

'Wapuuzi Sana nyie watoto, kwa hiyo mmeona mlete dhihaka hapa, sivyo?' Sheikh alikuwa kasimama Sasa. Amefura kwa hasira!

'Hapana mzee, Tumekuja kwa Nia njema TU. Tunatakutaka radhi na pia tunaomba ruhusa ya kumuoa binti yako Mwamvita.' Yusuf akaingilia Kati.

'Mmeona haitoshi kumtia mimba Mwanafunzi Sasa Unataka kunihonga Mimi nishiriki makosa yako? Jela ndiko kunakokufaa. Mjinga mmoja wewe?' sheikh Abuubakr alikuwa mbogo.

Mwamvita alikuwa chumbani kwake. Uzuri wa chumba chake, dirisha lake lilitazama hapo walipokaa Masu, Yusuf na wazazi wake, Chini ya mnazi. Alishuhudia harakati zile zilizokuwa zinaendelea. Masu alivyokula bakora, Mwamvita uvumilivu ukamshinda, Heri hizo bakora azipate yeye pia. Akatoka ndani akilia.

'Mimi ndiyo nastahili hizo bakora baba, Mimi ndio nikiyekufedhehesha. Sikumpa nafasi Masu kufanya maamuzi Sawa, Mimi ndio niliyemfuata kwake na kusababisha hii Hali. Kama Ni adhabu nastahili Mimi. La sivyo, nakuomba baba, tafadhali tusamehe. Yalikwisha tokea ya kutokea, tusamehe baba, tunahitaji baraka zako tuanze familia.'

'Sheikh Abuubakr mume wangu. Hebu punguza jaziba baba watoto. Wasikilize watoto. Wameonesha kujutia makosa yao, wape nafasi ya kujisahihisha tafadhali!' mama Mwamvita akaongea kwa hekima kubwa. Sheikh Abuubakr yakamwingia Hayo maneno. Mara nyingi, sauti ya mkewe Ilikuwa na athari kwenye moyo wake. Tangu alipomuoa, sauti yake Ilikuwa sauti iliyompa tumaini na kumpitisha kwenye changamoto. Aliiheshimu sauti hiyo. Akatuliza munkari. Akapumua Vema. Akapata kufikiri Vema bila ushawishi wa hasira.

'Hamna wazazi nyie?' lilikuwa swali la msingi.

Swali ambalo huenda vijana hao hawakulitarajia. Wakabaki wanatazamana.

'Kama lengo Ni kuleta barua ya posa, nyie hamjui taratibu?' akaongezea Tena Sheikh Abuubakr.

'Ah, mzee wangu Hilo litafuata hivi punde. Sisi tulitaka tu tuweke Mambo sawa kabla ya kuanza hatua rasmi za taratibu za kuoa. Tumekuja kwa lengo la kukutaka radhi.'

Sheikh Abuubakr akarudisha moyo wa imani.

'Mama Mwamvita mke wangu, hebu kawaandalie chakula wageni wetu.'

'Rabeka mume wangu, naenda Sasa hivi. Haya, amka twende mama!' mama Mwamvita akazungumza huku akimwashiria Mwamvita kuongozana naye. Nyuso zao ziling'ara kwa tabasamu. Mwamvita alifurahi mno!

'Enhee, Sasa naweza kuwasikiliza. Jitambulisheni Tena tufahamiane vizuri. Hivoo, umesema wewe wafanya kazi gani?' Sheikh akauliza. Alikuwa akitafakari habari kwamba, kijana huyo alotaka kumuoa bintiye Ni mbeba mizigo. Akatafakari pia juu ya yule mzee aliyeonesha Nia ya kutaka kumuoa binti yake, aluwatani Kisiki.

Mzee Kisiki alijulikana Sana hapo mtaani. Mwanajeshi mstaafu aliyetukuka kwa sifa kibao, ikiwamo ile ya kuongoza kikosi kilichofanikisha kurejesha amani visiwani Comoro. Mzee huyu, alikuwa na jumla ya wake nane, hivyo Ni kusema Mwamvita angefikisha namba Tisa. Kilichomfanya mzee Kisiki

amudu kuwa na wake wengi hivyo Ni uchumi wake mzuri. Alikuwa Ni miongoni mwa watu wenye hisa nyingi kwenye makampuni makubwa anuai hapo Zanzibar na kule bara. Mahotel ya nyota tatu Hadi tano, mzee alikuwa na mkono wake ndani. Alitumia Vema nafasi yake ya ukubwa jeshini wakati wake, kuwekeza.

Sheikh Abuubakr alitafakari Sana. Moyo wa bintiye ulikuwa umemwangukia mhuni, msukuma guta.. angeishi maisha hovyo Sana ya kimaskini kwa kuambatana na kijana huyo. Wakeze Kisiki walikula maisha, wengi aliwaoa TU ili kuwanusuru. Alifanya Kama kuoa Ni sadaka kuwasaidia wanawake waliokimbiwa na kuachiwa mimba, ama kutelekezwa na watoto wao. Hao ndio wakeze Kisiki. Aliwachukua hao, akawapatia maisha, kila mmoja akawa na uhakika wa kuingiza kipato. Akawafungulia miradi wasimamie. Hata ikawa kila mkewe, aliweza kula na kulala pazuri, kusomesha watoto kwenye skuli za kufunza kwa kiingereza, na wote waliendesha magari kwa ufahari. Huyo ndiyo mtu alotaka achukue dhamana ya bintiye. SI mhuni mmoja kutoka bara!

Sasa akabaki yuajiuliza, namna gani bintiye alichagua mtu lofa, avujaye jasho kupata' mkate usotosha hata kusaza? Sheikh Abuubakr akajikuta kwenye mtihani mgumu. Akatega sikio amsikilize kijana huyo, huenda akabaini hicho kilichomfanya bintiye. SI Ni Kweli kwamba wapo maskini wa Mali lakini wakawa matajiri wa busara? Alitafakari..

Masuke moyo ukamlipuka kwa furaha, akaweka tabasamu usoni kwake na kuanza kujieleza, tayari alikwisha hisi ushindi Unamnyemelea! Akajikohoza Kidogo na kulegeza Kidogo tai yake, akaweka pozi la ushindi.

'Ah, mzee wangu Mimi naitwa Masuke Masuke, Ni mzaliwa wa kijijini Malonje mkoani Morogoro. Kwa Zanzibar, huu Ni mwaka wa pili Sasa tangu nilipokuja Huku, SI haba, mwenyezi Mungu aliniangazia Nuru zake tangu nakanyaga hapa, akanibariki kupata' kipato changu Kidogo lakini halali, kwa kujituma kutumia mikono na nguvu zangu. Nimekuwa nafanya kazi ya kubeba mizigo lakini kwa Sasa natarajia kuanza kazi yangu mpya mwezi ujao, kwenye Hotel moja ya Mzungu hapa hapa kisiwani. Itakuwa kazi yenye maslahi mazuri na nakuahidi binti yako atakuwa kwenye mikono Salama, inshallah, kwa uwezo wa Mungu. Huyu mwenzangu Ni rafiki yangu ambaye tumekuwa tukifanya naye kazi pamoja'. Masuke alijieleza kwa ufahari.

Mzee Abuubakr alimtazama kijana huyo akakosa tumaini. Suti hii ya gharama, Kumbe kapewa na Mzungu kwa ajili ya kazi ya uhudumu hotelini. Eti maslahi mazuri, kwa kazi gani? Kwa mtu alozoea kupewa Mia tano miambili elfu moja, kazi nzuri itakuwa ya shilingi ngapi? Laki moja kwa mwezi? Sheikh Abuubakr akamdharau Sana kijana. Hata hivyo hakutaka kuonesha

Hali hiyo. Wakaendelea kupiga soga, chakula kikaletwa wakala na hatimaye wakaagana.

'Kumbuka kunisalimia wazazi wenzangu huko. Bila shaka tunawatarajia kwa ajili ya kukamilisha Taratibu hizi. Muhimu wakinipa taarifa mapema juu ya ujio wao.' Sheikh Abuubakr akachombeza.

Masu na Yusuf wakaondoka wakiwa na nyuso za furaha. Mwamvita furaha yake ndio kabisa, Ilikuwa haisimuliki.

***

'Naam Sheikh, …… nakupata vizuri Sheikh……. Hewalaa sheikh wangu. Sasa, Mimi Nina mpango maalumu wa kutatua Hilo tatizo, Wala lisikusumbue Hilo, sisi watu wazima bwana, watoto hawawezi kutuzingua kabisa. Unaonaje tuonane baada ya swala ya jioni nikushirikishe mpango huo?' Ilikuwa sauti ya mzee Kisiki!

'Naam, nitafanya hivyo!'

Jioni ya siku hiyo iliwakutanisha mzee Kisiki na sheikh Abuubakr. Wakazungumza mengi. Alipotoka hapo, Sheikh Abuubakr alikuwa na jibu dhidi ya suala la bintiye. Katu hangeridhia fukara msukuma mikokoteni ayaharibu maisha ya bintiye.

# 14

Kulikuwa na Hali ya furaha tele nyumbani kwa Sheikh Abuubakr. Furaha iliyochagizwa na wazee hao kuridhia uhusiano wa Mwamvita na M'bara, Masu. Mazungumzo yakanogea zaidi kwa kutangaziana msamaha baina yao. Lakini furaha ikazidi simu ilipopigwa kutoka Oman, shangaziye Mwamvita aishiye huko alikuwa anawasalimia. Mwamvita akamshirikisha furaha yao.

'Oh hongera Sana shangazi yangu, natamani ningelikuwa hapo tufurahi pamoja. Hata hivyo, kwa furaha niliyonayo, nitafanya kitu kwa ajili yako' shangazi Amina akamweleza Mwamvita.

'Kitu gani shangazi?'

'Siri yangu!'

'Nambie buana, shangazi!' Mwamvita akaongea kwa deko.

'Haya, kwa vile umesisitiza, unaonaje nikutumie nauli uje huku nikufanyie shopping kabla ya harusi yako? Hivi itakuwa lini hiyo harusi?'

'Bado haijapangwa shangazi, ila nitaongea na wazazi kwanza Kama watanikubalia nitakuja Mara moja!'

'Haya shangazi, Mie nakutakia kila la Heri!' shangazi Amina akatamka.

'Shukrani Sana shangazi. Nitakuja inshallah!' Wakafurahi Sana.

Kesho ya siku hiyo, Mwamvita akaitika wito wa babaake.

'Shangazi yako katuma nauli, itakubidi uende forodhani pale zilipo ofisi za 'money gram', ukazichukue. Neno la Siri Ni 'vita' kifupisho Cha jina lako. '

'Shangazi kweli amefurahi Sana. Mara hii keshatuma!'

'Naam, Hakuna kitu anachopenda shangaziyo Kama anavyokupenda wewe, ulipokuwa mdogo, Basi alikuwa muda wote yuakuangalia wee, muda wote kukutekenya mashavu yako, alikuwa anakuita Malaika. Nahisi kumbukumbu zile, Sasa zinamtamanisha akuone ulivyokuwa mdada, Tena anaposikia Una mimba, ah anajua utamletea katoto akatekenye mashavu yake katabasamu na kucheka Kama ilivyokuwaga zamani za utoto wako.' Sheikh Abuubakr alizungumza na kuamsha kicheko. Wakacheka sana, Mwamvita akifurahia hiyo kumbukumbu aliyoambiwa. Akafanya hima, akachukua usafiri wa boda boda kuwahi forodhani, kufuata hizo fedha za nauli Kama zilivyotumwa na Shangazi yake.

Alipofika forodhani kwenye afisi za money gram, aliulizwa neno la Siri, akawaeleza, akakabidhiwa riali za Oman Mia mbili hamsini, sawa na pesa za Tanzania shilingi million moja na nusu. Akaomba kubadilishiwa, na uzuri hapo hapo jirani na afisi hiyo kulikuwa na duka la banyani mmoja la kubadilisha fedha za kigeni, wenyewe' huita 'bureau de change'. Akafurahi mno. Akarejea nyumbani akiwa mwingi wa tabasamu.

Mwamvita hakutaka kumtia wasiwasi mumewe mtarajiwa. Akadhamiria kuifanya safari ya Oman Siri. Alikusudia kwenda huko atumie siku mbili tatu na zikiwa nyingi tano, arejee mapema. Hivyo kwa siku mbili alizokuwa anapanga mipango ya safari alikuwa anawasiliana vizuri na Masu. Hata siku aliyokuwa uwanja wa ndege Kisauni, alimpigia simu Masu na kumweleza alikuwa anasafiri Kidogo, na huko alikokuwa anaenda huenda asingepatikana kwenye simu. Masu alijawa na wasiwasi. Wapi alikuwa anaenda, kwa Nini asipatikane kwenye simu?, yeye akadai maeneo Yale mtandao ulikuwa tabu sana. Wapi? Masu akasisitiza, Mwamvita akalazimika kusema uongo.

Kisiwani Mafia. Kulikuwa na umuhimu gani wa kwenda huko kipindi hicho? Masu aliuliza, lakini akahisi amezidisha wivu, akahiari kumruhusu.

'Basi uwe makini, sitaki Jambo baya likupate wewe, Wala mwanetu, ukiona namna gani,..' akasita, halafu akamalizia, ' ..sawa, umesema simu yaweza isipatikane. Uwe makini tafadhali,' Masu alionesha wasiwasi. Hali hiyo ikamfurahisha Sana Mwamvita, ilimfanya aone jinsi gani mwanaume wake alivyomjali sana. Wakati bado tabasamu halijesha usoni mwake, ujumbe mfupi ukaingia kwenye simu yake. Ulikuwa mwamala wa fedha, alikuwa ametumiwa elfu hamsini na Masu. Mwamvita moyo wake ukatakata, SI wanasema pesa sabuni ya roho?

Baada ya makubaliano Kati ya mzee Abuubakr na Masu, Masu aliazimia kwenda nyumbani kuwashirikisha familia yake habari hizo ili kuchakata mipango ya harusi yake. Hivyo, Masu na Mwamvita walijua kinachofuatia ni wao kuanza familia.

Alipowasili kijijini Malonje, Masu aliitazama Nyumba ya wazazi wake, Ilikuwa Nyumba kubwa, lakini Ilikuwa ya zamani. Bati zilishaweka kutu, akaazimu moyoni, baada ya miezi mitatu hivi, angewawekea jengo la kisasa kabisa hapo kijijini. Angeweza kuwahamishia mjini lakini alijua wazazi wake walivyokuwa wabishi. Wangekataa na kuleta hadithi za Paukwa Pakawa. Wangesema mkataa Kwao mtumwa. Akaazimu kuwapelekea mahitaji muhimu pale pale.

Kabla ya kwenda Malonje, alikuwa kapitia chuo Cha mifugo pale Morogoro, akaulizia Bei ya ng'ombe wa maziwa wa kisasa, gharama za kuandaa mabanda na taratibu za utunzaji, akawapata na wataalamu wa kuweka miundo mbinu hiyo vizuri. Baada ya wiki moja, wazazi wake wangekuwa na mifugo hao. Aliwapasha wazazi habari hizo, mama yake akafurahi mno. Baba yake akafurahi Sana pia. Lakini habari iliyowafurahisha zaidi Ilikuwa juu ya kuoa. Hawakuwa na kipingamizi.

***

Wakati anaingia kwenye ndege uwanja wa Kisauni, Mwamvita alijaribu kuwasiliana na Shangazi yake

Amina. Simu yake haikupatikana. Akakumbuka pia Jana ya siku hiyo alijaribu kuwasiliana naye lakini hakupatikana. Hata hivyo hakujali Sana, baba yake alikuwa kawasiliana na Shangazi na kumhakikishia angempokea katika uwanja wa ndege wa Salalah, ambapo wangepanda gari kuelekea yalipo makazi ya Shangazi yake huyo, jijini Salalah kwenye mitaa ya watu wenye fedha zao, mtaa wa sultan Qaboos.

Safari ilianza, akiwa na matumaini mengi. Ndani ya ndege walifurahia huduma za shirika la ndege la Qatar, na hata huduma hizo ikawa ndio chanzo Cha mazungumzo Kati yake na kijana aliyekuwa pembeni mwake. Kijana huyo alijitambulisha kwake kwa jina la Issa Musa, na alimsimulia Mambo mengi kuhusu nchi ya kifalme ya Oman. Alimweleza kuwa yeye alikuwa na uwenyeji huko kwa sababu alikuwa Ni mfanyabiashara ambaye biashara zake alizifanyia Zanzibar, Dar, Oman na Dubai. Mwamvita furaha yake ikawa timilifu kwa sababu alipata mtu wa kupiga naye soga.

Mara ya Mwisho kwa Mwamvita kwenda Oman Ilikuwa kitambo Sana, alipokuwa na umri wa miaka sita au Saba hivi. Hivyo hakukumbuka mengi na unajua Tena umri huo utoto huwa mwingi, kiasi kila kitu aliona sawa na kilichomfurahisha zaidi ikawa Ni michezo tu na binamu zake Farouk na Farihad. Kumbukumbu ya shangazi yake pia Ilikuwa ile sura ya kipindi hicho, taswira ambayo huenda ilimdanganya. Lakini, si Kweli pia kwamba yeye mwenyewe Mwamvita alikuwa

kabadilika? Aliuona mtihani mbele yake. Sema Nini, hakuwa na shaka yoyote. Shangazi angempokea!

Walipotua Salalah airport, Mwamvita aliteremka akiwa na bashasha.

'Alhamdulilah, tumefika Salama inshallah!' alimweleza Issa Musa.

'Inshallah, imekuwa Heri. Hivyo tutaonana lini Tena bibie?' Issa Musa akauliza.

‘Ah, kusema Kweli sijui, maana Kama nlivyokueleza mie huku mgeni na sijui chochote hapa. Tuombe uzima, inshallah tutakutana TU Kama ilivyokuwa leo!'

'Loh, zama hizi bado watu hutumia kudra juu ya kukutana? Fanya kitu kimoja bibie, nipe anuani ya utakapokuwa au Basi namba ya simu tutawasiliana' Issa Musa alitaka urafiki udumishwe.

'Hapa tu, ntafanya kusubiri mwenyeji wangu, sijui anuani ya wanakoishi, enzi zile alikuwa aishi mtaa wa sultan Qaboos, Sasa huenda weshabadilisha makazi. Simu, labda nikupe nayotumia nikiwa Zanzibar!' Mwamvita alijieleza.

'Nshakufahamu, na hapo kitu rahisi Sasa itakuwa Mimi kukuachia namba yangu ili wewe upatapo namna utanipigia, naweza kukutembeza uifahamu vizuri Oman.' Issa Musa alipendekeza.

Shukrani Sana Musa, kitu Cha kwanza ntafanya nikifika nendako, itakuwa kukujulisha, nimefurahi kufahamiana nawe. Wakaagana!

Alipokelewa na mwanamke mwenye umri wa kukadria miaka 24 au 25 hivi. Huyu alikuja akiwa hamjui mgeni wake kwa sura Wala picha, alikuwa na kibao TU chenye majina yake, akimuonesha kila mdada aliyetoka kwenye ndege, na ilionekana Kama alikuwa anaangalia wanawake wenye mimba tu. Mwamvita alikuwa na mimba kubwa Sasa, lakini Ilikuwa sio rahisi kugundulika haraka, ilijificha kwenye mavazi aliyovalia. Miezi miwili mbeleni, angejifungua. Alikiona kibao chenye majina yake, Mwamvita Abuubakr, akajua huyo ndio mwenyeji wake. Akamfuata.

'Mwamvita? Karibu Sana, Mimi naitwa Mariamu, Shangazi yako alipata dharura tangu Jana akawa amesafiri kwenda Dubai, huenda leo akarudi. Ila Wala usijali, kila kitu Kiko sawa. Pole na safari' Mwamvita alikaribishwa.

'Asante Sana Mariamu, na je, hiyo dharura ni ya Nini?'
'Ni ile shida yake ya Mara kwa Mara, SI unajua amekuwa anasumbuliwa Sana na tatizo la Figo, Eeh, hivyo ikitokea ghafla amezidiwa, ana daktari wake huko Dubai.' Mariamu alimweleza wakiwa wanatoka nje ya uwanja huo wa Salalah. Kuna kitu kilimtatiza Sana Mwamvita. Huyu mwanamke. Kuna hofu ilimkabili kwa huyu mwanamke. Lakini pia, sauti yake, sauti yake haikuwa ngeni masikioni mwake, na hicho ndio kitu kilichomtia hofu zaidi. Hii sauti alipata kusikia, lakini lini na wapi, hakukumbuka. Moyo wake Hata hivyo, ulimweleza, Kuna kitu hakikuwa sawa!

Waliingia kwenye gari, Toyota Camry nyeusi yenye vioo vyeusi, tinted, huwezi kuona ndani ya gari kunani. Ndani mlikuwa na watu wawili, Dereva na kijana mwingine, wote waarabu. Walipomuona walizungumza kwa kiarabu, wakabaini hakuzungumza lugha hiyo.

'Karibo Sena Salalah!' Dereva alizungumza na kuondoa gari. Lafudhi yake ikamjulisha Mwamvita Hawa hawakukijua kiswahili vema.

'Asanteni sana.' Mwamvita alijibu akilazimisha tabasamu. Hakuwa katika Hali njema kabisa. Hakujisikia vizuri. Safari iliendelea akiwa hajui lolote, hajui wapi wako, wapi wanaelekea!.

'Hivo bado Shangazi anaishi pale pale!'

'Pale pale wapi?' Mariamu alihoji, Kisha Kama vile alijishitukia, akatamka haraka

'Oh, unamaanisha mtaa wa sultan Qaboos, haha, aah alihamaga haha, unajua Ni miaka mingi Sasa!' Mariamu aliongea huku akitoa kicheko kilichodhamiria kumpumbaza Mwamvita, kicheko kilichodhihiri Nia fiche.

Hii sauti ya huyu mwanamke, hii sauti...Akili ya Mwamvita ilikuwa inafanya uchakataji wa taarifa juu ya hiyo sauti. Wapi, lini aliisikia?.

'Oh, kwa hiyo alihamia wapi?'

'Alihamiaa, panaitwaa, unajua majina ya Oman bana, kunaitwa mtaa wa Umm Al Ghawarif' Mariamu alimweleza. Ah, akili ya Mwamvita bado Ilikuwa kazini, lakini Sasa ilifikia majibu.

Kumbukumbu ilimwijia barabara. Akachoka kwa ufahamu huu. Akajua ameuzwa Kama mbuzi kwenye gunia. Baba yake, Sheikh Abuubakr, alikuwa kamuuza bintiye, iwe kwa kujua ama kutokujua. Shangazi yake Amina, bila shaka hakujua chochote juu ya mpango huu. Maana sauti ya Mariamu ndiyo sauti ya Shangazi waliyezungumza naye kwenye simu siku mbili zilizopita. Machozi yake yalivyo jirani, uchozi ulimdondoka Mwamvita. Akazuga kwa kulifikicha jicho lake. Akajuta kumdanganya Masu. Nani atamuokoa sasa?

## 15

GARI liliingizwa kwenye geti la kifahari. Ndani ya geti Hilo kulikuwa na uwanja mpana TU wa maua, kijani kikitawala kwa maana maua na majani yaliyopamba mandhari ya kasri ndani ya wigo huu, yalimwagiliwa kwa Maji muda wote kwa kutumia springs. Mbele yao, Mwamvita akajionea tafsiri halisi ya ufahari. Jumba la kifalme, sio la mashahidi, kifalme kwa maana ya mamlaka isiyo na mamlaka zaidi yake. Wazungu huita, absolute monarchy,. Alijua Oman ni nchi ya kifalme, je alikuwa kapelekwa kwa sultan? Aliwaza.

Kulikuwa na Walinzi kila mahali ndani ya jengo hili. Aliingia ndani na kupokelewa kwa mapambo yenye thamani kubwa. Mapambo ghali kabisa yaliyoakisi tamaduni za kiarabu. Sebule Ilikuwa ukumbi wenye samani chache lakini za gharama kubwa. Zulia lilitambaa sebule yote, likiipatia miguu burudani ya kipekee. Raha. Aliketi kwenye sofa, akakodoa jicho kwenye skrini kubwa ya runinga. Mara, akamuona mtu anateremka ngazi kutokea juu, maana jengo hili lilikuwa la orofa tatu.

Alikuwa Ni mwanaume, mtu mzima. Mwamvita alijua atakuwa mwenye Nyumba hii. Akajiweka sawa ili kutoa heshima yake. Mwanaume yule akazidi kujongea.

'Innallah maasabrin' Mwamvita akahamaki.

Huyo hakuwa mwingine, alikuwa yule aliyekuwa kamhofia Toka awali. Mzee Kisiki. Alikuwa kavalia kanzu yake ya rangi ya maziwa, kichwani barakshia rangi ya dhahabu. Alitembea kwa kujiamini Sana. Tabasamu likicheza midomoni mwake.

'Asalaam alaikum, binti Abuubakr. Karibu ujisikie nyumbani. Nimefurahi Sana ujio wako. Wayaonaje mazingira Haya, karibu Sana Oman'

'Alaikum salaam. Shikamoo, mazingira yanavutia. Una Nyumba kubwa Sana hapa, ya kisasa na gharama yake itakuwa Ni kubwa Sana sio mzee Kisiki?'

'Kabisa' akatamka huku akiachia tabasamu laini, halafu akaongezea,

'Hili laweza kuwa lako, huhitaji kufanya kitu kingine ila kunikubali niwe mmeo. Na .. wala usihofie kwa habari ya mwanao, huyo atakuwa mwanangu pia. Unaweza kufikiria maisha Bora ya mwanao Kama atakulia katika maisha Kama Haya. Wewe Ni mrembo, Mungu alikupendelea uzuri, umalkia, unastahili kuishi katika himaya ya Malkia. Hebu kwanza usinipe jibu lako, chukua muda wa kutafakari, Kama hata baada ya mapendekezo yangu utaona Heri ukaishi na yule msukuma kokoteni, tafakari upya itakufaidi Nini usikie kakuacha mjane na mwanao!' mzee Kisiki alipomaliza sentensi hiyo alimwangalia Mwamvita Kama vile alikusudia kukazia ufahamu kwenye akili ya Mwamvita. Halafu akatamka Tena.

'Nimekuwa mshindi daima, sijawahi kushindwa na sitarajii Hilo litokee kamwe. Likitokea, Kisiki atakuwa SI Kisiki Tena. Aatakuwa kumbukumbu yake.'

Mwamvita hakujua Nini Cha kusema, ulimi ulikuwa mzito kusema neno, mikono ilitota kwa jasho, na pua yake nyeupe ikang'aa zaidi kutokana na mwanga wa taa pale sebuleni kuakisi ung'aro uliotokana na kijasho chembamba hapo puani. Alihisi joto, homa ya ghafla.

***

Issa Musa alipotoka uwanjani, akielekea nje kwenye teksi, alipishana na dada ambaye alimfahamu vema. Akajua Kuna shida inajitokeza. Alikwisha fanya biashara kadhaa na mwanamke huyo kabla hajagundua Ni Mafia. Mwanamke hatari ambaye biashara zake halali zilikuwa geresha TU kuficha kile kilichofanywa na genge lake hatari lililojiita 'Entry'. Miongoni mwa biashara za genge Hilo Ilikuwa Ni usafirishaji wa binadamu.

Issa Musa akashawishika kutaka kujua Molio alikuwa na ishu gani hapo uwanjani, aliingia kwenye mgahawa akawa anasubiri kumuona Molio angetoka na Nani.

Genge maarufu la 'Entry' lilimiliki makasino na maeneo mbalimbali ya burudani katika mataifa ya ulaya, Marekani, Asia na Africa. Kwa Africa waliweka makao yao makuu Afrika ya Kusini, lakini Zanzibar kilikuwa kituo muhimu kichosimamiwa na mzee Kisiki, mzanzibar mwenye mchanganyiko wa kizungu na

kiafrika. Mama yake Kisiki, alikuwa mtumbatu, na baba yake hakuwahi kumfahamu. Ilisemekana mama yake alikuwa dobi na katika moja ya Nyumba za wateja wake katika mitaa ya Michenzani, ndiko alikopatia ujauzito uliomleta Kisiki duniani. Jina lake halisi likiwa Ni Halfani Nassor. Kisiki Ni jina alilopata akiwa jeshini kutokana na uwezo aliooneshа katika drill za kijeshi. Alikuwa na uwezo wa kumudu kujificha na ukampita bila kujua Kama Kuna mtu hapo, wenzake kwa utani wakambandika jina Hilo. Likakolea Zaidi pale alipojaribu kulikataa kwa ghadhabu nyingi. Mwishowe akaliridhia. Akawa akiitwa anaitika. Likawa jina maarufu zaidi kuliko jina lake la Halfani Nassor.

Issa Musa aliagiza kikombe Cha kahawa akawa anakunywa taratibu akimsubiri Molio arejee. Mara akamshuhudia Molio akiwa kaambatana na yule mjamzito aliyekuwa kasafiri naye Toka Zanzibar, Mwamvita. Akashituka Sana. Alikuwa anampeleka wapi mjamzito? Mara nyingi biashara yake ilihusisha wasichana wadogo, miaka 12, 13, Hadi kumi na sita. Wasichana ambao kwenye biashara yao hiyo walihakikishia upatikanaji wa faida. Walikuwa Ni rahisi kuwarubuni na kuwatiisha chini ya genge lao kwa vitisho, madawa ya kulevya na hata kuwanyima chakula. Kazi yao kubwa ikiwa kuwaridhisha wanaume waliopenda kutoa fedha nyingi ili kushiriki ngono na hao watoto.

Issa Musa Mara moja akabaini kuwa Mwamvita Yupo kwenye hatari. Lakini angemsaidiaje ikiwa genge Hilo lilijaa watu katili, wengi wao wakiwa ni vijana ambao waliendeshwa Kama maroboti. Hawakuwa na hata chembe moja ya hisi? Mjamzito? Hakuelewa.

Waliopotoka na kuingia na ndani ya Toyota Camry, Issa Musa akadhamiria kuwafuatilia ili afahamu kituo Chao kilikuwa wapi. Hakujua kwa Nini aliamua kujihususha na hili. Labda Ilikuwa ile historia iliyokuwa baina yao hapo awali. Uhusiano Kati ya Issa Musa na Molio, ulikuwa zaidi ya biashara. Walikuwa wapenzi hapo awali. Mahusiano ambayo alilazimika kuyasitisha baada ya kubaini nyendo ambazo hazikumpendezea. Kitu kilichomtia hofu zaidi Ni ukweli kwamba mwananmke huyo katili, alikuwa mtiifu Sana kwake na yeye alidhani alimmiliki. Na huo ulikuwa ni ukweli mwingine ambao ulimshangaza. Hata baada ya kugundua upande wa pili wa mwanamke huyo, alipoamua kuachana naye kimahusiano, Molio alimlilia, akamsihi asimuache. Akambembeleza Sana. Issa Musa alichanganyikiwa. Hakuwa ametarajia kuwa Molio angeendelea kujishusha kwake, alihofia kuwa mwanamke huyo angembadilikia na kumuoneshea makucha yake, haikuwa hivyo. Zaidi, ilionekana kuwa mwanamke huyo aliathiriwa vibaya kihisia na tangazo la kuachana Kwao.

Issa Musa alipolitafakari Sana suala Hilo, alibaini kuwa, mwanamke huyo alimpenda kwa dhati ya moyo

wake. Lakini kwa Nini hakuwa tayari kuachana na 'Entry' ili wawe pamoja? Hapo ndio akagundua kuwa Huenda alikuwa ndani ya kundi Hilo kwa shinikizo. Mwanamke aliyempenda alikuwa Ni mateka, akitumikia kundi Hilo hatari kwa shinikizo kubwa. Kwa mapenzi aliyokuwa nayo Molio, kulikuwa na uwezekano wa kuachana na kundi Hilo, lakini uwezekano huo usingemhakikishia kudumu kwenye penzi lao. Wangempoteza. Issa Musa akajua, maisha ya mwanamke huyo yalishikiliwa na uwepo wake kundini, na kutoka kundini Ilikuwa kusaini mauti yake mwenyewe. Hakuwa na namna ya kumsaidia! Issa Musa akaumia Sana lakini baadaye akaamua kumtoa kichwani mwake na moyoni mwake.

Kumuona Tena hapa, ulikuwa mtihani. Mbaya zaidi, yule msichana mdogo, mjamzito, naye alikuwa anaingizwa kwenye genge hili hatari. Je angemudu kulitazama hili likitokea? Moyo wake ulijaa simanzi, akili yake ikamtuma kujaribu kuwasaidia watu Hawa. Huenda lingewezekana Sasa. Lingewezekana Kama angepata kampani ya mtu mwingine mwenye mapenzi na mmoja wa Wanawake hao, Mwamvita. Mwamvita alikuwa kamwelezea maisha yake ya kimapenzi na kijana Masu, akamweleza mvutano uliokuwepo Kati yake na familia yake ikimtaka aolewe na mzee umri sawa na wa baba yake, mzee Kisiki. Akakumbuka alivyomuuliza kwa utani wakiwa ndani ya ndege.

'Kwani huyo babu Ana sura mbaya kiasi gani, au Unadhani kazeeka haiwezi kazi?'

'Haha, we Kaka unalo lako jambo, maswali gani kuniuliza? Enewei, siyo mzee Sana, maana baba yangu mwenyewe SI mzee kihivyo, Ni miaka 45 hivi na Wala Hana sura mbaya hata Kidogo, nadhani wengi wanamuona mtanashati, Kumbuka Ana wake nane na Ni tajiri, isipokuwa moyo wangu umemwangukia msukuma mikokoteni ha!ha!. Lakini SI haba, tangu niwe na Masu maisha yake yamebadilika, sio msukuma mikokoteni Tena. Maisha yake yamebadilika na hivyo mie naamini Ni kwa sababu ya muunganiko wa nyota zetu. Na Nina amini atakuwa tajiri kuliko huyo babu! Kwa sababu nyota zetu zinang'ara zaidi tukiwa pamoja.'

Issa Musa akakusudia kumtafuta huyo Masu wawe kitu kimoja kuokoa Wanawake waliowapenda, ingawa hakuwa na hakika Kama Molio angekuwa tayari kuokolewa, hata hivyo, aliona Heri kujaribu.

Teksi iliyokuwa inalifuata gari la Molio, ambaye alijitambulisha kwa Mwamvita kama Mariamu, ilifika nje ya jengo lile la kifahari na kushuhudia gari la kina Molio likizama ndani ya geti. Kulikuwa na kibao hapo nje chenye maandishi, 'Halfani Nassor residence', kulikuwa na CCTV camera na ili kutowapa mashaka waliokuwa nyuma ya camera hizo, akamwelekeza Dereva kuendelea mbele na safari. Tayari angekuwa na pa kuanzia.

***

Alipomaliza kuongea maneno Yale, Kisiki aliwaagiza watumishi wake kuhakikisha wanampatia huduma za nyota tano mgeni wake. Yeye akatoka huku akionekana kuzungumza kwenye simu na mtu ambaye Mwamvita alidhania kuwa anaweza kuwa Ni baba yake sheikh Abuubakr.

Aneth Ni binti ambaye alikuwa umri sawa na wa Mwamvita, Ni huyo aliyekuwa amepewa jukumu la kumhudumia Mwamvita. Mtoto wa kiafrika, mrembo kwa sura na umbo lakini mpole asiye na maneno mengi. Aneth alimtembeza Mwamvita ndani ya jengo Hilo akimwelekeza kila sehemu na matumizi yake. Mwamvita akabaini yeye hakuwa Malkia pekee humu ndani, mfalme Kisiki alikuwa na wake wengi nao waliishi humu humu ndani. Kwa Maelezo ya Aneth, wenzao watatu walikuwa wametoka kwenda kufanya shopping kwa ajili yake. Aneth, alikuwa Ni mke mwenza, Kama angemkubalia mzee Kisiki.

Kuna namna Mwamvita na Aneth walionekana kuwa na uelewano. Mwamvita akatumia fursa hiyo kuulizia Mambo muhimu. Aliyoambiwa, yakamchosha na kumnyong'onyesha. Kulikuwa na hatari kubwa mbele yake.

## 16

'Umesema tuko watano, vipi sioni mtoto mdogo hata mmoja humu ndani?' Mwamvita akamhoji Aneth.

'Watoto hawaishi hapa, alishawajengea jengo huko Dubai, huko ndiko wanaishi hao watoto. Ukishazaa, unanyonyesha mtoto miezi sita TU, anapelekwa huko Dubai, watoto hao hulelewa na kukuzwa na watu wenye mafunzo! Anadai watoto hao watakuja kuwa watu muhimu hapo mbeleni.'

'Na mnaruhusu Hilo litokee bila kukataa?'

'Utafanya Nini? Kwa taarifa yako, hapa utaishi Kama Malkia lakini Kuna Mambo utaona Ni Kama uko

utumwani. Mzee Kisiki Ni mgonjwa wa akili nakwambia, maisha yake Ni ya kihuni Sana! Sijui ni Nini kinawafanya watu huko nje wamuone Kama Ni mtu mwema na kumpa heshima wanayompa. Lakini, hata ukijua huna Cha kufanya, Heri kuishi'

'Una maana gani?' Mwamvita akahoji kwa umakini.

'Ya Nini kuandikia mate ilhali wino upo, umefika, kuwa mstahimilivu, utajionea mwenyewe! La kukusisitiza dada Mwamvita, usijaribu hata Kidogo kufikiria kutoroka. Matokeo yake hutayapenda.'

'Aneth unanitisha!'

'Hapana, dada Halima alijaribu kufanya hivyo, akawasiliana na boyfriend wake, wakasuka mipango yao, bahati mbaya Sana, walimkamata huyo kijana, walimfanyia udhalilishaji mkubwa Sana. Halafu wakamwachia. Kijana wa watu alijiua mwenyewe. Huyu Kisiki Ni mtu mchafu Sana. Hafai.'

'Walimdhalilisha vipi?'

'Cha msingi Ni kutambua kuwa hafai, nisingependa kufafanua Sana huo udhalilishaji. Ah, labda nikueleze TU kuwa biashara zake ukiacha mahoteli ya kisasa, makasino, lakini pia anamiliki mitandao ya kusambaza picha za ngono. Hapo ndo ujue Ni udhalilishaji gani nazungumzia. Madawa ya kulevya, yaani biashara zote haramu, ndio Mambo yake.'

'Mh, mbona Haya Ni mateso Aneth?' Mwamvita alizungumza, akaona jinsi alivyokuwa kaingia kwenye shida. Akayakumbuka maneno ya mzee Kisiki, kwamba

je alikuwa tayari kuukana utajiri na bado amkose mtu wake? Kisiki alikuwa kaweka kitisho chake bayana. Alimweleza kumkatalia Ni kukubali ujane. Maana kwamba mzee Kisiki alikuwa tayari kumuua Masu. Habari ya Aneth nayo Ni Kama ilizidisha chumvi kwenye kidonda. Udhalilishaji? Alipokumbuka ulinzi uliopo hapo nje, wale vijana walioongozana na Mariam, uwezo wa kifedha wa Kisiki dhidi ya Masu, Mwamvita akachoka. Alijua Nini Cha kufanya. Alimpenda Sana Masu kiasi Cha kutoruhusu baya limkute. Alimpenda mno asingempenda Tena! Labda mbeleni, Huenda baada ya muda angepata namna ya kumtoroka mzee Kisiki, lakini kwa Sasa mtego wa mzee Kisiki ulinasa windo lake na asingeweza kujinasua. Akili yake ikamweleza ili kumlinda Masu sharti anaswe kwenye mtego wa mzee.

***

Jioni, mzee Kisiki alirejea na wakeze watatu. Mahanjumati yakaandaliwa ya kiwango Cha mgeni rasmi. Mzee Kisiki akatumia fursa hiyo kumhoji Tena Mwamvita juu ya ombi lake.

'Ningependa nikutambulishe, ila sijajua bado msimamo wako. Kama utaona vema, naweza kukutambulisha Kama dada yangu kwa leo, Hadi utakapokuwa tayari kwa heshima ya mke wangu. Je, ungependa nikutambulisheje?' Mwamvita akapepesa macho, Kidogo apaliwe na kinywaji alichokuwa anakunywa. Akatafakari ile simulizi ya kutisha

aliyosimuliwa na Aneth mchana. Akamtamkia Kisiki kwa Sauti laini,

'Nimekuwa naliwaza ombi lako tangu tulipozungumza mchana. Kusema Kweli, labda Ni utoto TU ulikuwa unanisumbua. Siwezi kuacha nafasi hii muhimu unayonizawadia mzee Kisiki. Waliosema vya kale dhahabu hawakukosea. Kwa hakika naaamini mzee wangu Sheikh Abuubakr, aliona mbali kwa hili. Nipo radhi kuolewa nawe mpenzi' Mwamvita alizungumza, Hilo neno mpenzi likimkinai moyoni, alilazimika kulitamka. Akili yake ilimpa tumaini. 'Nafanya hivi kwa ajili ya mwanangu na kipenzi changu Masu. Nakubali hili ili nipate kujipatia muda wa kuweka mipango yangu sawa. Mzee Kisiki, kwa hili sitakusamehe kamwe, nitakufanya ujutie maisha yako'. Mwamvita alijiapiza moyoni. Usoni alionekana kutabasamu na kujawa furaha wakati Halfani Nassor aka mzee Kisiki akimtambulisha kwa ufahari kwa wake wenza.

'Haya tusikilizane kidogo' mzee Kisiki alitamka. Watu wote wakampatia masikio yao, akajikohoza Kidogo kurekebisha Sauti akiwa kasimama. Mikono ya kanzu yake kaikunja Hadi kwenye kisuguti. Alikuwa mwanaume jabali, mgumu Kama Kisiki, bila shaka kazi ya jeshi ilimfunza Vema kugangamara.

'Aneth, Samira, Halima na Eva, Leo tumepata ugeni, najua wote tuliutarajia, na Ni furaha yangu kumtambulisha kwenu mke wangu Mwamvita binti Abuubakr. Mwamvita dear, hawa hapa Ni dada zako,

wake zangu Eva, Halima na Samira. Najua Aneth mmeshakutana na kufahamiana tayari. Kama uonavyo, hapa tunaishi kwa umoja na upendo. Ni matumaini yangu utaishi Vema na wenzako. Kwa leo, tumeonelea Vema tukibaki wanafamilia, lakini Kesho utatambulishwa kwa watumishi mbalimbali wa hapa nyumbani. Karibu Sana, cheers!' Akajinyanyulia glass yake ya wine na kugonganisha na ya Mwamvita, halafu zoezi likaendelea kwa wakeze wengine na wote wakigonganisha glass zao.

Mwamvita, alibaini kuwa wake wenza sawa na yeye hawakutofautiana Sana kiumri. Mkubwa wao Eva alikuwa na miaka 18, hao wengine walikuwa Ni miaka kumi na Saba isipokuwa Aneth, huyu alikuwa mdogo zaidi, miaka 16. Wote waliingia mikononi mwa mzee Kisiki kwa shinikizo la wazazi wao. Na wote kilichosababisha wajikute kwenye himaya ya Kisiki, Ni ule ujinga wao, wa kukimbilia mapenzi bila kujua Nini ingekuwa matokeo yake. Walipojikuta na mimba na kukimbiwa na wapenzi, mzee Kisiki alipendekeza kuwaoa, kuwaepusha na adha ya kunyooshewa kidole kwa kule kubeba mimba wakingali makinda.

Sio Kama waliyafurahia maisha waliyoishi hapo, la hasha, walilazimika kuishi. Hawakuwa na namna nyingine. Kisiki alidhani walifurahia maisha aliyowapa. Akaufurahia ule ushirikiano wao. Hakujua tu. Walimdharau. Ushirikiano wao uliumbwa zaidi na ile Hali kwamba walilazimika kuwa naye. Ule ukweli

kwamba hakuwepo aliyehisi wivu dhidi ya mwenzake kwa vile hakukuwa mapenzi ya dhati. Walimwigizia. Lakini pia ile tambia mbaya aliyofurahia zaidi mzee huyo, iliwafanya wakeze waishi naye kwa kuigiza ili kuepusha familia au watu wao na kichaa Cha mzee huyo. Kisiki hakuwahi kudhani kuua Ni kosa, kwake ilikuwa burudani TU kuunyofoa uhai wa mtu bila woga! Walimwogopa mno lakini haikupaswa kuwa bayana machoni pake. Hivyo, walimwigizia.

Alichokisema Aneth juu ya mzee huyo kuwa kichaa, Mwamvita alijionea usiku huo huo. Mzee huyo hakuwa na Soni hata Kidogo. Alikuwa chizi.

'Muda wetu tayari. Mke wangu mpenzi Mwamvita jiandae mama, Ni muda mwafaka ukutane na mumeo.' mzee Kisiki alitamka Kisha akaoneshà ishara kwa vidole vyake. Halima akatoka kwenda chumbani, aliporudi alikuwa na kamera mkononi. Video camera.

***

Issa Musa kutokana na safari zake za Mara kwa Mara huku Oman, na hasahasa jijini Salalah, aliamua kupanga kwenye apartment katika mtaa wa Al Muntanzah ili kupunguza gharama kubwa za kulala mahotelini. Apartment yake Ilikuwa ya wastani, ilimfaa Sana kwa maana hiyo. Pale alipokuwa hayupo, apartment hiyo ilifanyiwa usafi na kampuni la usafishaji Nyumba la jijini humo, maarufu Kama Clean Home Co. LTD. Kwa

kawaida aliporejea, wafanyakazi wa kampuni hiyo walipata taarifa ili kuhakikisha anakuwepo mtu wa kukabidhi funguo. Alipofika alimkuta Ramla akimalizia usafi, wakasalimiana, akapata taarifa mbili tatu, Ramla akaondoka.

Issa akaweka mizigo yake, begi dogo lenye vitu vyake muhimu. Akafanya mawasiliano na wafanyabiashara kwa ajili ya kuweka Oda au appointment ya kuonana. Alipomaliza, akachukua kitabu Cha anuani, akatafuta jina Halfani Nassor residence. Akanakili namba ya simu. Akaiacha mezani na kishajara chake Kidogo. Akaingia bafuni kuoga. Baada ya mipango yake ya Kesho, alikusudia kupiga simu nyumbani kwa huyo tajiri Halfani Nassor walikoingia Mwamvita na Molio. Alitaka kufanya upelelezi wake kabla ya kuchukua hatua madhubuti kwa ule mpango aliokuwa anaandaa akilini mwake. Kuwaokoa Molio na Mwamvita.

Usiku ulipoingia, Issa alielekea kwenye mgahawa maarufu pale mtaani kujipatia chajio. Akiwa hapo, alimuona mmoja Kati ya wale vijana wa kiarabu waliokuwa na Molio wakati wanamfuata Mwamvita pale uwanja wa ndege. Issa akapata Wazo! Huyu lazima atakuwa na mawasiliano ya Molio. Tangu walipoachana na Molio, aliona Vema kufuta namba za mwanamke huyo. Wazo lake lilikuwa hatari. Alihitaji namba ya Molio, asingeweza kuipata hivi hivi. Asingeweza kumuomba kijana yule mwenye tattoo mikononi na

shingoni. Angeweza kuipata kwenye simu ya kijana huyo.

Alijongea mezani alipokuwa amekaa kijana yule akiangalia mechi Kati ya Liverpool na Manchester. Alikuwa shabiki wa mashetani wekundu kutokana na rangi ya jezi aliyovalia.

'Ah, tayari mashetani washafanya yao?'
Issa alizungumza akikusudia kumvuta kwa mazungumzo kijana yule.

'Hatukawiagi sisi, mtu mbaya Pogba keshafanya yake.' kijana alijitapa. Wakaendeleza porojo zao za mpira na hatimaye akapata alichohitaji.

'Naitwa Ibra, nimefurahi kukufahamu. SI vibaya nikipata namba yako ya simu. Umesema Una biashara Zanzibar, Mimi hufika hapo Mara kadhaa, naamini nimepata mwenyeji'

'Kabisa kabisa. Issa ndio jina langu Kaka. Nipe simu nikuandikie namba yangu.' Ibra akimkabidhi bila wasi wasi. Issa Musa alipoishika simu ya Ibra moja kwa moja akaingia kwenye simu zilizopigwa. Akaliona jina la Molio. Akaikariri namba ile kichwani halafu akamwandikia namba yake Ibra. Alipomaliza zoezi Hilo, aliihifadhi namba ya Molio Kisha wakaendeleza soga zao za mpira. Liverpool walikuwa wamesawazisha kupitia penalti iliyochongwa vyema na kiungo mshambuliaji Salah.

Aliporejea kwenye apartment yake, Issa alimpigia simu Molio.

'Hallo' Sauti yake haikubadilika, Ilikuwa vile vile. Sauti tulivu isiyo na pupa. Kikawaida usingeamini mwanamke huyo alikuwa sehemu ya genge hatari kabisa la 'Entry'.

'Mambo vipi Molio, unazungumza na…'

'Najua, nikusaidieje' Molio alimkatisha na kuuliza swali lililotafsiri chuki au kuchokwa kulikokinaisha.

'Nahitaji kuonana na wewe. Kuna Jambo…'

'Kinachokufanya uhisi Nina muda wa kupoteza na wewe Nin…'

Safari hii Issa aliamua kudinda. Akamkatisha kauli Molio na kuzungumza.

'Jawhareity apartments, no 23. Ukitaka Njoo ukiona vipi acha.' Issa akakata simu. Hakutaka mwanamke huyo amwendeshe. Alimfahamu Vema. Kubembeleza kungechelewesha Mambo lakini pia alijua kwa staili hiyo Molio angebaki njia panda. Angetaka kujua Ni Nini hicho kilichomtia kiburi. Na kusema Kweli, Issa hakuwa na hakika ya lolote. Aliamua kucheza patapotea. Kama asingetokea, angelazimika kupiga simu ya nyumbani kwa Halfani Nassor ili kupata mawasiliano na Mwamvita. Akaamua kupotezea swala Hilo, akawasha runinga ajionee yanayoendelea ulimwenguni.

Mwendo wa saa tano hivi, usingizi ukiwa unaanza kushika hatamu, akasikia hodi mlangoni. Akanyanyuka Taratibu, na kusogea mlangoni. Akachungulia kwenye kitasa. Nje alisimama Molio. Issa Akatoa tabasamu na kufungua mlango.

## 17

Mlango ulipofunguliwa TU, Molio akaingia ndani bastola ikiwa mkononi. Issa Musa hakuelewa. Akashituka mno na kuhofia maisha yake.

'Unafurahi kucheza na hisia zangu sivyo? Unachonitaka Ni Nini? SI ushanikataa? Kunifuata fuata maana yake Nini?' Molio aligeuka mbogo. Alishajishusha Sana kwa mwanaume huyo, akambembeleza kwa magoti, lakini jamaa akajifanya kauzu.

'Siwezi kuwa nawe Tena. Labda uachane na Entry.' Ilikuwa kauli yake ya Mwisho. Kauli iliyomfanya Molio anyanyuke kimya kimya na kuondoka zake kwa unyonge. Alimpenda Sana Issa angeweza kufanya chochote kwa ajili yake isipokuwa kuachana na 'Entry'. Hiyo Ilikuwa ngumu. SI kwa sababu alifurahia Sana kuwa ndani ya genge Hilo. La! Bali kwa sababu alikuwa mtumwa, ambaye maisha yake yaliendeshwa na kundi Hilo. Alishajaribu kutoroka. Lakini daima walikuwa na namna ya kumpata. Na Mara zote walimpata akiwa nusu kaputi au kwenye maumivu makali. Wakubwa wa 'entry' walitumia teknolojia kuwaweka chini ya himaya yao daima. Akakumbuka jaribio lake la Mwisho.

Alikwisha fika Zanzibar na Kesho yake alikuwa apande boat kwenda jijini Dar. Kutoka hapo alikusudia kwenda kijijini Kwao huko Bukoba. Alikuwa amejiwekea vijisenti vya kutosha ambavyo angemudu kuweka duka la vinywaji na angeishi maisha ya Kawaida. Hakutaka Tena maisha ya kutumikishwa kufanya kazi iliyodhalilisha Wanawake. Lakini ilipofika saa Tisa usiku, akiwa hotelini, alianza kuhisi maumivu ya kichwa. Akaamka apate walau Panadol za kuyatuliza maumivu yale. Hazikusaidia. Muda ulivyozidi kwenda alihisi anapata wazimu. Macho yake hayakuweza kuona Tena, akajaribu kutoka akapate huduma ya daktari. Akaanguka chini na kuzima. Alipoamka, alikuwa Oman. Mara ya kwanza pia ilimtokea Hali Kama hiyo, akajua Ni ugonjwa TU. Alikuwa airport Salalah, wakamfuata hapo. Mara ya pili, ndio alibaini kuwa sehemu fulani mwilini mwake kulipandikizwa microchip ambayo ilimletea shida hiyo. Na zaidi pia, ilitumika kuwaonesha wapi alipokuwa ili wao wamfuate.

Hivyo, ombi la Issa Musa kwamba aachane na 'Entry' lilikuwa gumu kutekeleza. Asingeweza. Hakujua namna ya kujitoa kundini humo ikiwa waliyaweka maisha yake mkononi mwao.

'Hey hey hey, tafadhali Sana mpenzi, bastola hiyo' Issa Musa alitamka huku akinyanyua mikono yake juu, akirudi nyuma kwa kihoro.

'Nani mpenzi wako? Unacheza na maisha yangu? Unaona sawa kuchezea hisia zangu?'

'Ungenisikiliza kwanza Molio, hujui nimekuitia Nini, mbona Una maamuzi ya ghafla ghafla hivyo?' Issa Musa alikuwa kakifikia kiti pale sebuleni. Akajibweteka bwete bila kupenda. Jasho lilikuwa linamvuja usoni Kama kanyeshewa, Hali hiyo ikamfanya Molio afurahi moyoni. Kicheko kikaishia kooni. Akajikaza kukizuia na kuendeleza ubabe wake.

'Enhee umeniitia Nini?' akatamka Molio, akishusha bastola yake, Kisha akaangua kicheko.

'Hahaha, dah sijawahi kuona mwanaume mwoga wa kifo Kama wewe! haha!. Sijui hata nilikupendea Nini lol, mwonee!'

Issa alikuwa kalowa jasho. Alikuwa anahemea juu juu. Hofu yake Ilikuwa bayana. Tangu alipotambua uhusika wa Molio kwenye genge la Entry, alianza kumuogopa. Alifahamu ukatili wa watu hao. Hawakuwa na hisia hata chembe na ukatili Ilikuwa hobby yao. Walikuwa wanaweza kuua huku wakicheka, na Hadi ukifikie kifo, ulikuwa uwe umepitia mateso makali Sana. Watu wa entry hawakuwa binadamu, walikuwa maroboti. Majitu yasiyo na hisia za huruma Wala hofu ya kifo. Hicho ndicho kilichomtoa jasho. Vipi Kama Molio alikuwa keshafikia kiwango hicho. Na SI hatari zaidi kwamba alimtia chuki kwa kule kumuacha wakati yeye alimpenda?. Issa alikuwa taabani.

'Tafadhali Molio, plizz iweke mbali hiyo silaha.!'

'Mbona unaniogopa hivyo Issa, Ni Mimi, Molio. Unaweweseka Ni Kama umeona jini jamani! Huwezi kutaniwa?'

'Tatizo sio wewe mpenzi, unajua sikuogopi, shida Ni kwamba sijui Kama umekuja Kama Molio au Kama 'Entry'. Nawafahamu entry, wale Ni zaidi ya jini. Wanaogopesha. Na ulivyoingia hapa,kusema Kweli umeingia Kama entry. Umenitisha Sana!'

'Mh, Haya Basi, hebu nyanyuka bwana, Ni Mimi Molio, nimekuja kuitikia wito wako. Wasemaje Issa?' Molio akatamka kwa Sauti tulivu, ile Sauti aliyozoea Issa.

'Oh, Nahitaji maji ya kunywa, naona kiu.' Molio akamchukulia maji kwenye jokofu na kumkabidhi Issa.

Alipokwisha kunywa, wakaketi kwenye sofa, Molio akimfuta jasho kwa kitambaa chake. Issa akatulizana.

'Nimekumiss Sana mpenzi, nimejaribu kuwa bila wewe, siwezi. Nakuhitaji. Amini, kwa Kweli sitanii kabisa Molio' Issa alitamka. Muda wote akiyazungumza hayo, Molio alikuwa anamwangalia TU usoni. Hisia zikijijenga taratibu. Alimhusudu kijana huyo. Hivi Ni kwamba Jamaa alipokuwa akijieleza, Molio alikuwa anapiga hesabu itakavyokuwa muda mfupi ujao. Maelezo ya Jamaa aliyokuwa anaeleza Wala hayakuwa yanamfikia Molio. Alikuwa kazama kwenye ndoto zake kihisia.

'Molii' Issa akaita kwa Sauti, lakini kimahaba. Molio akazinduka. Akapanda miguuni kwa Issa wakawa

wanatazamana Ana kwa ana, Molio akaishika shingo ya Issa wakakutanisha midomo yao. Ni Kama walikuwa na njaa ya mabusu. Maana Ilikuwa Kama wanashambuliana. Issa Musa akanyanyuka juu akiwa kashika chini ya makalio ya Molio kwa uthabiti. Akambeba na kwenda naye chumbani.

***

Ilikuwa ijumaa tulivu. Habari zilizohusika na kuvuma siku hiyo zilikuwa habari za matokeo ya kidato Cha nne. Masu alizisikia habari hizo akiwa jijini Dar es salaam. Miongoni mwa waliofanya mtihani huo ambao katibu mkuu wa baraza la mitihani alitangaza ongezeko la ufaulu kwa asilimia tano, alikuwa Ni mpenziwe Mwamvita. Mwamvita ambaye kwa siku ya pili Sasa alikuwa hampati kwenye simu Kama alivyokuwa kamweleza. Alikuwa na wasiwasi mwingi juu yake, lakini alipokumbuka kauli ya mrembo huyo kuwa Hilo la simu kutopatikana linaweza kutokea, alituliza mtima wake.

Aliingia mtandaoni na kugoogle 'matokeo kidato Cha nne 2018', akaletewa machaguo mengi kutoka kwenye websites na blogs kibao. Akaamua kutambaa na website ya NECTA, alipoingia hapo, akaona link iliyokuwa na maandishi yenye wino mwekundu yakianza na neno 'new', matokeo kidato Cha nne 2018. Akaibonyenza. Link ikafunguka. Kwenye search, akaandika Maji kupwa sec. Jina Hilo likatokeza na yeye akalibonyeza, matokeo

ya Maji kupwa yakaonekana barabara. Kwenye summary pale juu ya ukurasa huo, ilionesha Shule ilifaulisha wanafunzi 00 kwa daraja la kwanza, yaani Div I, Watano Div II, 59 Div III, 168 Div IV, waliopata zero, walikuwa 92 na watoto 34. Akajiuliza Mwamvita atakuwa kundi gani. Hiyo ikamtia mshawasha wa kutaka kuyajua matokeo ya mkewe tarajali. Akatafuta namba ya mtihani ya Mwamvita, namba 167. Akatabasamu, Mwamvita alikuwa miongoni mwa wale waliopata Div III, ya kwake ikiwa inang'ara kwa point 21, Ni kusema alikosa point moja tu, kupata Div II. Akachukua simu yake ampigie Tena Mwamvita, hakupatikana. Akaazimu Kesho yake kuingia Zanzibar.

Kama kawaida, Masu alipoingia Zanzibar, alimtafuta msela wake Yusuf, akamweleza anataka wafike ukweni. Yusuf akatinga suruali ya kitambaa nyeusi na shati jeupe na kiatu chake Cha mchongoko. Ile gari ist, ilikuwa hapo kwa Yusuf, kamanda Masu alimwachia bila kinyongo apigie misele. Na watoto wa kike walimkoma kwa siku tatu hizi alipokuwa na gari hiyo. Alipotoka nje, aligundua gari hiyo Ilikuwa na vumbi kutokana na misele hiyo. Kama akiipeleka car wash, atamchelewesha rafiki yake. Ilionekana Masu alikuwa na furaha kubwa Mwamvita kufaulu mtihani. Alitaka awashirikishe, au kuwa sehemu ya furaha ya famia yake. Alikuwa keshapiga simu kwa Sheikh Abuubakr na kumweleza kuwa wangefika hapo kwa mazungumzo. Sheikh

Abuubakr akauliza muda gani, Masu kwa furaha Sana akamweleza saa Tisa alasiri. Miadi ikakubalika!

Sasa, Ilikuwa yapata saa Tisa kasorobo. Master Park Hye alishawafundisha kufanya Mambo kwa muda, Yusuf akaona heri wakienda na piki piki yake aina ya Kapoor, ile iliyotumika pia kwenye tukio kwa Nzinyangwa tapeli. Walipokutana, wakashangaa kujiona wamevaa sare. Ungedhani walipanga hivyo. Walipendeza SI Kidogo. Watanashati wawili.

Waliingia kwa Sheikh Abuubakr saa Tisa kamili. Wakakaribishwa. Chakula kilikuwa kimeandaliwa na Mama Mwamvita akishirikiana na dada wa kazi. Sheikh Abuubakr alikuwa kaalika wazee wenzake watatu, mzee Abdalla, mzee Juma na mzee Khamis. Wote majirani zake. SI haba kwamba wao pia walikuja na wake zao. Basi ikawa Kama sherehe hivi, maana wamama wale wa kizanzibar, walipiga vigelegele Masu na Yusuf walipoingia na sare zao. Mazungumzo yakashika hatamu, Masu akaeleza mpango wake wa kuhakikisha Mwamvita anaendelea na masomo ya kidato Cha tano baada ya kujifungua. Wazee wale wakamsifu Sana kwa uungwana huo. Ilikuwa furaha. Ila, Kuna vile Sheikh Abuubakr alionekana kukaa tenge Sana, akawa yuatazama Sana getini muda mwingi, na Hali hiyo Yusuf aligundua. Mlango wake wa fahamu, ule wa sita waliofundishwa na Master Park Hye, ulikuwa unampa taarifa. Lakini, ah, akaamua kujumlisha na kugawanya, akapata sawa sawa na wasi wasi wa bure. Yaani akahisi

kuwa,Huenda mzee huyo alikuwa tu na mchecheto wa kawaida.

Mara, akamuona Sheikh Abuubakr anaomba udhuru Kidogo. Akatoka nje ya geti. Mh! Alamu kichwani kwa Masu ikagonga kengele. Hataa! Kuna Jambo. Haiwezekani. Akamnong'oneza Masu.

'Ebwanaee, mkweo mbona simusomi, simwelewi walahi'

'Ah Yusuf mtu wangu, unakuwa aleti muda wote. Tulizana. Huyo atakuwa kuna mgeni anamtarajia Sema kachelewa kufika. Hapo ameona heri ajue Kulikoni. Atakuwa kaenda kuchungulia Kama yuakuja na asipomuona, atamrukia hewani.'

'Yaa, Hilo litakuwa Hivo bila shaka'. Yusuf akaona heri kulipotezea. Wakaendelea kujichana kwa kuku, pilau, soda, roast ya nyama, mboga mboga, Jamaa, mamkwe mpishi nyie!

Sheikh Abuubakr akarejea. Wasiwasi ule aliotoka nao, alionekana kuutua huko huko nje! Ile sehemu iliyokuwa wasiwasi Yusuf akaona ridhiko, yaani Kama vile kulikuwa na uhakika na SI mashaka Tena. Chochote alichofanya huko nje, kilimpa tulizo la moyo, moyo ukatuama. Lakini Hali hiyo, kwa Yusuf iliamsha Tena wasiwasi wake maradufu. Akamsogelea Tena Masu na kumnong'oneza,

'Kaka, kaa kikamanda, nna uhakika mzee wako bado ana gubu, Kuna kitu hapa hakiko sawa, nahisi harufu ya

Shari. Huyu mzee wako sijawahi kumwamini toka alipokutandika bakora hapahapa.'
Wakati anamalizia kuongea, Masu akiwa anataka kujibu hoja, kukasikika hodi getini.

Huyoo!

Sheikh Abuubakr akakurupuka kwa Kasi ya kimbunga. Akaelekea getini. Hata Masu Sasa akajua hapa Pana msala. SI kwa haraka ile aliyosimamia mzee Abuubakr. Vijana wakakaa mguu sawa!

Ah! Jamaa!. Masu na Yusuf wakamuona mzee anarudi, nyuma yake walikuwa wajomba. Askari wa jeshi la polisi wanne. Ule muungurumo wa gari nje, Kumbe Ilikuwa defender la polisi. Sasa Sheikh Abuubakr alikuwa anawanyooshea kidole chake, na Sauti yake ilisikika barabara.

'Huyo mjinga kamtia mimba binti yangu, Sasa kamficha sijui wapi, na anathubutu kuja hapa akitaka amuoe, binti mdogo, mwanafunzi wa skuli Hapo maji kupwa. Nataka muwashughulikie vizuri na washitakiwe kwa kosa la ubakaji na utekaji!' Sheikh, Sauti yake ilitoka kwa Sauti ya mrindimo mithili ya subwoofer, mishipa ikimsimama barabara shingoni. Povu Kama lote. Na alionekana kubadilika rangi ya ngozi yake usoni, alifura na kuwa mwekundu, Kama mtu anojaribu kujizuia asibanje! Kijasho chembamba kikimshuka kwenye pua yake ndefu!


Hakika ulikuwa mshituko mkubwa Sana. Mama Mwamvita Kiasi azimie, wazee wenzake Sheikh, majirani waliokuwa na furaha muda mfupi uliopita, walibaki vinywa wazi kwa mshituko.... Kilikuwa kisanga Cha aina yake.

ASANTE SANA MSOMAJI WANGU. KAMA UMEIPENDA NA UNGEPENDA KUJUA KAZI YA MZUNGU NI NINI, NINI HATIMA YA WAHUSIKA WETU MASU, MWAMVITA, MOLIO NA ISSA, FUATILIA SEHEMU ZIFUATAZO.

SIMULIZI HII INAENDELEA HADI SEHEMU YA 36. KUPATA MWENDELEZO WAKE, LIPIA TSH 4000/= KWENDA VODA **0744509465,** iliyosajiliwa kwa jina DAVID NGOCHO SAMSON, AU HALOTEL **0629077792** iliyosajiliwa kwa jina DAVID NGOCHO SAMSON. KISHA NIJULISHE NIKUTUMIE KWA EMAIL, WHATSAPP, TELEGRAM AU VYOVYOTE UTAKAVYOONA INAKUFAA.

USIKOSE NAKALA NGUMU YA VITABU VYANGU VIWILI AMBAVYO VITAKUWA MADUKANI KUANZIA JUNE 2020. TINEJA NA MATEKA WA HUBA.

# TINEJA




# PATA KIONJO CHAKE

**U**siku wa manane katika mji wa Embakasi nje kidogo ya jiji la Nairobi ukimya ulitawala. Giza totoro liliufunika uso wa nchi. Zilisikika sauti za mikoromo ya watu waliokuwa wamelala fofofo na kupotelea katika ulimwengu wa usingizi. Ulimwengu ambao bila shaka unakaribiana sana na lango la peponi. Mahali ambapo kila mtu anatamani kufika siku moja baada ya kumaliza safari yake ya kuishi duniani.

Kelele na purukushani za usiku hazikusikika usiku huu. Stima ilikuwa imekatika na hivyo kuwafanya wafanyabiashara waliotumia mwanga wa stima kufanya biashara zao wawahi majumbani mwao kupata usingizi

kujiandaa na kesho yake. Kimya kilitawala jiji hili mashuhuri kwa afrika mashariki. Jiji lenye watu wanaojua kutumia muda vema. Usingemkuta mtu anatembea kizembe jijini Nairobi, ni kama kila mtu alikuwa anakimbizana na muda na alikuwa na shughuli ya kufanya, ilikuwa ni ajabu kwamba siku hii purukushani hizo hazikuonekana.

Mvua kubwa ilikuwa inanyesha ikiambatana na upepo mkali na mwanga wa radi ukimulika jiji na ngurumo kubwa zikiwafanya wakazi kuvuta mablanketi yao.

Katika kitongoji cha Kibera, kitongoji maarufu sana jijini Nairobi kwa kukusanya watu wengi waliobahatika kukosa maisha mazuri lakini wakiwa na imani tele juu ya maisha. Watu waliishi maisha ya umaskini mkubwa katika nyumba zao walizojenga kwa kutumia maboksi na mifuko ya nailoni huku wakijisaidia kwenye vifuko vya plastic kwa kukosa vyoo. Kitongoji kilichoandamwa na magonjwa ambukizi ya mara kwa mara. Ni katika kitongoji hiki pekee kulipoonekana kuwa na harakati na purukushani, purukushani za kutetea maisha dhidi ya hasira ya mvua hii kubwa. Kelele za vilio vya watoto na watu wazima zilisikika. Wengi walikuwa bize wakijaribu kuziba matundu yaliyokuwa yanavuja na wengine wakijaribu kuchimba mifereji ili kuzuia mafuriko yaliokuwa yanazidi kuvamia makazi yao. Hii ilikuwa ni moja ya tofauti kubwa ambayo binadamu alimudu kuumba na sasa ilionekana ni kawaida tu kwa mtu kuwa maskini sana na mwingine kuwa tajiri kupindukia. Waliokuwa maskini siku zote walijikuta pamoja wakishiriki bakuli la umaskini na hawa walikuwa wengi. Tajiri nao walionekana pamoja lakini

kila mmoja akiwa na bakuli lake la utajiri huku akiutamani mchuzi wa bakuli la mwenzie.

Huko *Baraka estate* ,Embakasi,hali ilikuwa tofauti ukilinganisha na Kibera. Huku waliishi watu waliokuwa na uwezo wa wastani. Hawa walimudu kumiliki magari aghalabu kwa sababu wengi walikuwa ni wafanyakazi wa serikali na wajasiriamali. Mvua hii kubwa wala haikuwa na madhara yoyote kwao. Ilikuwa ni hali ya kawaida tu. Nyumba zao imara na miundo mbinu bora iliwawezesha kulala bila wasiwasi wowote.

Eve aliyekuwa amelala na mumewe Salimu alijaribu kupata usingizi lakini usingizi ulidhamiria kumkimbia. Kwa wiki nzima sasa alikuwa anasumbuliwa na ndoto za utoto wake. Mara zote alipoota na kushtuka alikosa kupata usingizi tena. Usiku huu pia alikuwa kaota ndoto, na kushtuka. Aliamuka na kuwasha taa. Stima (umeme)ilikuwa imekatika. Alielekea panapo dirisha na kukunja pazia, ulikuwa usiku wa kiza na mwanga wa radi ulimulika ndani na kutia mwanga mkubwa chumbani. Alishika pazia lile na machozi yakamtiririka. Kichwani mwake alikuwa anasikia sauti ya kilio cha mtoto mdogo na sauti ya mwanaume akimbembeleza asimwache mwanae aliyekuwa analia. Tukio lililotokea miaka zaidi ya ishirini na mbili iliyopita bado lilizidi kumtesa na kujirudia mara kwa mara na kila alipojaribu kupuuza tukio hili lilizidi kumfuata kupitia ndoto. Tukio hili likamchukua na kumrudisha enzi za utoto wake akiwa mtoto wa pekee kwa baba na mama yake. Alipendwa sana na kuthaminiwa na kukuzwa huku akipata mahitaji yote ya muhimu. Akakua mwenye afya na akili njema. Darasani akifanya vizuri kuliko wengine. Historia ikabadilika alipokuwa kidato cha pili. Nafasi

iliokuwa yake haikuwa yake tena. Mwanafunzi mmoja alihamia shuleni kwao na darasani kwake. Huyu aliitwa Elineema, kijana mwenye akili na mwili wa mazoezi. Huyo alichukua umaarufu wake pale shuleni. Alichukua nafasi yake ya kuongoza darasa na umalikia wake wa urembo pale shuleni.

Elineema alikuwa si maarufu tu kwa kufanya vema kimasomo la! Habari ya urembo wa Eve ilipotea na kumezwa kabisa na sifa za Elineema aliyekuwa anazungumzwa na wasichana kwa uzuri wake wa sura na umbo la kimazoezi. Wavulana nao walikuwa wanaanza kumhofu Elineema kwamba alikuwa anachukuwa nafasi zao kwani wasichana marafiki zao walikuwa wanamuongelea yeye hata walipokuwa nao. Hali hiyo ilimfanya Eve aone wivu. Atamani kurejesha enzi yake, alipokuwa mrembo mwenye akili darasani.

Elineema kwa upande wake aliamini kuongoza ni haki yake, mama yake hakusita kumsisitiza kwamba anapaswa kuwa kichwa na sio mkia. Hivyo alisoma kwa bidii na kuhakikisha nafasi hiyo ya kwanza inakuwa ya kwake daima. Mbali na masomo, Elly kama alivyojulikana zaidi, alikuwa kinara kwenye michezo pia. Alikuwa Fundi wa kusakata kabumbu, mbio za meta mia, basketball, volleyball na hata bao. Alijaliwa mwili wa michezo na kichwa cha hisabati. Alimudu masomo yote kwa ufanisi wa juu! Hakuhitaji muda mwingi kushika alichofundishwa, zaidi sana kile alichosikia kilidumu kichwani mwake na kusoma kwake hakukuhitaji beseni la maji baridi ili kutoboa anga. Muda wa darasani kwenye vipindi ulimtosha, muda wa michezo ulitumika kwa michezo. Alijua kufuata ratiba ya shule kwa nukta.

Kitendo cha kufanya vizuri darasani na kupendwa na watu kilimfanya Eve amchukie sana. Alijiuliza ni kitu gani alichokuwa nacho zaidi cha kumfanya awe hivyo. Alitaka kujua. Ili kujua ilimbidi awe karibu na huyo adui yake. Isingekuwa rahisi. Asingefahamu chochote kwa kuwa karibu tu, kulitakiwa kuwepo na hatua zaidi. Kama angetumia udhaifu wa adui yake ingekuwa rahisi, ilibidi aanzishe uhusiano wa kimapenzi.

Taratibu alianzisha urafiki na Elineema, urafiki wa kusoma pamoja. Hilo likamtia hasira zaidi kwani alijiona mjinga sana pale ambapo mambo magumu yalionekana mepesi sana kwa Elineema. Urafiki huu haukufaa chochote. Alidhamiria kumfanya awe mjinga , kama angefanikiwa kumteka kimapenzi ingekuwa rahisi kwani huenda angepunguza ufanisi. Eve akaanza harakati za kumpoteza Elineema kimapenzi. Kwenye kusoma akavaa nguo za kimahaba na kutumia macho yake mazuri kumtega Eli. Alipoona muda unaenda mbele na bado mambo hayaeleweki, Eve akadhamiria kutamka wazi juu ya kutaka uhusiano huo.

Walipokutana kwenye kusoma Eve alikuwa keshaandaa maneno ya kumweleza Eli. Ambacho Eve hakujua ni kwamba harakati zake za awali zilikuwa zimezaa matunda. Macho yake na sauti yake ya kimahaba vilikuwa vimejenga mvuto kwa Eli na sasa ulikuwa umewadia muda wa kushindwa na uzalendo na kuvunja miiko yake binafsi. Waliketi na kutazamana, Eve akitafakari namna ya kuanza kueleza uongo wake

‘Eli......’ Eve alianza kuongea lakini hakumalizia kwani Eli alimshika mkono na kumtazama usoni kwa huba, walitazamana kwa sekunde kadhaa halafu Eve akahisi haya na kutazama chini.

'Eli, naona tuahirishe mjadala' Eve alitamka kwa sauti hafifu sauti ya mahaba huku akimtazama Eli kwa macho ya hisia kali.

Huku akichezea vidole vya Eve, Eli aliuliza

'Una uhakika hicho ndo unachotaka?'

'Nimetoa oni, lakini kama unataka tuendelee sawa tu. Nadhani tuangalie swali la pili hili la kwanza lina njia ndefu' Eve alitamka na kumtupia Eli jicho la kichokozi. Eli hakujibu alibaki anamtazama tu

'Elii! Nini Unaniangalia hivyo?! mimi sipendi!' Eve alitamka tena, mara hii kwa sauti ya kumtoa nyoka pangoni. Eli alihisi mapigo ya moyo yanamwenda kasi,na baadhi ya sehemu za mwili wake zilianza kuhisi mabadiliko. Haikuwa kawaida yake.

'Eve, nataka nikuambie kitu' Hatimaye Eli alitamka. Sauti ya chini, sauti ya kujisalimisha. Alijiona kama mateka wa vita aliyekuwa ameamua kuweka silaha chini na kunyanyua mikono juu.

'Kitu gani?' Eve aliuliza kwa sauti ya mnong'ono.

'Eve...' alisita.

'Sema tu'

'Eve, shati lako..'

'Shati langu!'Eve alihisi hasira, hakutaka kusikia habari ya shati, alitaka kusikia kuwa mtego wake umenasa.

'Eve , nakupenda' Eli alitamka kwa wasiwasi halafu tena

'Eve nakupenda, tafadhali niambie kwamba unanipenda' ni kama alitaka kulia. Eve alimtazama usoni kisha akasimama.

'Eve !'

'Baadaye' Eve alitamka huku akiondoka, moyoni mwake akiwa kajaa furaha kwani hatimaye mtego wake ulifanikiwa kunasa windo lake.

'Baadaye nini?' Eli alihoji

'Utapata jibu'

Baadaye ilipowadia, jibu lilikuwa ni ndiyo ya herufi kubwa. Ndiyo iliyomfanya Elineema atamani kupaa angani. Ndiyo aliyokuwa ameisubiri kwa muda mrefu.

Uhusiano wa mapenzi ukawa umeanza namna hiyo. Uhusiano ulioanza kama mtego ukaendelezwa kwani kwa sehemu ulimrejeshea umaarufu wa sifa yake ya urembo kila mtu akijua Eve anatembea na Elineema. Uhusiano huo ukadumu hadi kidato cha nne, wakiwa wamebakiza siku chache tu kufanya mtihani, siku ya mahafari yao walijikuta wakiwa kitandani wakifurahia mapenzi yao na miaka minne ya sekondari. Tukio lililoonekana la kawaida kwao, tukio la kufurahia mapenzi likawa limefanyika siku ambayo hawakupaswa kulifanya. Siku ambayo Eve alijikuta akishikwa matamanio na kumhimiza Eli wafanye tendo hilo na matokeo yake yakaonekana baada ya kumaliza shule. Eve alipata mimba. Mimba katika umri wa miaka kumi na sita tu.

Baada ya kubaini hilo Eve alimweleza Eli juu ya mimba. Alimtaka Eli amsaidie waitoe hiyo mimba suala ambalo lilikuwa gumu Eli kukubaliana nalo. Eve akidai hakuwa tayari kuitwa mama kwani alikuwa mdogo.

'Eli mimi bado mdogo!'

'Nafahamu Eve, ndio maana naomba usifikirie kutoa mimba mimi nitajitahidi kadri niwezavyo kukuhudumia. Watu wengi wamekufa wakijaribu kutoa mimba na isitoshe ni dhambi kuua..'

Kutokana na taarifa kufika nyumbani Eve aliambiwa kumtafuta mwenye mimba. Alirejea kwa Eli aliyekuwa anaishi na Mr Msofe. Mr Msofe alikuwa ni hakimu katika mahakama ya mwanzo huko Tanga na ilitokea tu wakawa marafiki kutokana na uenyeji wao wa Kilimanjaro. Mr Msofe akawa ni kama kaka yake na Eli. Haikuwa kawaida,kwani pamoja na uhakimu wake Mr Msofe aliamua kumsaidia Eli pale ilipobainika anatakiwa kulea mimba ya Eve. Aliwapokea na kuwasaidia kwa miezi  yote ya ujauzito wakati huo Eli akifanya kazi ya ya muda mfupi kwenye library ya mkoa wa Tanga. Alipoulizwa kwa nini haendi nyumbani Eli aliwajibu wazazi wake kuwa alikuwa anafanya kazi ya muda mfupi na mara baada ya kumaliza angeenda nyumbani.

Hatimaye Eve alijifungua salama mtoto wa kike. Walimpa jina la Jacque. Kwa pamoja walimlea mtoto wao kwa miezi miwili. Baada ya miezi miwili Eve aliyeamini kwamba alikuwa mtoto bado alijikuta anaumia sana kwamba yeye ni mama. Suala hilo hakuliafiki. Uamuzi aliofikia ulikuwa ni kuondoka na kwenda mbali. Huko angeishi kama msichana mrembo na kutua mzigo mzito wa kuitwa mama katika umri wa miaka 16.

Alifanikiwa kupata nauli ambayo ingemwezesha kwenda Dar es salaam kwa shangazi yake. Alimbeba mwanae ambaye alikuwa analia, akajaribu kumbembeleza huku yeye mwenyewe akilia machozi kwa kitendo alichodhamiria kumfanyia. Kumwacha bila mtu wa kumuita mama. Alimfuata Eli na kumwambia

‘Eli, nisamehe tafadhali. Ukweli ni kwamba sipo tayari kuitwa mama. Naondoka, tafadhali mtunze

mwanao. Mtunze vema na awapo mkubwa mwambie mama yake alikufa alipokuwa mtoto, kwa sababu sistahili kuwa mama yake. Siwezi kuwa mama yake.' Alliongea huku machozi yakimtiririka.

'Mwanangu Jacque nisamehe mpenzi, nakupenda ila sipo tayari kuwa mama yako. Nisamehe tafadhali.' Alimwambia mwanae wa miezi miwili tu.

'Eve, tafadhali fikiri upya. Naamini hujachukua uamuzi sahihi. Kwa nini unanifanyia hivi Eve. Unajua siwezi kunyonyesha na mtoto hajafikia umri wa kula vyakula vingine mimi nitafanya nini? Tafadhali tuvumilie kwa miezi minne ijayo ndo uondoke. Unajua pia kwamba nakupenda sana Eve, usiniache tafadhali' Eli aliongea machozi yakichezacheza.

'Nisamehe Eli, ilikuwa bahati mbaya, hatukutarajia kuzaa mimi na wewe na vile vile siwezi kuendelea kujifanyiza kwamba nakupenda. Ni huruma tu ilionifanya nikukubalie. Siwezi kuolewa na wewe. Nisamehe tafadhali.'

Alibeba begi yake na kumbusu mtoto na halafu akaondoka na kuingia kwenye daladala na kutokomea mbali akimwacha mwanae Jacque na baba yake wakimlilia.

Mr Msofe alimfuata Eli na kumshika begani.

'Wewe ni mwanaume, jikaze. Unachotakiwa kufanya kwa sasa ni kutulia na kufikiri namna ya kumtunza Jacque. Usilie bwana.' Alimsisitiza!

Jacque akazidi kukua na kuongezeka kimo. Lakini miezi michache baadae matokeo ya Kidato cha nne yakawa yametoka. Elineema Urio akiwa kinara katika mkoa wa Tanga. Alitakiwa kujiunga na shule ya sekondari Ilboru kwa kidato cha tano. Kwa hali hiyo

ilimbidi kumuacha mwanae na kwenda shule ili kumuandalia maisha mazuri mwanae kipenzi…………...

MATEKA WA HUBA




PATA KIONJO CHAKE

**JIONI** ya saa mbili usiku. Giza limeshaingia lakini mwanga wa taa za umeme majumbani mwa watu na taa za magari barabarani unaniongoza kutembea mdogo mdogo ili kwenda kituo cha daladala, kuna kaumbali kidogo, kama kilometa moja na nusu hivi.

Natokea kwenye pati ya siku ya kuzaliwa ya rafiki yangu Janet, yeye anaishi mtaa wa uzunguni, wana pesa, magari, maduka makubwa ya kisasa, masupa maketi, kwa kifupi ni matajiri sana. Mtaa wao wa uzunguni unajulikana hivyo kwa sababu licha ya kuishi waafrika weusi tii, maisha wanayoishi hapo ni ya kizungu halisi.

Mimii.. Ah! Kusema ule ukweli, baba yangu huwa anatuambia eti tutakuwa matajiri hivi karibuni kama tulivyokuwaga zamani, eti safari hii tutakuwa matajiri zaidi sana. Nampenda baba yangu, hajawahi kusema uongo. Najua hivi karibuni tutakuwa matajiri kweli.

Naitwa Rose, Rose Sanga, nina miaka 16. Mimi, mdogo wangu Sajo, baba na mama, kwa sasa tunaishi mtaa wa uswazi, hapa jijini Mtu kwao.

Huku uzunguni kwa kina Janet, kuna utulivu Fulani hivi wa kuogofya. Kelele pekee zinazosikika muda huu ni za mbwa wakali wanaoshirikiana na walinzi wenye bunduki kulinda majumba ya matajiri, yenye kuta ndefu sana, ambazo juu yake kunaonekana nyaya za umeme, makamera ya cctv pia yametandazwa kila mahali. Sijawahi kuona watu waoga kama matajiri! Sijui wanaogopa nini?

Usiku huu napotembea mdogo mdogo kwa miguu yangu, nipo peke yangu! Marafiki wengine wa Janet wameshaondoka kwa magari yao, mimi tu ndio nimekuja kwa mguu na sasa narudi kwa mguu. Najua unajiuliza kwa mtoto wa uswazi mimi nimeanzaje kuwa rafiki na mtoto wa kishua Janet, nitakusimulia baadae!

Kwangu mimi, saa mbili usiku ni mapema sana, kule uswazi hata saa 6 usiku bado kunakuwa kama mchana tu. Nasikiaga kina Fatuma wao ndo kwanza kunakuwaga kunakucha. Wao wanafanya kazi  ya kuburudisha wateja wao kwenye magest na mabaa!

Nikiwa nusu ya safari kutoka uzunguni kwenda kituo cha daladala itakayonipeleka uswazi, ghafla, he! Si umeme umekata! Haki ya mama asikudanganye mtu, huku uzunguni kunatisha. Giza lilivyofunika ardhi, hata kama wewe ni jasiri kiasi gani, utaogopa tu? Na hivi kuna miti mirefu iliyoshonana kwenye barabara za mitaa, mamaa! Nywele zimesimama dede kichwani kwangu.

Najikaza kisabuni, nazamisha mikono yangu kwenye mfuko wa sketi yangu ili kutoa kisimu changu cha tochi! Naitoa na kubonyeza batani zake ili nipate japo mwanga wa kunifaa hapa ugenini kwenye kiza totoro! Dah siku ya kufa nyani walahi, inapowaka tu, inanipa mkono wa buheri, 'battery low, shutting down' maandishi yanasomeka na kuishilia, kamezima. Mamaa! Hofu inanivaa si kidogo, nasikia mapigo ya moyo wangu yanavyoenda kasi. Sioni kitu. Sioni kitu kabisaa!

Mara, nasikia kitu kama hatua za miguu za mwenda kwa miguu. Ka ka ka ka!!

'Nani mwenzangu?' napayuka kwa kwa kihoro. Kimya!

*Ka ka ka ka*! Hatua zinazidi kunisogelea. Kishindo kikubwa tofauti na cha awali. Mwili wangu unapata ganzi, nywele zinasimama wima kichwani.

'Haloo!' namudu kutamka kwa woga, ni kama tumbo la kuhara linanishika ghafla, miguu nayo, inagoma kuchukua hatua mbele au nyuma. Jasho, linanivuja si kidogo, sijawahi kuogopa namna hii!!

*Ko ko ko*!!

Hatua zimenifikia.

'Nani….' Simaliziii sentensi, nahisi kiganja cha mkono kikifunika mdomo wangu, mkono shujaa wa mwanamme, mguso wake tu unapenyeza maumivu yasiyo haba ubongoni mwangu. Nagugumia kwa maumivu nikijaribu kupiga kelele, sauti yangu inaishia kwenye wazo tu!

Nahisi kitu kikinitembea pajani, kimiminika cha vuguvugu, oh my God, siamini, siamini kama nimejikojolea.

Najaribu kufurukuta ili kujinasua mikononi mwa mvamizi wangu, siwezi. Ananikaba zaidi, Mungu jalia, nashuhudia mwanga wa gari ukija upande wetu, ni kama nguvu zinanijaa ghafla. Nakusanya nguvu zote nazoweza kumudu kwa muda huu ili kujinasua mikononi mwa adui yangu. Nanyanyua mguu wangu na kuukita kwenye ugoko wa huyu mtu. Nasikia ukelele wa maumivu, jamaa ananiachia na kusepa. Najaribu nimuone, lakini siwezi kumtambua. Kichwani kuna mzula, mwilini kapachika koti refu mithili ya jasusi la Kirusi.

Haraka sana naipungia gari iliyojitokeza mbele yangu mkono. Gari inasimama! 'Oh ahsante Mungu' natamka. Dereva anashusha kioo. Ni mzee mwenye umri, umri wa magharibi, labda sitini hivi! Mvi zimetaradadi kichwani mwake kama unga wa sembe.

Msaada tafadhali!' ndicho kitu nachomudu kutamka nikiwa nahema juu juu, nikijifuta jasho kwa kiganja cha

mkono wangu. Mzee hasemi kitu, anafungua mlango wa nyuma, nami najitoma ndani.

Ndani ya gari nalakiwa na marashi yenye harufu kali sana. Sijui nini kinaendelea, nachohisi ni kuishiwa pumzi, huku nuru ikinikimbia machoni mwangu. Kimya!

…

USIPANGE KUKOSA NAKALA YAKO.

DAVID NGOCHO anapatikana kwenye mitandao ya kijamii. Unaweza kufuatilia kazi zake huko pia.

Facebook: David Samson (King David), hii ni account binafsi. Pia utampata kwenye ukurasa wa facebook ujulikanao kama SIMULIZI ZA KING DAVID – NGOCHO au unaweza pia kuomba kujiunga na group la facebook lijulikanalo kwa SIMULIZI ZA KING DAVID (NGOCHO)

Instagram. Samdevy12

Twitter. David Ngocho.

Karibuni sana.